

KUFA UFUFUKO JAHANNAM

**Kimefasiriwa na kuhaririwa na:
Adam S. Kaoneka na Abdiin H. Kifea**

Harun Yahya

Dibaji

Kuandaliwa kwa Kitabu hiki kumelenga kumpa msomaji picha halisi juu ya maisha ya Jahannam. Jahannam inawakilisha tabaka za Moto wenye mwako mkubwa utakaobabua na kuunguza miili ya viumbe walioishi duniani kwa kukana na kukiuka maamrisha ya Muumba. Maisha ya Motoni ni adhabu watayokapewa watu na majini ambao matendo yao hapa duniani yalikuwa maovu ya ukafiri, shirki, udhalimu na ufisadi.

Kitabu hiki kinatoa picha ya jumla na ya kweli juu ya Jahannam ili kuwapa khofu na woga wale wote watendao maovu hapa duniani. Ukumbusho huu umekusudiwa, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, uwe msukumo wa kuyaeleka mema ili iwe tashiwishi kwa kiumbe ya kujiokoa kutumbukia Jahannam ambalo ni umbile lenye jiografia ya kutisha. Maudhui ya kitabu hiki yamelengwa kumjenga msomaji aweze kuepuka makatazo na kufuata maamrisha ya Mwenyezi Mungu(SW).

Dhana na taswira inayojengwa na maudhui ya kitabu hiki, ni njia za kumsaidia msomaji kuweza kuuchambua ukweli juu ya maisha haya. Inatarajiwa taswira hiyo iwe kichocheo cha kufanya utafiti wa kina ili kupata usahihi juu ya dhana, itikadi na maelezo mengi yatolewayo juu ya adhabu ya moto.

Kwa kuwa ufahamu juu ya maisha ya Motoni umezungukwa na hakika za kiimani, basi maelezo yaliyotolewa kitabuni humu yanawianishwa na maisha halisi ya ulimwengu huu. Kitabu hiki kumelenga kusaidia kumpa msomaji uhalisia wa kile ambacho amekuwa akikisikia na pengine kudhani na kuitakidi kuwa ni ngano au simulizi za watu wa zamani zisizo na uhalisia!

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aikubali jitihada hii, atusamehe upungufu wetu na atie Tawfiiq maudhui ya kitabu hiki yafahamike vyema ili sote tuweze kuishi kulingana na atakavyo Muumba tuweze kujiepusha na adhabu mbaya ya Motoni.

Abdiin Hussein Kifea

Box 90399

Dar es Salaam

Utangulizi

Kifo kinaweza kumkabili mtu wakati wowote. Nani ajuae, pengine huu ndio wakati wenyewe. Au, kinaweza kuwa karibu zaidi kuliko mategemeo yake.

Pengine kuidurusu mistari hii ndio fursa yake ya mwisho, ukumbusho wake wa mwisho au onyo la mwisho kwake kabla kifo hakijamkabili. Kwa kweli mja anayeendelea kuisoma mistari hii, hajui kama atakuwa hai baada ya saa moja kumalizika. Hata kama uwezekano huo po, lakini uwezekano wa lipi linalofuata uhakika huo hana. Yawezekana muda wake wa kuishi ukawa mfupi zaidi ya hapo kabla kifo hakijamkuta.

Uhakika wa kumaliza kusoma kitabu hiki pia hana. Kifo kwa hakika kinaweza kuwadia wakati wowote, muda mfupi kabla mwanadamu hajawa na fikra juu yake.

Kwa hakika mwanaadamu atakufa. Kama itakavyo kuwa kwa wale awapendao waliopita na wajao naye vivyo hivyo kifo kwake hakina budi. Miaka mia moja ijayo mwanadamu huyu hatakuwa na hata mmoja katika watu wa wakati huo anayemfahamu ambaye atasalia katika uso wa dunia.

Mwanadamu amekuwa anashughulishwa mno na malengo yahasuyo maisha yasiyo na ukomo katika bongo lake. Miongoni mwa malengo hayo ni kumaliza kidato cha sita, kuingia chuo kikuu, kumaliza chuo kikuu, kuwa na kazi yenye hadhi, kuoa au kuolewa, kulea watoto, kuongoza maisha yenye amani. Haya ni baadhi ya malengo yaliyo ya kawaida kabisa na ya jumla aliyonayo mwanadamu katika mipango yake. Mbali na haya, yapo mengine elfu na zaidi yanayoonesha hali halisi inayomzunguka mwanadamu.

Kifo ni moja ya mambo machache katika maisha ambayo kutokea kwake kuna uhakika wa asilimia mia moja. Baada ya miaka mingi ya kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, mwanafunzi anafanikiwa kuingia chuo kikuu, lakini mwanafunzi huyu anaaga maisha njiani akielekea darasani.

Mtu mwingine ambaye hivi karibuni tu ndio kaajiriwa afanye kazi, anapoteza maisha yake asubuhi ya siku ya kwanza wakati anaelekea kazini. Ajali ya barabarani nayo inamaliza uhai wa maharusi wawili ambao ndio tu wamo katika siku yao ya kwanza ya kufunga ndoa. Mfanyabiashara naye ambaye mambo yake yanamuendea vizuri, huonelea kusafiri kwa ndege ni njia bora ya kuharakisha mambo yake. Lakini, lililojificha ambalo halijui ni kwamba ni usafiri huo huo wa ndege ndio utakaofikisha tamati ya maisha yake katika ajali mbaya kupita kiasi na hivyo roho yake kunyakuliwa na kuwa mwisho wa uhai wake hapa duniani.

Katika hatua kama hiyo, mipango itakuwa haijatekelezwa. Kuiacha mipango nyuma, maana yake ni kuwa haitatekelezwa tena milele kwani mwanadamu amefikia kilele, mahali ambapo hawezi kurejea

tena kuja kuitekeleza. Hata hivyo, muhimu ni kuwa mwisho huu mwanadamu hakuupangilia. Kwa masikitiko makubwa, kwa miaka kadhaa, mwanadamu ametumia muda huo katika kuichambua na kuiweka sawa mipango ambayo tangu hapo haitakuja kutekelezwa tena. Zaidi mwanadamu huyu hakuchukuwa muda wake katika kuwaza lile ambalo kutokea kwake kwa hakika ni kwa asilimia mia moja.

Ni kwa njia gani basi mwanadamu ambaye mwenye busara na utambuzi wa hali ya juu atapangilia vipaumbele vyake? Hivi ataweka mipango yake kwa kuzingatia kile ambacho ana uhakika wa kutokea kwake au kwa kile ambacho hana hakika ya kutokea kwake? Wengi, imedhihirika, wamekuwa wakiweka vipaumbele katika yale malengo ambayo kuyatimiza kwake hakuna uhakika wa mia kwa mia. Bila kujali hatua ya maisha waliyonayo kwa wakati huo, utawaona bado wanaendelea katika kupanga mipango ya kuwa na kesho nzuri yenye kutimiza zaidi maisha yake ya mbeleni hapa duniani. Tabia hii itaonekana ya hekima zaidi, kama mwanadamu, sio kiumbe. Bado ukweli unasalia kwamba mipango yote hatima yake ni ule usio na kigeugeu, usio na shaka, nao ni ule unaoitwa kifo.

Hivyo sio busara kuacha kujali kifo, ambacho kutokea kwake kuna hakika badala yake kuendeleza juhudi kubwa na mazingatio kwenye mambo ambayo ama yanaweza kutokea au yanaweza yasitokee na kukamilika.

Hivyo, kutokana na kuwa na maneno yasiyoingia akilini ambayo bado yanatafuna fikra zetu, wanadamu tumeshindwa kuona jambo hili ambalo liko wazi mno.

Kwa hali hii, mwanadamu, hawezi kukamilisha taratibu za kuwa katika hali yao ya maisha halisi ambayo huanza mara baada ya kufa. Watakuwa si wenye kufanya maandalizi yoyote yale kwa ajili ya maisha hayo. Mara watakapofufuliwa, hawataongoza kuelekea popote zaidi ya Jahanam, mahali palipoandaliwa rasmi kwa ajili yao.

Madhumuni makuu ya kuandika kitabu hiki ni kumfanya mwanadamu atafakari juu ya jambo ambalo anajizuia kulifikiria na kumuonya juu ya jambo lililo na uhakika wa kutokea. Kuacha kulifikiria, kwa hali yoyote ile hakufanyi kuwa ndio kupatikana kwa suluhisho.

IMANI ZA KISHIRIKINA NA HAKIKA ZA UKWELI

Katika zama zote za historia, mwanadamu ameweza kufanikiwa kukabiliana na ama changamoto au tashiwishi mbalimbali za kimaisha. Lakini kifo kimebakia ni tatizo kwake na jambo lisiloepukika. Kila mmoja aliyewahi kuwepo katika dunia, bila kujali ni lini, alihitimisha maisha yake kwa kifo. Mwanadamu huishi hadi siku fulani kisha anakufa. Wengine hufa bado wangali wachanga, wengine hupitia hatua zote za maisha na kufariki dunia katika umri mrefu. Hakuna chochote anachomiliki mwanadamu, si vitu vyake, bahati, cheo, uwezo, watoto, ujasiri au mvuto wake unaoweza kuepusha kifo.

Bila ya upendeleo, wanadamu wote hawana cha kuwasaidia kuweza kuwaepusha na kifo na hali itabakia hivyo. Wengi katika watu hujizuilia kufikiria kifo. Haiwapambanukii kwao kwamba mwisho huu yaani kifo lazima siku moja utawakuta tu. Wanajenga fikra za imani za kishirikina kwamba, kama watajizuilia na fikra juu ya kifo, basi itakuwa kinga kwao juu ya kifo. Yanapofanyika majadiliano ya kila siku, wanaoleta mjadala juu ya kifo huzuiliwa na wenzao. Mwingine mwenye kuanza mazungumzo juu ya kifo, kwa kukusudia au bila kukusudia, na kurejea dalili za Mwenyezi Mungu, japo kwa kiwango kidogo tu, huibua wingu zito la kutokuwa na mwelekeo uliotanda katika macho ya watu.

Hata hivyo, wengi katika watu wanaofanya udanganyifu ndio njia yao ya maisha, hukosa utulivu wakati ukweli huu ‘unaowachukiza’ unapowasilishwa kwao.

Bado, jinsi wanavyojitahidi kuweka fikra zao juu ya kifo, ndivyo hivyo hivyo kifo nacho kinavyozidi kuwanyemelea karibu. Hali yao hiyo ya kutawaliwa na shetani (kumfanya ndiye mlinzi wao) kutadhihirisha ni kwa kiwango gani watataharuki na kutishwa na hali ngumu watakayokabiliana nayo wakati wa kifo, siku ya hukumu na katika adhabu ya milele.

Muda hufukuzana na mwanadamu. Je, mwanadamu amewahi kusikia mtu aliyezuia asizeeke au kufa? Au, mwanadamu anamjua mtu yeyote ambaye hatakufa? Hili si rahisi kupatikana. Haiwezi kupatikana kwa sababu mwanadamu hana ushawishi wa namna yoyote ile kuhusu mwili wake au maisha yake. Kwamba yeye mwenyewe hana maamuzi juu ya hata kuzaliwa kwake, kufanya jambo hili liwe wazi zaidi. Ushahidi mwingine ni pale mwanadamu anapokata tamaa katika kukabili kifo. Mmiliki wa uhai ndiye aliyempa mwanadamu uhai huo. Na hivyo pindi akipenda, huuchukua kwake. Mwenyezi Mungu, mmiliki wa uhai, anamfahamisha mwanadamu juu ya hili katika aya aliyomfunulia Mtume wake:

“Nasi hatukumfanya mwanadamu yeyote wa kabla yako aishi milele. Basi kama ukifa wewe, wao wataishi milele? (Al-Anbiyaa:34)

Kwa wakati huu, wapo mamilioni ya watu waishio ulimwengu mzima. Kutokana na hili tunahitimisha kwamba, idadi ya watu isiyo na hesabu wamekuwepo na kutoweka tangu kuumbwa mwanadamu wa kwanza kutokea duniani. Wote wamekufa bila ubaguzi. Kifo ni mwisho ulio hakika kabisa; kwa watu waliotangulia na wale ambao kwa sasa wako hai. Hakuna hata mmoja anayeweza kuepuka kifo. Kama Qur'an inavyohibitisha hili:

'Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtalipwa ujira wenu kamili kamili siku ya kiama. Na aliyewekwa mbali na moto na kuingizwa Peponi, basi amefuzu. Na maisha ya dunia hii si kitu ila ni starehe idanganyayo. (Al-Imraan:185)

KUDHANIA KIFO NI JAMBO LA BAHATI NASIBU AU BAHATI MBAYA

Kifo hakitokei kwa bahati nasibu. Kama ilivyo kwa matukio mengine, hutokana na mpango wa Mwenyezi Mungu. Kama ilivyo kuwa tarehe ya kuzaliwa mtu imekwisha pangwa, ndivyo hivyo hivyo kwa tarehe na sekunde atakayokufa.

Mwanadamu anaharakishia kwenye mwisho wake, nyuma zikipita saa na dakika alizopewa kuishi. Kifo cha kila mmoja, mahali kitakapotokea na wakati, na pia namna mtu atakavyokufa, vyote vipo katika Qadar ya Mwenyezi Mungu, (au Mpango wa Mwenyezi Mungu).

Mbali na hili, watu wengi hudhania kuwa kifo ndio hatua ya mwisho katika mlolongo wa matukio, wakati ambapo sababu halisi anayezijua ni Mwenyezi Mungu peke yake. Kila uchao, habari za kifo katika vyombo vya habari kama magazeti, redio na runinga ndizo zinazotawala. Baada ya kusikiliza na kusoma taarifa hizi, pengine utasikia hoja za baadhi ya watu wajinga wakisema:

“Angenusurika kama tahadhari muhimu zingechukuliwa”

“Asingekufa kama hili na lile lingefanyika.”

Hakuna sekunde inayoongezwa au kupunguzwa katika maisha ya mtu zaidi ya muda ule alioandikiwa na Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, watu ambao wako mbali na ufahamu utokanao na imani, hukitazama kifo kama moja ya matukio ya bahati nasibu. Ndani ya Qur'an, Mwenyezi Mungu ametahadharisha waumini dhidi ya hoja iliyopindishwa namna hii ambayo kimsingi ni maalum kwa Makafiri:

“Enyi Mlioamini msiwe kama wale waliokufuru na wakasema juu ya ndugu zao waliposafiri katika nchi au walipopigana: ‘Kama wanalikuwa kwetu wasingalikufa wala wasingaliuwawa. Mwenyezi Mungu atawafanya wawe ni wenye kujutia maneno yao hayo katika nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuhuisha na kufisha. Na Mwenyezi Mungu anaona yote mnayoyatenda. (Al-Imraan: 156).

Kudhania kuwa kifo ni bahati nasibu ni ujinga ulio wazi. Kama aya hapo juu inavyobainisha, hili husababisha kuporomoka kwa imani na matatizo yasiyozuilika kwa mwanadamu.

Kwa makafiri au wale wasio na imani kwa mtazamo wa Qur'an, suala la kuondokewa na ndugu au yule unayempenda ni sababu tosha ya kukata tamaa na huzuni kubwa katika nafsi yake. Kitendo cha kukioanisha kifo na mkosi au balaa, watu hao hufikiri kuwa ni njia mbadala ya kukiepuka kifo.

Haya ni maamuzi ambayo hatima yake ni kuwafikishia majuto na maangamizi. Maangamizi na majuto haya si lolote zaidi ya kule kutokuamini kwake. Hata hivyo kinyume na mtazamo wa makafiri ulioainishwa hapo juu, ukweli ni kwamba kifo hakisababishwi na ajali, wala maradhi wala kingine chochote. Kwa hakika ni Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba sababu zote hizi. Pindi muda uliowekwa kwa ajili yetu unapokamilika, maisha yetu hukoma kwa kupitia hizi sababu zinazoonekana kwa nje kuwa ndio chanzo hasa. Wakati huo huo, hakuna kinga yoyote ya kimaada inayoweza kumuokoa yeyote kutoka katika kifo na kuleta uhai mwingine. Mwenyezi Mungu anaonesha kanuni hii yake katika aya ifuatayo:-

‘Na nafsi yoyote haitaweza kufa ila kwa amri ya Mwenyezi Mungu kwa ajali iliyopangwa... (Al-Imraan:145).

Muumini ana hakika juu ya maisha ya dunia hii kuwa ni ya muda tu. Anajua kuwa Mwenyezi Mungu, aliyemzawadia kila jema linalopatikana hapa Ulimwenguni, siku moja ataichukuwa roho yake katika mahali na muda alioupanga ili amuhesabu matendo yake. Hata hivyo kwa kuwa katika uhai wake wote ametumia neema za Mwenyezi Mungu, hakuwa ni mwenye kuhofia kifo. Mtume Muhammad (reheema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake) aliurejea mwenendo huu mwema katika moja ya dua zake kwa kusema:-

‘Hakika Swala yangu, kujitoa kwangu Muhanga, uhai wangu, kifo changu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Bwana wa Ulimwengu.’

Hadithi hii ilisimuliwa na Jabir bin Abdallah na kunukuliwa na At-Tirmidh, hadith namba 262.

KUELEWEKA VIBAYA KWA QADAR

Watu wengi wameendeleza mitazamo potofu kuhusu Qadar, hasa kama suala lililoko mbele yao ni kifo. Mawazo yasiyo na mashiko kama kusema ‘Mtu anaweza kuishinda qadar yake’ au ‘mtu anaweza kubadili yaliyomo katika Qadar’ yameenea mno. Kuchukulia matazamio yao na dhana zao kuwa ni Qadar, watu ambao si werevu na ambao ni wajinga huamini kuwa ni Qadar ndiyo iliyobadilika pindi tukio linapokwenda kinyume na matarajio yao au utabiri wao.

Wanadhani bila ya kutumia busara na kutenda kama vile wamesoma Qadar kabla na kwamba matukio hayakwenda sawa na vile walivyosoma. Upindishaji na kukosekana kwa mfuatano mzuri kiasi hicho, ni matokeo ya uelewa finyu unaokabili utoshelezaji wa ufahamu juu ya Qadar.

Qadar ni mpango wa Mwenyezi Mungu unaohusu uumbaji kamili wa matukio yote yaliyopita na yanayokuja bila ya kuwekewa mipaka ya muda. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba dhana ya muda na nafasi bila ya maada yoyote, ndiye anayemiliki wakati na nafasi na hawekewi pingamizi na chochote kati ya hiyo. Mfuatano wa matukio ambayo yametokea kabla au yatakayotokea mbeleni, ni hatua kwa hatua, yamepangwa na kuumbwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba muda, hivyo hufungwi nao. Vivyohivyo, kwamba anafuata matukio ambayo yeye mwenyewe ameyaumba pamoja na yule anayeyatenda haikubaliki kiakili. Kwa mnasaba huu, hakuna haja ya kusema kwamba Mwenyezi Mungu hasubiri kuona namna tukio litakavyokamilika. Katika utaratibu wake vyote mwanzo na mwisho wa tukio viko wazi mno. Hali kadhalika, hapana shaka kwamba ni wapi tukio hili lipo katika mfumo mzima wa umilele. Kila kitu kimeshafanyika na kimekwisha. Hii ni sura ya picha katika mkanda wa filamu kama ambavyo picha haiathiri chochote katika mkanda na kumbadili, vivyo hivyo mwanadamu ambaye ana nafasi yake katika utendaji wa maisha hawezi kubadili mlolongo wa matukio uliorekodiwa na kuhifadhiwa katika mkanda wa Qadar. Wadamu hawana lolote wanaloweza kubadili katika Qadar. Kinyume chake, ni Qadar ndiyo kigezo katika maisha ya watu.

Mwanadamu, ambaye ni mmoja katika mpango mzima wa Mwenyezi Mungu, kamwe hawezi kutoka na kuwa nje ya mpango huo. Si tu kwamba hawezi kuibadili Qadar, vivyo hivyo hawezi kwenda nje ya mipaka iliyo katika Qadar. Kwa uelewa mzuri zaidi; mtu anaweza kuoanisha baina ya mtu na muigizaji katika mkanda. Muigizaji hawezi kujitoa nje ya mkanda, na kuwa mwigizaji halisi na hivyo kuanza kubadili katika filamu kwa kuondoa matukio ambayo hayampendezi au kwa kuongeza matukio mapya. Kwa hakika hili litakuwa ni wazo ambalo halikubaliki kiakili.

Kwa mtazamo huo, dhana kwamba mtu anaweza kuishinda Qadar au kupindisha mfuatano wa matukio yaliyo katika Qadar ni upuuzi mtupu. Yeyote anayesema ‘Nimeishinda Qadar’ hana zaidi ya

kujidanganya mwenyewe na ukweli kwamba amefanya hivyo ndio Qadari iliyoko juu yake. Elimu na taaluma ya Qadari iko nje ya ufahamu wa Mwanaadamu.

Mtu anaweza kuwa mahututi kwa siku kadhaa. Inaonesha kwamba yaelekea hataweza kurejea tena na kuwa buheri wa afya. Hata hivyo, pindi atakapokuwa amepona, hii haina maana kwamba ‘ameishinda hatima yake, au ‘madaktari wamebadili hatima yake’. Kwa wepesi kabisa hii inaashiria kwamba muda wake wa kuishi bado haujakwisha. Kurejea kwake katika afya njema si chochote zaidi ya dalili kuwa hawezi kukwepa mwisho wake, yaani kifo. Mwisho wake ni sawa na wanadamu wengine mbele ya mpango wa Mwenyezi Mungu:-

“Na mwenye kupewa umri hapewi umri zaidi wala hapunguziwi umri wake kuliko ule ulioandikwa katika kitabu. Bali haya ni sahali kwa Mwenyezi Mungu (Al-Fatir:11)

Mtume Muhammad (SAW) katika kitabu cha Imam Muslim - Sahih Muslim hadithi namba 6438 amesema yafuatayo kwa Muumin ambaye amemuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amuwezeshe kunufaika kutoka kwa ampendae. ‘Umeomba kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya umri ambao tayari umekwishapungua, na urefu wa masiku ambayo tayari yako kwenye mpango na kuendeleza fungu ambalo fungu lako tayari limekwisha kukadiriwa. Mwenyezi Mungu hafanyi chochote ama kukatisha au kukichelewesha kwa muda ambao umekwisha kadiriwa.’ Hali kama hizo ndiyo njia ambazo Mwenyezi Mungu anamdhihirishia mwanadamu elimu yake isiyo na ukomo, busara zake, aina na rehema zilizorithishwa viumbe vyake na pia njia anayotumia kumjaribu Mwanadamu. Aina kama hizo za mifano iliyotolewa hapo juu huongeza kuridhishwa kwake, kustaajabu na hali ya kipekee katika Imani za waja wake.

Kwa upande wa makafiri, wao kinachoongezeka ni hisia kati ya mashaka, kukerwa na kurejea nyuma katika maovu. Kinyume na matarajio yao yaliyojengeka katika ujinga wa kiakili hupelekwa watu hawa wawe na fikira za kuwa waasi zaidi kwa Mwenyezi Mungu. Wakati huo huo, ufahamu wa waumini juu ya kundi hili linaloendelea kubobea katika maasi, wao huzidi kumshukuru Mola wao kwa kuwaridhia kuwa na Imani na busara, vitu ambavyo huwafanya wawe bora kuliko makafiri.

Kutokana na ‘kipande cha busara’ kilichopokelewa toka kwa kundi la wenye shaka juu ya Qadar, kifo cha mtu mwenye umri wa miaka 80 na zaidi ni ‘Qadar’ lakini anayekufa akiwa bado mtoto mchanga au mwenye umri wa kati ni kitendo cha kuhuzunisha. Kifo kitahesabika ni kitendo cha kawaida kwao wao kama kitawafikiana na matakwa yao. Kwa mfano, mtu anapougua kwa muda mrefu, kifo kinaonekana kukubalika. Lakini kama mtu ameugua ghafla au kutokana na ajali mtu akafariki dunia, hilo ni janga lisilotegemewa. Ndio maana watu wengi hukutwa na kifo hali ya kuwa wanakichukia huku wakidhihirisha uasi wao kwa Mwenyezi Mungu.

Tabia hii ni wazi kwamba muhusika amekosa imani juu ya Qadari na hivyo juu ya Mwenyezi Mungu. Hao wanaonawirisha fikra hizo vichwani mwao wameandaliwa maisha ya fedheha na shida katika maisha haya. Kwa hakika huu ni mwanzo tu wa adhabu ya milele ambayo ni matokeo ya kukosa imani.

IMANI KUWA ROHO HUENDA KUISHI KWENYE MWILI MWINGINE BAADA YA KIFO

Moja kati ya imani potofu inayoshikiliwa na watu kuhusu kifo ni ile inayodai kuwa ‘Kuna uwezekano wa roho ya mtu kupachikwa katika mwili mwingine na kuendelea kuishi hapa hapa duniani. Tafsiri ya maneno hayo ni kuwa kifo kinapomkabili mtu, mwili ndio hufa, lakini roho yake ama huhamishiwa katika mwili mwingi au huzaliwa upya katika mwili mwingine kwa nembo tofauti kwa wakati na mahali pengine. Hivi karibuni, hali hii imekuwa mkakati unaovutia wengi miongoni mwa makafiri na wafuasi wa Imani za Kishirikina.

Katika mtazamo wa kitaalam, sababu zinazochukuliwa kuwa ndio hasa zinazozusha imani hizi za kishirikina kuungwa mkono - (bila ya kuwa na hoja madhubuti) ni ile hali ya wasioamini wanayoifanyia kazi. Kwa kukosa kwao imani juu ya Akhera, watu wanahofia kurejeshwa na kuwa si chochote baada ya kifo. Wale wenye imani dhaifu, kwa upande mwingine, hukosa utulivu juu ya fikra kwamba kuna kupelekwa motoni kwani wanafahamu, au walau, wanafikiria kwamba kutokana na Mwenyezi Mungu alivyokuwa muadilifu, wao hawana makazi mengine zaidi ya motoni.

Kwa yote mawili, kuhofia kurejeshwa kuwa daraja la chini, na kukosa utulivu juu ya kupelekwa motoni, wazo la kuzaliwa upya kwa roho katika mwili mwingine katika zama tofauti na mahali pengine linaonekana ndilo lenye uwezekano mkubwa. Hivyo, kundi fulani lililobuni fikra hizi hasi limefanikiwa kuwachota watu na kuamini uongo huu kwa msaada wa muono finyu wa mawazo. Ya kwamba wafuasi wao hawahitaji ushahidi zaidi na hivyo kuwapa nguvu ya kuzidisha undumila kuwili wao.

Kwa bahati mbaya, imani hii potofu imepenyezwa ndani ya mduara wa Waislamu. Waislamu hawa wengi wao ni wale ambao wanaghera ya kukuza taaluma na uhuru wa kujiona. Kuna mtazamo mwingine kuhusu hili unaohitaji kudokezwa: Watu hao hufafanua mambo yao na kutoa ushahidi kutoka katika kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa tafsiri yao. Kwa hili, wanapindisha maana iliyo wazi ya aya za Qur’an na kubuni tafsiri yao. Lengo hapa ni kusisitiza kwamba imani hii iliyopinda ni kinyume kabisa na Qur’an na Uislamu wa aina hiyo kwa ujumla unapingana na aya za Qur’an ambazo kwa hakika ziko wazi mno na zenye kueleweka.

Makundi haya hudai kwamba zipo aya chache ndani ya Qur’an ambazo zinafungamana na mawazo yao hayo potofu. Miongoni mwa aya hizo ni:

‘Watasema, “Mola wetu! umetufisha mara mbili na umetuhuisha mara mbili! Basi tunakiri dhambi zetu. Basi je, iko njia ya kutoka?” (Al-Muumin:11).

Kwa mnasaba wa aya hii waumini wa nadharia ya kuzaliwa katika kiwiliwili kingine hutoa ufafanuzi kama ifuatavyo:

Mwanadamu amepewa maisha mengine baada ya kuishi katika maisha hayo kwa muda na kisha kufariki dunia. Hii ni mara ya pili anayofanywa kuwa kiumbe tena na pia ndicho kipindi ambacho roho yake inakamilika. Hadai kwamba, ni baada ya kifo kinachofuatiwa uhai huu wa mara ya pili, ndipo mtu atafufuliwa akhera.

Kama mtu atajiepusha na uegemezi wa fikra na kuamua kuwa huru, uchambuzi wa aya hii utakuwa kama ifuatayo:

Kutokana na aya ni dhahiri kuwa mwanadamu hujuta katika hatua mbili za uhai na vifo. Kwa mnasaba huu, kwamba kuna uhai wa mara ya tatu au kifo cha mara ya tatu hakina nafasi hapa.

Kama hali ndio hii; swali moja huja katika akili: ‘Ni ipi kati ya awali ya mwanadamu? Kuwa hai au kuwa mfu? Jibu lake linapatikana katika aya ifuatayo:

“Vipi mnamkanusha Mwenyezi Mungu, na hali mlikuwa wafu, akakuhisheni kisha atakufisheni, kisha atakuhisheni? Kisha kwake mtarejeshwa?” (Al-Baqara:28)

Aya inajieleza yenyewe na kujitosheleza; awali, mtu alikuwa mfu. Kwa maneno mengine, kwa namna mwanadamu alivyoubwa, alianza na vitu ambavyo havina uhai kama vile, maji, udongo na kadhalika kama aya zinavyobainisha. Kisha, umbo hili litokanalo na vitu visivyo na uhai vikapewa uhai, ‘akauumba na kuupa sura’. Hiki ndicho kifo cha kwanza na hivyo uhai wa kwanza kutoka kwenye umaiti.

Kisha, baadhi ya huu uhai wa kwanza kutoka kwenye umaiti, uhai hukoma na mwanadamu hufa tena. Anarudi katika udongo tena kama ilivyokuwa katika hatua ya awali na anarudishwa na kuwa si chochote. Hii ni hatua ya pili ya mpito kuelekea katika kifo. Hatua ya pili na ya mwisho ya mtu kufufuliwa kutoka katika umaiti itatokea Akhera. Kwa kuwa hali iko hivi, hii ingelazimisha kuwepo na mfufuko wa tatu. Hata hivyo hakuna aya hata moja inayoainisha kuwepo kwa mfufuko wa tatu.

Ukizingatia aya zilizokuliwa hapo juu, yaani Al-Muumin:11 na Al-Baqara:128 hakuna inayogusia kuwepo kwa mfufuko wa mara ya pili katika dunia hii. Kwa upande mwingine, aya hizi zinadhahirisha juu ya kuwepo mfufuko wa kwanza duniani na wa pili Akhera.

Cha kusikitisha wanaoamini juu ya uhai zaidi ya mara moja hapa hapa duniani egemeo lao ni katika aya hizi mbili tu. Aya ambazo, badala ya kuthibitisha ufufuo wa pili hapa duniani zinakanusha uwezekano wa kuwepo kwa hali hiyo. Kwa nyongeza, aya kadhaa ndani ya Qur’an zinabainisha wazi

kwamba kuna uhai wa mara moja tu hapo duniani ambao mwanadamu yuko katika mtihani na kwamba hakuna kurejea tena duniani baada ya kifo. Hili limebainishwa katika aya ifuatayo:

‘Hata yanapomfikia mmoja wao mauti, husema ‘Mola wangu! Nirudishe (ulimwenguni) ili nifanye mema sasa badala ya yale niliyoyaacha! (Ajibiwe) ‘Haiwezekani! Kwa hakika hili ni neno tu analolisema yeye; na mbele yao kuna maisha ya baada ya kufa mpaka siku ya kufufuliwa. (Al-Muuminun:99 - 100).

Majadiliano yaliyo katika aya hizi, ni ushahidi kuwa baada ya kifo cha pili hakuna tena kurejea katika dunia hii. Kwa upande mwingine, aya hii inatufahamisha kwamba katika hali ya kukata tamaa, makafiri watatamani wapewe uhai wa mara ya pili hapa hapa duniani kabla ya ule wa Akhera ili warekebishe mwenendo wao. Aya inabainisha kuwa hilo ni muhali tena bali wasubiri ufufuo wa pili utakaokuwa Akhera, tayari kwa malipo ya matendo ya wanadamu wote, kila mmoja na hesabu yake.

Kuhusu watu wa peponi na watu wa motoni pia baada ya kufufuliwa Akhera, watu wa peponi: ‘Humo hawajaonja mauti ila mauti yale ya kwanza, na atawalinda na Adhabu ya Jahannam. Kwa fadhila zitokazo kwa Mola wako; huko ndiko kufuzu kukubwa. (Ad-Dukhan:56 - 57). Kuhusu watu wa motoni: ‘Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema kwanini? Kwa haki ya Mola wangu ninyi lazima mtafufuliwa; kisha lazima mtajulishwa mliyoyatenda. Na hayo ni sahali kwa Mwenyezi Mungu. (Taghaabun: 7.) Na walisema: Haukuwa (uhai) ila ni uhai wetu huu wa dunia, tunakufa na tunaishi, wala hakuna kinachotuangamiza ulimwengu; lakini wao hawana elimu ya hayo wanadhani tu (Al-Jathiyah:24)

‘Je sisi ni wenye kufa tena? Ila kifo chetu cha kwanza! Wala sisi hatutaadhibiwa? Kwa hakika huku ndiko kufuzu kukubwa.’ (As-Saaffah:58 - 59).

Baada ya aya hizo, wazo au nafasi ya maswali zaidi kuulizwa inakuwa haipo. Kwa kuukamilisha mjadala huu ni kwamba, pamoja na umauti kutajwa kuwa ni mara mbili, lakini kifo atakachohisi mwanadamu ni kimoja tu, kile ambacho hufuatia baada ya uhai wa hapa duniani. Wakati huo mwanadamu anakuwa na hisia zote na kufahamu kila linalotokea. Kifo cha kabla ya uhai wa duniani mwanadamu huwa hana analotambua.

Kwa mtazamo huu, kushikilia kuwa roho huhama na kuvikwa kiwiliwili kingine cha mnyama au mwanadamu mwingine na kuendelea kuishi hapa duniani, au kwamba kuna kufa zaidi ya mara mbili, ni dhana ambazo hazina lengo jingine zaidi ya kumkanusha Mwenyezi Mungu na Qur’an.

Hali kadhalika, kama Mwenyezi Mungu ameumba mfumo wa maisha ambao moja ya matukio ya mfumo huo ni roho kuhamishiwa katika kiwiliwili kingine na kuendelea kuishi hapa hapa duniani, asingesita kumtambulisha hilo mwanadamu katika muongozo aliouleta yaani Qur’an. Aya za Qur’an

zinaanisha uhai wa namna mbili tu. Wa kwanza ni huu wa hapa duniani, na wa pili ni ule wa baada ya huko Akhera.

‘Yeye ndiye aliyekuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga; kisha mkafikia wakati wa nguvu zenu kamili; kisha muwe wazee. Na wengine katika ninyi hufishwa kabla (ya kufikia uzee au ujana au utoto). Na ili mfikie muda uliowekwa ili mpate kufahamu. Yeye ndiye anayehuisha na kufisha; na anapolihukumia jambo (liwe), basi (mara moja tu) huliambia ‘kuwa’ nalo likawa (Al-Muumin: 67 - 68).

‘Na kwa yakini wale wanaozisopotoa aya zetu (ili wasizifuate na wapoteze wengine) hawatufichiki. Je! atakayetupwa motoni ni bora au atakayetajwa kwa amani siku ya kiama? Fanyeni mnayopenda, kwa yakini yeye anayaona yote mnayoyatenda. (Haa mym Sajidah (Sussilat):40).

PAZIA LA KUGHAFILIKA AU KUKOSA MUELEKEO AU KUKOSA MALENGO

Kimaumbile binadamu ni mbinafsi; hisia zake huwa kali pale mambo yake ya kimali na mambo mengine ya kimaisha hususan ya kivotu yanapoguswa. Kimaumbile, mwanadamu huhidhihirisha kuwa haafikiani na masuala ya kifo, ambayo kimtazamo kuonesha kuwa jambo hilo linahusu watu wachache. Hali hii ya kutokuwa makini kifika na hivyo mja kuyumba na kukosa pa kushika, Mwenyezi Mungu ameziita *'Ghaflatin'*. Yaani *'Mghafala' Kughafilika*.

Maana ya *'kughafilika'* ni ile hali ya kushindwa kufikia muafaka katika maamuzi na hivyo kushindwa kuyaenda mambo ipasavyo kutokana na upungufu alionao mwanadamu katika utambuzi au hali ya kukosa utambuzi kabisa. Mfano wa kughafilika au kukosa muelekeo imeelezwa katika aya ifuatayo:-

'Imewakaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala wanakengeuka tu, (wanapuza)'. (An-biyaa: 1)

Hisia zilizojengeka miongoni mwa watu ni kwamba yeyote aliyeathirika kutokana na maradhi mabaya basi atakufa. Ukweli ni kwamba, wote wawili, aliyeathiriwa na ugonjwa wa yule aliyejenga hisia kuwa mwenzake atakufa, wote watakufa. Suala ni lini litatokea leo au kesho au baada ya miaka kadhaa, halibadili ukweli huu. Mara nyingi yule aliyeathirika hupuuza ukweli huu. Kwa mfano, inamkinika kwamba yule aliyeathirika na virusi vya UKIMWI - HIV – atakufa muda si mrefu. Lakini ukweli unabaki kuwa hata yule ambaye ana nguvu aliyejirani na mgonjwa – kama ukweli utasemwa siku moja isiyo na jina naye atakufa. Pengine umauti wake unaweza kumjia kabla ya aliyeathiriwa vibaya na maradhi yatokanayo na virusi vya UKIMWI. Hali hii inaweza kumtokea wakati wowote bila ya kutarajia.

Watu wa familia huhuzunika jirani na kitanda cha mgonjwa. Lakini hawajihuzunikii wenyewe ambao kwa vyovyote siku moja watakufa. Hata hivyo, kutokana na uhakika wa tukio lenyewe la kifo, haitegemewi upokeaji wa tukio uhilitilifiane ama kwa kifo kuwa jirani au kuwa muda mrefu ujao kabisa huko.

Kama kusikitika na kuhuzunika ndio njia sahihi katika kukabiliana na kifo, basi kila mmoja angeanza kujisikitikia au kujihuzunikia yeye mwenyewe kisha kwa ajili ya mwingine. Au ni busara akabiliane kwa kuishinda hali ya kusikitika na kuhuzunika kwake badala yake afanye juhudi katika kuwa na uelewa wa kina juu ya kifo.

Kwa hitimisho hili, kujua sababu zinazosababisha mtu aghafilike itakuwa ni muhimu.

VYANZO VYA WATU KUGHAFILIKA NA KUKOSA MWELEKEO

Kwanza, kutokana na kukosa maamuzi mazuri kutokana na kukosa uelewa na busara.

Watu wengi ndani ya jamii hawajishughulishi katika kufikiria mambo muhimu yanayohusu maisha yao. Mfumo wa maisha wa kundi hili la watu ni kughafilika. Yaani mfumo wao wa maisha ni ule mfumo uliosahau kuwa kuna leo na kesho. Watu hawa huwaza zaidi mambo ambayo si katika vipaumbele huku wakidai kuwa kuwaza ambayo hakuna wavunacho leo ni kupoteza muda kwani wao wametingwa. Ni kwa mnasaba huu kwamba hata wazo kuhusu kifo ni miongoni ya mambo yanayopoteza muda. Wao shughuli kubwa ni kufikiri zaidi matukio yaliyojitokeza badala ya kufikiri mambo ya msingi katika maisha.

La kusikitisha ni kwamba, inapotokea mada juu ya kifo inajadiliwa, kujiridhisha kwa kutoa hoja butu na wanapoelemewa kihaja, badala ya kuunga mkono na kuhisi hoja, wao hujitenga wasiendeleo kusikiliza. Muda wote hufikiria mambo madogo madogo ya kimatukio.

Pia, hutokana na mkanganyiko na uhalisia wa maisha. Maisha yaenda kwa kasi mno huku yakiwavutia watu wengi. Kama juhudi ya makusudi haitafanyika, ni dhahiri kuwa kifo kinaweza kusababisha. Kusahau huku hakuondoi ukweli kwani ni lazima kifo kitatokea ama muda mfupi tu ujao au baada ya miaka kadhaa. Kukosekana kwa imani juu ya Mwenyezi Mungu, wengi wao huwa mbali na mitazamo mingi juu ya yale ya Mwenyezi Mungu. Mifano hai ni kama ifuatavyo: Qadar, kumtegemea Mwenyezi Mungu, na kujisalimisha kwake. Huwa anapigania zaidi mahitaji ya kimaada na kupigania maisha mazuri duniani. Kamwe muda wa kujishughulisha na maandalizi ya kifo hana. Dunia imemzonga. Tahamaki kifo kimewadia. Anatamani apewe muda zaidi kwa kujutia aliyoyafanya, lakini hayupo wa kumsaidia tena.

Tatu, kughilibika kutokana na ongezeko la watu

Moja ya sababu inayosababisha watu kughilibika na kukosa mwelekeo ni kuongezeka kwa vizazi. Idadi ya watu duniani imeendelea kuongezeka kamwe haipungui. Maisha yanapokolea utamu, mwanadamu hudhani kuwa hiyo ndiyo hatima ya maisha. Humpa hisia za kuweza kutamka kuwa ‘nyota njema huonekana asubuhi’, ‘Vizazi vimeziba pengo la kifo’ Kwa kuona kuwa hakuna tatizo kwani kama aliyekufa ni mmoja na waliozaliwa ni watatu, tatizo liko wapi?’ Fikra kama hizi humpa mwanadamu ujasiri wa kidhalimu na kifisadi wa kutojali kifo. Hata hivyo kuanzia sasa, kama hakutakuwa na vizazi tena, bado tutashuhudia kifo kimoja baada ya kingine na hivyo idadi ya watu kupungua. Kifo kitaanza kuonekana kwamba ni janga kuu. Mtu atianza kuona watu wanaomzunguuka kwanza kutoweka mmoja baada ya mwingine. Hili litaleta hisia kwamba mwisho usioweza kuzuilika utamkabili tu. Hii ni sawa na wale walio katika mstari wa kusubiri adhabu ya kifo. Kila siku wanashuhudia watu wawili au mmoja

wakipungua kwa ajili ya kupelekwa kukamilisha adhabu. Idadi ya watu katika Selo za gereza inazidi kupungua kila uchao. Jinsi siku zinavyozidi kuyoyoma, ndivyo hivyo hivyo wale walio hai gerezani, hulala na hali ya wasiwasi kwamba huenda siku inayofuata ni zamu yao. Kamwe hawawezi kusahau kifo, hapo kwa sekundi hivi.

Kimsingi, uhalisia wa mambo hautofautiani sana na maelezo ya mfano huu. Anayezaliwa sasa, hana athari zotote kwa yule aliyemkuta duniani kuhusu kifo chake. Hili ni suala lililoleweka vibaya tu kisaikolojia miongoni mwa baadhi ya watu. Watu waliokuwepo miaka mia moja na hamsini iliyopita katika uso wa dunia hii, leo hawapo – Vizazi vilivyofuata nyuma yao havikuweza kuwakinga na kifo. Vivyo hivyo miaka mia moja ijayo kuanzia sasa, ukiondoa wachache, waliopo katika uso wa dunia hii hawatakuwa hai tena. Hii ni kwa sababu dunia sio Mahali pa kudumu kwa mwanadamu.

NJIA YA MWANADAMU YA KUJIPA MATUMAINI NA KUJIRIDHISHA

Pamoja na sababu zinazopelekea watu kutotilia maanani kifo na hivyo kujitumbukiza katika kughafilika, zipo njia kadhaa anazojihami nazo mwanadamu ili kujiliwaza. Njia hizo ambazo baadhi zitaelezwa hapa chini, humrudisha mwanadamu kuwa sawa na mbuni. Mbuni hufukia kichwa chake katika mchanga ili kujihami katika mazingira ya hatari.

Mosi, kuahirisha kufikiria kifo mpaka miaka ya baadaye katika uhai. Watu kwa kawaida hudhania kuwa wataendelea kuishi hadi watakapofikisha umri zaidi ya miaka sitini au sabini. Hali hii ndio inayotanabahisha sababu zinazopelekea vijana na watu wa makamo kutumia njia hii katika kujihami. Kwa kupiga mahesabu kama hayo kichwani, tafakari juu ya kifo huahirishwa hadi hapo baadaye.

Katika ujana wao au umri wa makamo hawataki kuteseka kwa kufikiria mambo ambayo yatawapa huzuni bure. Na kwa kuwa umri mkubwa haukupukiki, basi kipindi hicho ndicho cha kufikiria kifo. Wakati huo mwanadamu atasugua bongo lake na kutafakari kwa kina juu ya kifo na hivyo kuanza maandalizi ya maisha yajayo.

Hili nalo hutoa nafuu ya kiroho, kwanzi hutoa mwanya wa hisia kuwa ipo haja ya kufanya maandalizi kwa ajili ya akhera (maisha yajayo).

Ukweli unabaki kuwa, kwa kuweka mipango hiyo ya mbali, mwanadamu anahakika ya kukamilisha mipango hiyo. Bado mwanadamu hana hakika juu ya kupumua kwake atafikisha huko au la. Kila uchao mwanadamu anashuhudia watu wa rika lake au wadogo kiumri kuliko yeye wakiaga dunia. Rambirambi za vifo zimetengewa sehemu maalum kwenye magazeti ya kila siku. Kila saa, runinga (television) na redio hutoa taarifa juu ya vifo ama vya mtu mmoja mmoja au vya makundi ya watu. Ama kutokana na ajali, vita au majanga kama kimbunga, matetemeko ya ardhi, mafuriko na kadhalika. Mara nyingi mtu kushuhudia vifo kwa wale waliomzunguuka. Lakini, kamwe hafikiri japo kwa uchache kuwa watu waliomzunguuka watashuhudia kifo chake au watasoma katika magazeti babari za kifo chake. Kwa upande mwingine, japo anaweza kuishi kwa muda mrefu, hakuna litakalobadili maisha yake, maadam mtazamo wake umebakia kama ulivyo. Mpaka kifo kitakapomkabili, bado ataendelea kuahirisha kufikiria kifo.

Pili, kudhania kuwa, mtu atatumikia adhabu yake' motoni kwa muda tu. Mtazamo huu ambao umeenea katika jamii, si chochote ila ni aina ya ushirikina tu. Tangu hapo si imani iliyo na mizizi madhubuti katika Qur'an. Hakuna sehemu kutoka katika Qur'an inayoonesha kuwa mtu ataenda kuadhibiwa motoni kwa kipindi fulani tu kisha atolewe humo kwa kupata msamaha. Kinyume chake,

katika aya zote zinazozungumzia suala la adhabu kwa waovu na malipo mazuri kwa watu wema, inaainishwa kuwa siku ya hukumu watu watakuwa katika makundi mawili, yaani waumini na makafiri. Pia kutokana na mafundisho ya Qur'an, imeelezwa kwamba waumini watakuwa peponi milele na makafiri nao watatumbukizwa motoni ambako adhabu yao itakuwa milele.

Na walisema: 'Hautatugusa moto (wa Jahannam) isipokuwa kwa siku chache tu.' Sema: Je! Mmepata ahadi kwa Mwenyezi Mungu? Kwa hivyo hatutakhalifu ahadi yake. Au Mnamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua.'

Naam, wanaochuma ubaya – na makosa yao yakawazunguuka – hao ndio watu wa Motoni; humo watakaa milele. Na wale walioamini na kutenda mema, hao ndio watu wa peponi, humo watakaa milele (Al-Bagara:80–82)

Aya nyingine inayotilia mkazo juu ya hili:-

'Hayo ni kwa sababu walisema: 'Hautatugusa moto isipokuwa kwa siku chache.' na yakawadanganya katika dini yao yale waliyokuwa wakiyazua. Basi itakuwaje tutakapowakusanya katika siku ambayo hapana shaka kuja kwake? Na kila nafsi italipwa kwa ukamilifu kila iliyo chuma, nao hawatadhulumiwa. (Al-Imraan:24 – 25).

Jahannam ni mahali ambapo ukali wa adhabu yake haifikiriki. Hata hivyo, hata kama kubakia katika moto itakuwa ni kwa kipindi tu, yeyote mwenye akili timamu hawezi kuitamani adhabu hiyo kisha eti ndio asamehewe. Motoni ni mahali ambapo, sifa ya Mwenyezi Mungu ya al-Jabbar – (Mwenye kuteza nguvu) na Al-Qahhar (Mwenye Nguvu – Muweza) hudhihirika. Adhabu ya motoni kamwe haiwezi kulinganishwa na adhabu yoyote ya kidunia. Mwanadamu ambaye hawezi kustahamili walau kuungua kwa kidole chake lakini bado akatamka kwamba anaweza kukabiliana na adhabu ya motoni anadhihirisha ule udhaifu wake wa kifikra mara zote, yeyote ambaye haogopeshwi na kupata ghadhabu za Mwenyezi Mungu, hushindwa kumpa Mwenyezi Mungu haki yake ya kutukuzwa. Mtu wa aina hiyo huwa hana chembe japo ndogo ya Imani, na ni mtu maskini ambaye hastahili hata kutajwa.

Njia nyingine inayotumwa katika harakati za kujiridhisha wenyewe na suala la kifo ni kitendo cha kufikiria tayari wanastahili Pepo kwa baadhi ya watu. Watu hawa hujiona kwamba kwa kujihusisha na vitendo vidogo wanavyodhania ni vitendo vizuri na kuepua mambo makubwa ya kufanya. Wameona kuwa hayo wanayofanya yanatosheleza kuwaingiza peponi. Wamezama katika kufanya mambo ya kishirikina na kutamka maneno kadhaa waliyoyasikia wanayoyanasibisha na dini, hawafuati chochote zaidi ya ukweli kwamba wanafuata imani iliyo kinyume kabisa na ile iliyofafanuliwa ndani ya Qur'an. Hujionesha kwamba wao ndio waumini kweli. Wakati huo huo, Qur'an imewaweka katika kundi la wale wanaomfanyia Mwenyezi Mungu washirika:

Na wapigie mfano wa watu wawili: Mmoja wao tulimfanyia (tulimpa) mabustani mawili ya mizabibu tukaizungushia mitende, na pia katikati yake tukatia miti ya nafaka (nyingine). Haya mabustani yote mawili yalijaa matunda yake wala hayakupunguza chochote (katika uzazi wake); akamuambia rafiki yake; ‘Mimi nina mali nyingi kuliko wewe na watu wengi katika milki yangu. Na akaingia katika shamba lake na hali ya kuwa anajidhulumu nafsi yake kwa kusema: “Sidhani abadan’. Wala sidhani kuwa kiama kitatokea. Na kama nitarudishwa kwa Mola wangu bila shaka nitakuta makazi mazuri.” Na mwenzake akamwambia na hali anajibu, ‘Je humuamini yule aliyekuumba kutokana na udongo, kisha kutokana na mbegu ya manii, kisha akakufanya mtu kamili?’ Lakini, Yeye Mwenyezi Mungu, ndie Mola wangu na si mshirikishi na chochote. (Al-Kahf: 32 – 38).

Kwa maneno, ‘Lakini kama nitarudishwa kwa Mola wangu’, Mwenye bustani anaonesha hisia zake kwamba hana imani na Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na hivyo kudhihirisha kwamba ni mshirikina ambaye ana mashaka mengi. Wakati huo huo anadai kuwa ni muumini mkubwa sana. Hivyo, anadhani kwamba hakuna wasiwasi kwamba Mwenyezi Mungu atamlipa Pepo. Tabia hii ya kujifaragua na pia kuwa na vitendo duni vya washirikina ni maarufu mno miongoni mwa watu.

Watu hawa katika nafsi zao wanajua kwamba ni waharibifu. Lakini pindi wanapoulizwa juu ya mwenendo wao huo, wanajaribu kuthibitisha kuwa kwa hakika hawana hatia ya aina yoyote ile. Hudai kuwa kuchunga maamrishi ya dini yao sio muhimu sana. Zaidi, hujaribu kujitakasa, kwa kudai kuwa wanaodhaniwa ni watu wa dini wanaowaona kila upande si waadilifu na wala si waaminifu. Hujaribu kuthibitisha kwamba wao ni ‘watu wazuri’ kwa kusema kuwa hawakusudii ubaya wowote kwa yeyote. Husema kuwa wao hawana kikwazo katika kutoa fedha kwa ajili ya waombaji, ambao wamekuwa wakiutumikia ummah kwa uadilifu mkubwa kwa miaka mingi. Na haya ndio mambo yanayomfanya Mtu awe Muislamu mzuri. Ama hawajui au wanajifanya hawajui kwamba kinachopelekea mtu awe Muislamu si kwa kuonekana mzuri kwa watu tu kwa kuwapa fedha bali ni kwa kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu na kufuata maamrishi yake. Na mwishowe katika kuiegemeza dini yao waliyoipindisha kwa namna fulani ya kuhalalisha wanayofanya, hubakia katika lindi la uongo. Kwa hakika hii ndio aina hasa ya kukosa kwao uadilifu. Katika kuhalalisha wanayotenda, wanajikinga kwa misemo kama ‘Aina bora ya Ibada ni kufanya kazi’, au kinachoangaliwa ni usafi wa moyo.’ Kwa maneno ya Qur’an huku ni “kumzushia uongo Mwenyezi Mungu” na inastahili kupata adhabu ya milele Jahannam.

Katika Qur’an, watu wa aina hiyo Mwenyezi Mungu amewaelezea kama ifuatavyo:-

'Wanadhani wanamhadaa Mwenyezi Mungu na wale walioamini. Hawamhadai yeyote isipokuwa nafsi zao, lakini hawajui'. (Al-Baqara:8).

Njia nyingine wanayoitumia ni ile ya kuwa ndumila kuwili (wanafiq). Wakati mwingie watu wanapofikiria juu ya kifo, huweka fikra kuwa watatoweka milele. Fikra kama hizo huwafanya waweke

kanuni ya kujiliwaza kwamba ni asilimia hamsini tu ya kuwepo uwezekano wa kuwa na “maisha mengine baada ya kufanya yaliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu.” Hitimisho kama hili huamsha matumaini fulani kwao. Wakati wanapotafakari wajibu wa muumini kwa Mola wake, huamua moja kwa moja kukanusha kuwepo kwa maisha ya milele baada ya kifo. Hujiliwaza kwa kusema “Tangu hapo, tutarejeshwa kuwa si chochote, na kusagika sagika kabisa katika udongo. Hakuna maisha baada ya kufa.” Dhana kama hizo huondosha kabisa hofu na uwajibikaji, kama vile kuulizwa na kuhesabiwa matendo yao siku ya hukumu au kuadhibiwa motoni. Katika mazingira hayo yote ya namna mbili, husababisha waendeshe maisha yao bila ya malengo (wakiwa wameghafilika) mpaka mwisho wa masiku yao ya kuishi hapa duniani.

HATIMA YA KUGHAFILIKA NI KUKOSA MUELEKEO

Katika sehemu iliyopita, imeainishwa kwamba, maadamu mtu yungali hai, hapana budi kukitilia kifo maanani. Ukumbusho huu umethibitisha kuwepo kwa faida, kwani kumshukuru mwanadamu kujitathmini upya katika yale aliyoyapa kipaumbele katika maisha yake ya kila siku na hivyo kutathmini mitazamo yake kwa ujumla. Hata hivyo upo wakati ambao hali ya kujihami miongoni mwa wanadamu inachukuwa nafasi ya juu na hivyo kuufanya kila uchao wa mtu huyo kuzidi kugubikwa na giza la kughafilika. Kama makafiri wanasubiria kifo katika hali ya kutokuwa na wasiwasi na wana hisia zisizo sahihi kwamba ni aina fulani ya kujiliwaza, hata kama watakuwa wana yakini kabisa ya kukaribia kwa kifo hicho katika miaka inayofuata mbele, wao hawatakuwa na wasiwasi wowote kutokana na blanketi hili. Hii ni kwa sababu kifo kwao wao huwa na maana kuwa ni mapumziko na usingizi mnono, utulivu na unyenyekevu, na nafuu ya milele. Ni maarufu maneno kama Fulani amekufa, amekwenda kupumzika mapumziko ya milele.

Kinyume na kile wanachofikiria, hata hivyo, Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye Muumba wa kila kiumbe kutokana na kisichokuwepo na ambaye atavijaalia vife na ambaye atavipa uhai viumbe vyote siku ya hukumu, amewaahidi majuto na adhabu ya milele. Pia, watashuhudia ukweli huu wakati wakifariki dunia, muda ambao walifikiri wanakwenda katika mapumziko ya milele. Watatambua kwamba kifo sio kupotea moja kwa moja, bali ni mwanzo wa ulimwengu mpya uliojaa misukosuko ya adhabu. Hali ya kutisha ya awali ni ya sura za kutisha za malaika wa kifo. Hii ni dalili ya awali ya adhabu kubwa iliyoko mbele.

‘Basi iakuwaje (hali yao), malaika watakapo wafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao. (Muhammad:27).

Muda huu, ujeuri waliokuwa nao makafiri kabla ya kifo na hali ya majivuno hugeuka kuwa vitisho, kujuta, kukata tamaa na maumivu ya milele. Ndani ya Qur’an hali hii imeelezwa kama ifuatayo:-

Nao husema ‘Je tutakapokuwa tumemezwa katika ardhi, ndio tutarejeshwa katika umbo jipya? Bali wao hawakiri kwamba watakutana na Mola wao! Sema ‘Malaika wa mauti wamepeva jukumu juu yenu, watizinyakuwa roho zenu na kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu! Na ungaliwaona waovu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao’ (na Kusema) ‘Mola wetu! Tumekwisha kuona na tumekwisha kusikia, basi turudishe, tutafanya vitendo vizuri; (hakika (sasa) tumeyakinisha.’ (As-Sajidah:10–12).

KIFO HAKIEPUKIKI

Kifo, hasa katika umri mdogo, ni mara chache mno kumpitukia katika akili yake mwanadamu. Kwa kufikiria kuwa huo ndio mwisho mwanadamu hujitahidi kugeuka hata kukifikria. Hata hivyo, japo kukimbia mbali ili ukwepe kifo hakukuponyeshi kukabiliwa nacho, hivyo hivyo kujizuilia kufikiri juu ya kifo hakukuathiri ama kuwepo au kutokuweo kwake. Vyovyote iwavyo kufikiria kuwepo kwa kifo, hakuzuiliki. Kila siku uchao, taarifa za vifo ama vya mtu mmoja mmoja au vya makundi ya watu ndiyo vinavyotawala taarifa za magazeti, maredio, Runinga na vinginevyo. Yanayosemwa juu ya kifo, mwanadamu huwa anayasikia au amepata pia kupita Makaburini. Ndugu na jamaa zake wanakufa. Mtu anapokwenda kwenye mazishi au kutoa rambirambi kwa wafiwa, kwa vyovyote hupita katika ubongo wake habari kuhusu kifo. Kama vile ambavyo mtu anashuhudia kifo cha wengine, hasa wale anaowapenda, ndivyo hivyo hivyo hupata fikra juu ya kifo chake mwenyewe. Fikra hizi humgusa sana ndani ya moyo wake, na hivyo humfanya akose utulivu.

Bila kujali ni kwa nguvu kiasi gani mtu anapiga juu ya kifo, lakini anajua kuwa wakati wowote atakutanacho, ama awe anatafuta hifadhi mahali au anajaribu kukipiga chenga. Kuhesabu muda na sekunde kuelekea kwenye kifo kamwe hakuzailiki japo kwa muda mdogo tu. Popote atakapoelekea, kifo kitamkuta huko. Mduara, unajikurubisha na mwisho utamnyakua.

‘Sema: “Hakika mauti haya mnayoyakimbia, bila shaka yatakutana nanyi; kisha mtarudishwa kwa mjuzi wa siri na dhahiri; hapo atakujulisheni yote mliyokuwa mkiyatenda.” (Al-Jumua:8).

‘Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome madhubuti (Nisai:78).

Ndio maana mwanadamu analazimika asijidanganye au kupuuza ukweli na badala yake afanye juhudi ili apate furaha kutoka kwa Mola wake ambayo tayari amekwisha mfahamisha kabla. Ni Mwenyezi Mungu pekee anayejua ni lini hasa muda huo utawadia. Mtume Muhammad (s.a.w) amesema njia bora kwa mtu kuepuka adhabu na kuingia katika mwenendo mwema ni kukumbuka kifo mara kwa mara.

Abdallah bin Umar amehadithia, ‘Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) amesema: ‘Hizi nyoyo hupata kutu kama kipatavyo chuma kinapoathiriwa na maji. alipoulizwa ni nini kinachoweza kusafisha nyoyo, alijibu. Kukumbuka kwa wingi Kifo na Kusoma Qur’an (Al-tirmidh, 673).

KIFO HALISI NA KIFO CHA NAFSI

Je! Umewahi kuwaza namna gani? Na ni kitu gani kinatokea wakati wa kufa?

Hadi leo, hakuna yeyote katika wafu aliyerejea tena katika uhai huu ambaye anaweza kutusaidia mawazo kuhusu uzoefu wake na hisia zake wakati wa kufa. Mwenyezi Mungu ambaye ndiye aliyejaalia uhai kwa mwanadamu na ndiye anayeuchukuwa kwake kwa kufuata utaratibu aliojiwekea, anatufahamisha ndani ya Qur'an kuwa ni nini hasa kinachotokea. Hivyo Qur'an ndio chanzo pekee ambacho mwanadamu anajifunza kuwa kifo kinatokeaje na hasa ni yapi anayohisi na yanayomtokea yule anayekufa. Kifo kama kinavyoelezwa ndani ya Qur'an si sawa na 'Kifo cha Kimazingaombwe' mwanadamu anachoshuhudia kutoka nje au kwa sura ya nje. Kimsingi, aya kadhaa zinatufahamisha juu ya tukio lenyewe kama lionekanavyo toka kwa yule anayekufa, ambacho hakuna yeyote anayehisi hivyo ila muhusika tu. Hayo yamebainishwa katika Surat Waqi'ah.

'Basi Mbora (Roho) ifikapo kooni. Na ninyi wakati ule mnatazama. Nasi tunakaribiana naye zaidi kuliko ninyi, wala ninyi hamuoni (Waqiah:83 – 85).

Kinyume kabisa na kifo cha makafiri, kifo cha watu wema ni rehema tupu.

Wale ambao Malaika huwafisha katika hali njema, wakasema: 'Amani itakuwa juu yenu; ingieni peponi kwa sababu ya yale (mema) mliyokuwa mkiyatenda. (An-Nahl:32).

Aya hizi zinadhihirisha hoja muhimu na isiyobadilika kuhusu kifo: Wakati wa kukata roho, mtu anayekufa anapita kwenye nini? Na wale walio karibu yake (wanaomtazama) wanapata uzoefu wa aina gani! Ni maono mawili tofauti kwa tukio moja.

Kwa mfano: Mtu anayetumia maisha yake yote kama kafiri asiye na faida anaweza kuonekana kwa nje, 'Kifo chake ni cha amani'. Wakati huo huo, Roho, katika mtazamo mwingine, inaonja mauti kwa namna iumizayo kweli kweli.

Kwa upande mwingine, Roho ya Muumini, pamoja na kuonekana kama mwenye kuugulia na kuumia mno, huuacha mwili wake katika hali ya uchaji Mungu. Kwa ufupi kufa kwa mwili na kufa kwa roho kulikoainishwa ndani ya Qur'an ni hali mbili tofauti kabisa.

Kwa kutoujua ukweli huu unaoainishwa ndani ya Qur'an, makafiri ambao hujaalia kifo kuwa ni usingizi wa amani na wa kudumu, pia husaka njia ambayo kwayo wakati wa kufa nao uwe kama maumivu na uwe wa raha.

Ni kutokana na mtazamo huo finyu wa uhalisia, baadhi ya watu ili kuepuka kifo chenye machungu, huamua kujiua ama kwa kuvuta gesi ya sumu, au kunywa sumu yenyewe au kujipiga risasi. Ukweli unabakia palepale, kifo kwa upande wa makafiri namna yake huwa ni sehemu ya adhabu kwa hiyo machungu makali ni lazima yapatikane kwa kiwango kile kile kilichokadiriwa. Kwa upande wa waumini, kifo kinakuwa rehema kwao. Hivyo hawaonji machungu kama yale yapatikanayo kwa waliomkufuru Mwenyezi Mungu. Hata kama kwa nje ataonekana anaugua hasa na kuonesha wazi athari za kuumwa kwake au majeraha yatokanayo na vita vya kuihami dini ya Mwenyezi Mungu.

Qur'an inatubanishia machungu wanayoyapata makafiri wakati wa kutoka roho zao, namna malaika wanavyotoa roho hizo.

Basi itakuwaje wakati Malaika watakapowafisha wakawa wanawapiga nyuso zao na migongo yao. Hayo ni kwa sababu wao walifuata yaliyomchukiza Mwenyezi Mungu na wakachukia yanayomridhisha, basi akaviondoshea thawabu vitendo vyao. (Muhammad: 27 – 28).

Katika Qur'an pia kuna maelezo juu ya mahangaiko ayapatayo mtu muovu ambaye kwa hakika ni matokeo ya taarifa ya Malaika kwake juu ya adhabu ya milele inayomsubiri baada ya kifo:

'... Na kama ungewaona madhalimu watakapokuwa katika mahangaiko ya mauti, na malaika wamewanyoshea mikono yao (na kuwaambia), 'Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ifedheheshayo kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu na kwa vile mlivyozifanyia aya zake' (Al-An'am: 93).

'Na laiti ungaliwaona malaika wanapowafisha wale waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao na (kuwaambia). 'Ionjeni adhabu ya moto! Hayo ni kwa sababu ya (maasi) yale yaliyofanywa na mikono yenu. Na hakika Mwenyezi Mungu Si mwenye kuwadhulumu waja wake. (Al-Anfal:50–51).

Kama aya zilivyobainisha, kifo kwa wasio na imani ni 'kipindi tosha cha kupata adhabu iumizayo. Wakati ndugu, jamaa na marafiki wakiwa wamekizinguuka kitanda kuonesha mapenzi kwa ndugu ya huyu, wanaona kila kitu ni shwari tu. Lakini ukweli ni kwamba, kwake yeye anamuona malaika na mauti akimchukuwa roho yake kwa nguvu:

'Naapa kwa wale (malaika) wavutao kwa nguvu. (Naziat:1)

'Sivyo (mnavyofanya)! (Roho) itakapofika katika mitulinga, Na kusema; Ni nani wa kumzingua (na kumpoza mgonjwa huyu?'

Na mwenyewe akajua kwa hakika kuwa hiyo ni (Saa ya) kufariki (dunia) – (Al-Wiyama: 27 – 28).

Kwa wakati huu, kafiri anadhihirikiwa na ukweli alioukanusha kwa muda wake wote alipokuwa duniani. Kwa kifo, ataanza kuona uchungu, ambao ni matokeo ya majuto yake na kukanusha kwake. Malaika watakapokuwa ‘Wanawapiga migongoni mwao’ na pia ‘Wakiwatoa roho zao kwa nguvu’, ni dalili tu za mwanzo na majuto na mateso yanayowasubiri.’

Kinyume na hali hiyo kwa makafiri, watu wema (waumini) kifo chao huwa ni mwanzo wa furaha ya milele na rehema. Tofauti na kafiri ambaye roho yake huchukuliwa huku akiteseka kwa machungu, roho ya muumini hutolewa na kuchukuliwa kwa upole.

‘Na kwa wale wanaotoa(roho za watu wema) kwa ulatifu (taratibu).’ (Naziat:2).

Wale ambao malaika huwafisha kwa hali njema, wakasema, “Amani itakuwa juu yenu, ingieni peponi kwasababu ya yale (mema) mliyokuwa mkiyatenda. (An–Nahl:32).

Hii inafananana hali ya mtu anapokuwa usingizini. Ndani ya usingizi, roho kwa utaratibu huhamishwa na kuwekwa katika mazingira tofauti na haya. Hayo yamebainishwa katika aya ifuatayo:-

‘Mwenyezi Mungu hutakabadhi (huchukuwa) roho wakati wa mauti yao. Na zile ambazo bado hazijakufa, wakati wakiwa usingizini. Huzizuilia zile ambazo kifo kimekwisha hukumiwa juu yao, na kuzirudisha nyingine mpaka wakati uliowekwa ... (Az-Zumar: 42).

Huu ndio ukweli kuhusu kifo. Kwa sura ya nje, watu hushuhudia kifo cha mwili; mwili kushindwa kufanya kazi zake za kawaida. Watu hawaoni, kafiri akipigwa usoni au mgongoni wakati wa kukata roho, wala roho inapovutwa hadi kufika katika matulinga ya mabega yake. Ni roho ya muhusika tu ndiyo inayoshuhudia na kuhisi yote haya na kuyakabili. Hata hivyo, kifo halisi ‘kinaonjwa’ katika upana wake wote ambazo hazioani na zile za watazamaji kifo kwa nje. Kwa maneno mengine, yale yanayotokea wakati wa harakati za kifo ni mabadiliko ya hali, kutoka katika mtazamo wa kidunia na kuingia katika mtazamo wa kiakhera. Kwa muhtasari, maelezo ya aya iliyobainishwa hapo juu yaweza kuwa kama ifuatayo:-

‘Ama kwa kuwa kwake Muumini au kafiri, mwanadamu yeyote hawezi kukisogeza kifo chake kwa kukiwahisha zaidi au kukichelewesha baada ya muda uliopangwa japo kwa saa moja. Popote alipo mwanadamu kifo kinaweza kumfikia tu. Katika harakati za kukata roho, ‘Sakarati Mauti’, kila mtu ana namna yake atakayohisi kutegemeana na matendo yake japo katika sura ya nje ni ngumu kuwatofautisha.

KIFO CHAMUUMINI

Jua kuwa kifo hakiepukiki. Kwa Umri wake wote uliompitukia, Muumini hujiandaa kwa kifo.

Malaika wa mauti humpa bishara njema kuwa ataingia peponi.

Malaika hutoa roho yake Muumini kwa upole.

Muumini huhisi haja ya kuwapa habari njema waumini wengine waliobaki hapa duniani kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli na kwamba hakuna kuogopa wala kusikitika kwa waumini. Hata hivyo, hili halitaruhusiwa.

KIFO CHA KAFIRI

Atakutana na kifo alichokuwa muda wote wa uhai wake akikikwepa.

Katika kipindi cha Sakarati Mauti (Kukata roho) atakuwa mwenye kukumbwa na mtetemeko wa hali ya juu na hivyo kumuumiza.

Malaika watamkunjulia mikono na kumpa habari kuwa atakuwa mwenye kuathirika kwa adhabu ya motoni inayomsubiri.

Malaika wataitoa roho yake hali ya kuwa wanampiga usoni na mgongoni mwake.

Roho yake inachukulikuwa kwa nguvu na hivyo kusababisha maumivu makali mno yaendayo ndani.

Roho ichukuliwapo na ikafika katika mitulinga ya mabega yake hakuna yeyote katika wanadamu awezaye kumponya na kifo kilichokwisha wadia.

Roho inachukuliwa kwa shida kubwa wakati anajiingiza katika kukanusha.

Wakati wa kukata roho, hakutakuwa na fursa tena ya kuonesha kuwa sasa anaamini au anatumia itakayo kubaliwa.

Kifo cha mwili namna kinavoonekana katika sura ya nje, yaani kwa (wale wanaotazama mwili wa marehemu) hutoa mafunzo kadhaa ya kuyazingatia:-

Namna kifo cha mwili kinavyomrejisha mwanadamu na kuonekana si lolote wala chochote humfanya mwanadamu kujua hakika ya mambo muhimu sana. Hivyo basi, 'kifo cha mwili' na kaburi, kinachomsubiri kila mmoja katika wanadamu, pia kinahitajika kuainishwa na kuzingatiwa.

KIFO CHA MWILI KAMAKIONEKANAVYO KATIKA SURA YA NJE

Punde mtu anapofariki dunia, wakati roho inatengana na mwili wa mwanadamu, huacha nyuma mwili usio na uhai. Kama ilivyo kwa viumbe kama nyoka, ambao hujibua ngozi yao au kuchuna ngozi ya juu ya mwili wake kuacha jibuo lisilo na uhai naye akiendelea na maisha mengine, vivyo hivyo kwa mwanadamu. Roho ambayo imetoka katika mwili, hendelea na maisha mengine yenye hakika huku mwili (ganda) likiachwa bila ya uhai wowote.

Tangu wakati huo na kuendelea, hatakuwa tena uhusiano na mwili wake kwa namna yoyote ile. Mwili ule uliodhaniwa ndio ‘mwanadamu mwenyewe’ kwa kipindi chote cha uhai wake, utabadilika na kuwa mlundikano wa nyama tu. Kwa kifo chake, mwili wake utabebwa na watu wengine. Watakuwepo watu wakiwa wanalia na kuomboleza. Kisha mwili huo utapelekwa chumba cha kuhifadhia maiti kwa usiku nzima. Siku inayofuata hatua za mazishi zinaanza. Mwili uliokufa, sasa umekuwa mkakamavu, utaoshwa kwa maji baridi. Wakati huo huo alama za kifo zitaanza kuonekana huku baadhi ya sehemu za mwili wake zikianza kubadilika rangi na kuwa zambarau. Kisha mwili huo utavishwa sanda na kuwekwa katika jenzea la mbao. Wakati wanaelekea makaburini, maisha ya mitaani yataendelea kama kawaida. Baadhi ya watu watakapokuwa wanashuhudia anayepitishwa, wataonesha kujali huku kundi kubwa likiendelea na mapambano yao ya maisha ya kila siku. Huko makaburini, jenzea lake litabebwa na wale vipenzi vyake au wale wanaodhaniwa wana mapenzi naye. Si ajabu, pia watakuwepo watu wakiendelea kulia na kuomboleza. Kisha watu watawasili katika makazi yasiyoepukika, kaburi. Katika kikuta cha sementi, jina lake litaandikwa. Mwili wake katika jenzea na kuwekwa katika mwanadani. Maiti ikiwa tayari kabla ya kutolewa kwenye jenzea, sasa dua mbalimbali zikiendelea kuombwa watu watakuwa wamejiandaa kwa kazi moja muhimu, kuuweka mwili kwenye mwanandani na kufukia shimo lenye mwili wake (kaburi). Mwisho, watu watabeba mabeleshi, makoleo, machepeo, sululu na majembe na kuanza kufukia kaburi kwa udongo. Hatimae, udongo utafikia sanda yako na hivyo hakutakuwepo tena nafasi ya kupata mwanga. Hapo watu watarejea majumbani na kuacha kimya kizito makaburini. Watu watarejea katika shughuli zao kama kawaida. Kwa Mwili aliozikwa, maisha yatakuwa hayana maana tena. Nyumba nzuri, warembo, sehemu ya kupunga upepo, vyote vitakuwa havina maana tena. Mwili ule hautakutana na marafiki zake tena. Kuanzia hapo na kuendelea, kitakachokuwa na uhakika ni kwamba udongo na wadudu na bakteria ndio waishio humo.

Mwanaadamu amewahi kufikiria juu ya hali ya mwili wake baada ya kufa utakuwaje?

Kwa kuzikwa, mwili utaoza kwa haraka mno kutokana na sababu za aina mbili, zile za umbile la mwili wenyewe, au zile za nje ya mwili. Mara baada ya kuwekwa kaburini na kufukiwa, bakteria na wadudu wengine wataanza kuzaliana mwilini kutokana na kukosekana hewa ya oksijeni. Gesi itakayotengenezwa kutokana na viumbe hawa itapelekea mwili kugandamizwa, kuanzia kwenye kiwiliwili (tumbo) umbile likibadilishwa na muonekano wake kadhalika. Damu itaanza kutoka mdomoni, na puani kutokana na shinikizo (pressure) la hewa katika kifua. Hali itazidi kuwa mbaya kwani nywele, kucha, nyayo na mikono vitameguka meguka.

Hali hii ya nje itaendelea sanjari na viungo vya ndani navyo kuathirika vibaya. Viungo kama mapafu, moyo na ini navyo vitaoza. Wakati huu tumboni nako hali si shwari. Ngozi haiwezi tena kustahamili shinikizo la gesi. Hivyo tumbo litapasuka, na kutoa harufu mbaya sana. Kuanzia katika fuvu hadi mishipa vitaachana kutoka mahali vilipokuwa. Nyama na ngozi vyote vitasagika sagika kabisa. Ubongo utaoza na kuonekana kama udogo tu. Hali hii itatendeka hadi mwili utakapobakia huwa mifupa tu.

Mwili, uliodhaniwa kuwa ndio mtu, utakuwa umepotea kabisa kwa njia ambayo kwa hakika ni yenye kutisha mno. Wakati kundi la wale waliobaki hai likiendelea kuomboleza na kufanya visomo mbalimbali, minyoo, wadudu a bakteria katika udongo, nao watakuwa wanashambulia na kuumaliza kabisa mwili kwa kuula.

Kama umauti wake umetokana na ajali na utakuwa haukupata fursa ya kuzikwa, matokeo yake yatakuwa ni yenye kutisha zaidi. Mwili wake utakuwa na wadudu mithili ya mzoga anavyoshambuliwa na wadudu katika joto la kawaida kwa kipindi kirefu. Mara ulaji huo utakapokamilika kinachosazwa ni mifupa tu.

Kwa nini? Kwa hakika hii ni kutokana na mpango wa Mwenyezi Mungu kuwa mwisho wa mwili wa mwanadamu uwe huo. Kwa utaratibu huo, somo lenye kuhitajia mazingatio litakuwa limepatikana. Mwisho huu unaomsubiri Mwanadamu, kumtanabahisha kuwa yeye sio ‘huu mwili pekee’ bali ni ‘Roho’ iliyomo ndani ya mwili huu. Kwa maneno mengine mtu lazima atanabahi kuwa yeye ni zaidi ya mwili huu. Mwisho huo wa kushitua, pamoja na mazingatio yake, umefanywa hivyo, ili mwanadamu ajue kwamba yeye sie ‘nyama na mifupa.’ Kwamba yeye si ule mwili uliokufa katika ujumla wake. Yeye ni roho iliyotoka na kuhifadhiwa anakokujua Muumba ukisubiri kuvikwa umbile jingine utakapofufuliwa na baada ya hukumu. Na kwa ajili hiyo yeye si huo mwili unaoshambuliwa na wadudu pale kaburini na kuchakachika kabisa.

MAISHA YA ULIMWENGU HUU NI YA MUDA TU

Mwanadamu amekwishapata kufikiri ni kipi kinachomfanya atumie muda mwingi na juhudi kubwa katika kuuweka mwili wake uwe safi? Ni kwanini mwili mchafu, mdomo unaonuka, mwili uliotapakaa girisi wa fundi makanika au nywele zisizotunzwa vizuri hauvutii? Kwa nini mwanadamu hutoka jasho?

Na kwanini jasho lake huambatana na harufi mbaya yenye kuudhi? Tofauti na hali hiyo, kwa upande wa mimea, hiyo hutoa harufi nzuri. Mawaridi au muasumini kamwe si wenye kukera pamoja na ukweli kwamba haukuwa katika udongo na kubakia katika mazingira ambayo ni ya vumbi na machafu. Mwanadamu hawezi kamwe kufikia hali ya mawaridi au muasumini na harufi ya mimea ya aina nyingine yenye kutoa harufi nzuri. Hali hii ni ukweli bila kujali kwamba anaangalia mwili wake vizuri au la!

Hivi mwanadamu amewahi kutafakari kwa nini ameumbwa hali ya kuwa ni mwenye udhaifu kwa kiwango hiki? Kwa nini Mwenyezi Mungu ameumba mimea ikawa ni yenye kutoa harufi nzuri kwa kiwango hiki na mwanadamu naye licha ya kuoga na kujisafisha mara kwa mara awe ni mwenye kutoa harufu mbaya katika mazingira yaliyoelezwa juu?

Udhaifu wa mwanadamu si katika kutoa harufi mbaya tu, bali pia unapatikana kwa kuchoka, kuumwa njaa, kupata majeraha, kupata magonjwa sugu na kadhalika. Yote haya yameonekana ni ya kawaida mno kwa binadamu. Lakini tafakuri inabainisha kuwa yamo mafunzo makubwa mno ndani yake. Ingewezekana kabisa kuwa mwanadamu asitoe harufi mbaya katika mwili wake. Vivyo hivyo ingewezekana mtu asiugue kabisa japo kichwa au maradhi mengine. Udhaifu wote huu kwa mwanadamu hautokei kwa bahati nasibu au hautokei kwa bahati nasibu. Yote yameumbwa na Mwenyezi Mungu kwa kudhamiria kwa malengo mahususi. Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu jukumu maalum na akamjaalia udhaifu.

Mbinu hiyo inafanya kazi ya aina mbili kimalengo. Mosi, humfanya mwanadamu atanabahi kuwa yeye ni kiumbe dhaifu, ‘Mtumwa’ wa Mwenyezi Mungu. Kuwa mkamilifu ni Sifa ya Mwenyezi Mungu. Watumwa wake kwa upande mwingine ni dhaifu mno na hivyo humhitajia mno Mwenyezi Mungu ambaye ndiye Muumba wao. Haya yanafanuliwa katika Qur’an kama ifuatavyo:-

Enyi Watu! Ninyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi, asifiwaye. Kama akitaka atakuondoeni na ataleta viumbe wapya. Na jambo hili si gumu kwa Mwenyezi Mungu – (Fatir: 15 – 17).

Udhaifu wa mwili wa Mwanadamu muda wote humkumbusha juu ya udhaifu wake. Mwanadamu anaweza kudhania kuwa yeye ni bora na kiumbe mkamilifu. Lakini, ukweli ni kwamba anahitajia kwenda haja kila siku. Na anayoyaona huko humfanya atanabahi juu ya ukweli kuhusu yeye kwa nafsi yake.

Pili, udhaifu wa mwanadamu husaidia kumkumbusha ukweli kuwa maisha haya siyo ya kudumu. Hii inatokana na sababu kuwa udhaifu unaompata mwanadamu ni wa aina yake kwa mwili wa Mwanadamu. Katika maisha yajayo; watu wa peponi watakuwa na miili mingine. Mwili dhaifu na usiotimilifu na mnyonge katika Ulimwengu huu, sio mwili halisi wa Muumin, atakaokuwa nao bali huu ni umbile la muda analobaki nalo kwa muda mahsus tu hadi atakapoondoka katika ulimwengu huu.

Ndio maana, katika ulimwengu huu, uzuri usio na upungufu haujawahi na hautaweza kufikiwa. Yule mwanadamu anayevutia kimaumbile, mtimilifu na mrembo, pia huenda haja, akitokwa na jasho, hutoa harufi mbaya mdomoni nyakati za asubuhi, hapa na pale akiugua madonda au mapele kwenye ngozi yake. Mtu huhitaji kujiwekea ratiba ya kila siku kujisafisha na kujiweka msafi. Baadhi ya watu wana nyuso za kuvutia lakini hawana maumbo yenye kuvutia. Wapo baadhi ambao hali zao ni kinyume na hayo. Wapo wenye macho ya kuvutia lakini pua kubwa. Ipo mifano mingi ya aina hiyo. Mtu anaweza kuonekana mrembo kwa nje, lakini kwa ndani ana maradhi makubwa mno. Anaweza kuwa mremba wa kutazamika lakini ana tabia mbaya na za kukera zisizovumilika.

Juu ya yote haya, yule aonekanaye mtimilifu kwa kumtazama huzeeka na kufa. Ama yawezekana, katika ajali ya barabarani isiyotegemewa, mwili wake unaweza kupata majeraha

yasiyopona. Izingatiwe kuwa, sio mwili wa mwanadamu pekee ambao si mtimilifu, la hasha, pia maua ya aina zote nayo hunyauka, vyakula vyote vitamu navyo huharibika kwa kuoza. Yote haya mwanadamu anayashuhudia hapa ulimwenguni. Umri mfupi katika ulimwengu huu, aliopewa na Muumba na miili ya wanadamu waliyopewa kama zawadi na Mwenyezi Mungu haitakikani wamsahau Mola wao. Maisha ya kudumu na umbo timilifu yatapatikana katika maisha ya Akhera tu. Qur'an inafafanua hili katika aya isemayo:

‘Basi vyote mliyopewa ni starehe ya maisha ya dunia tu, lakini kilichoko kwa Mwenyezi Mungu ni bora na chenye kudumu. Watahistahiki wale walioamini na wakawa wanamtegemea mola wao tu. (Ash-Shuura: 36).

Katika aya nyingine, lengo halisi la ulimwengu huu limefafanuliwa kama ifuatayo:

Juani ya kwamba maisha ya dunia hii ni mchezo na upuuzi na pambo la kufahamishana baina yenu, kufahamishana kwa mali na watoto. Ni kama mimea inastawi vizuri wakati wa mvua, hili huwafurahisha wenye mashamba, kisha hunyauka ukaiona imepiga umanjano, kisha inakuwa mabua. Na akhera kuna adhabu kali, na msamaha wa Mwenyezi Mungu na radhi. Na hayakuwa maisha ya dunia ila ni starehe idanganyayo: (Al-Hadyd:20).

Kwa muhtasari katika ulimwengu huu, Mwenyezi Mungu, kama dalili ya kuonesha nguvu yake zisizo kikomo na elimu yake iliyopea, ameumba vitu vingi vizuri na vya kustaajabisha, na hali kadhalika vitu dhaifu mno. Vitu vya kudumu na bora kupita kiasi ni kinyume cha kanuni za ulimwengu huu. Hakuna akili ya mwanadamu inayoweza kufikiri pamoja na maendeleo ya teknolojia na ufundi uliofikiwa, kuweza kubadili kanuni hii ya Mwenyezi Mungu. Ndivyo hivyo ili watu wapiganie kufikia maisha baada ya kufa ni kuonesha shukurani na kumtukiza Mwenyezi Mungu. Aidha imekuwa hivyo ili watu waweze kutanabahi kuwa zawadi hizi tulizojaliwa nazo si za ulimwengu huu wa muda bali ni zawadi kwa ajili ya ulimwengu wenye kudumu ulioandaliwa kwa ajili ya waumini. Katika Qur'an hayo yamebainishwa kama ifuatayo:-

‘Lakini ninyi mnapenda zaidi maisha ya dunia. Hali ya kuwa ya Akhera ni bora na yenye kudumu.’ (A’laa:16 - 17).

Aya nyingine inasema: ‘Hayakuwa maisha hayo ya dunia ila ni upuuzi na mchezo; na nyumba ya Akhera ndio maisha hasa: Laiti wanalijua (Ankabuti:64)

Kuna mpaka mwembamba sana baina ya ulimwengu huu (ambao ni wa muda) na maisha halisi ya Mwanadamu (Akhera). Kifo ndicho kinachonyanyua pazia hili. Kutokana na kifo, mtu anakata uhusiano na mwili wake na dunia hii, na kisha anaanza maisha ya milele na umbile lake halisi za asili ni hizo zinazohusu maisha baada ya kufa.

Kukonda, kutokamilika na kutodumu ni miongoni mwa kanuni za ulimwengu huu, hivyo si halisi na zisizobadilika. Kanuni halisi zimefumwa katika mfano ambao msingi wake mkuu ni kutokuwa na mwisho, yaani ni za milele. Kakuna kufa na ni zenye ubora wa hali ya juu kabisa.

Kwa maneno mengine, iliyokawaida ni maua yasiyonyauka, mtu asiyezeeka, matunda yasiyooza. Kanuni halisi huweka taratibu za utambuzi wa haraka juu ya yale anayopenda mwanadamu ikiwemo kuondolewa maumivu, ugonjwa, kutokwa jasho na hata kuhisi baridi. Hata hivyo, kanuni zisizo za kudumu (za muda) ndizo zinazotawala ulimwengu huu wa muda, wakati ambapo sheria halisi zinahusiana na ulimwengu wa maisha yajayo. Yote tunayokumbana nayo yasiyo na utimilifu na yenye mapungufu katika dunia hii yapo kutokana na mpango wa makusudi wa kupindisha hizo kanuni halisi.

Kuendelea kwa kanuni halisi baada ya zile za muda, zijulikanazo kama kiama au maisha baada ya kufa sio mbali sana kama inavyofikiriwa. Mwenyezi Mungu anaweza akakatisha maisha ya mwanadamu wakati wowote ule akipenda. Hapo hapo mja atakuwa amekwisha fika katika ulimwengu huo uliotawaliwa na kanuni za kudumu. Mpito huo unaweza kuwa ndani ya muda mfupi mno, kiasi cha kupepesa jicho. Hii ni sawa na kuamka kutoka kwenye njozi. Aya ya Qur'an inafafanua kuhusu umri katika dunia hii kwa kusema:

Atasema 'Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hisabu ya miaka? Watasema, 'Tulikaa siku moja, au sehemu ya siku.' Basi waulize wale wajuao hesabu.' Atasema, 'Ninye hamkukaa humo ila kidogo tu, laiti mngalikuwa mumejua. Je, mlidhani ya kwamba tumekuumbeni bure na ya kwamba ninyi kwetu hamtarudishwa? (Al-Muuminun: 112 - 115).

Wakati kifo kinapowadia, njozi nazo hufikia ukomo na mwanadamu huanza maisha halisi. Mwanadamu ambaye ameishi duniani kwa kitambo kifupi mno, kiasi cha kupepesa jicho, anakuja mbele ya Mwenyezi Mungu kuhesabiwa matendo yake.

Kama katika maisha yake alizingatia kifo na akaishi kwa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Katika Qur'an wale watakaopewa kitabu 'kwa mkono wa kulia' wamenukuliwa kama ifuatayo:-

'Basi ama yule atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kuume atasema 'Haya someni daftari langu.' Hakika mlifua ya kuwa nitapokea hisabu yangu. (Al-Haqqah: 19 - 20).

WASIOJIFUNZA KUTOKANA NA KIFO HALI YAO HAPA DUNIANI NA HUKO AKHERA

Wengi katika watu hawana dhana kamili juu ya kifo. 'Kifo ni pale maisha yanapokwisha' ni miongoni mwa maneno yao. Tukipiga hatua moja mbele, mwingine anadhani kuwa ni pale maisha yanayofuatia yanapoanzia. Ufahamu huu mfinyu humfanya kafiri kufinyanga kila kitu anachotaka

katika kipindi hiki kifupi cha maisha haya. Ndio maana wale ambao hawatanabahi juu ya maisha baada ya kufa, wanaotaka kufanya kila liwezekanao katika dunia bila kujali kuwepo kwa upande wa pili. Si wenye kutofautisha zuri na baya. Wanatafuta kutosheleza matamania yote ya nafsi zao katika uso wa dunia hii. Hali hii imeegemea katika fikra kwamba kifo kinahitimisha furaha na starehe za mwanadamu. Haamini kuwa bado wana miaka mingi usoni, wanayofukuzia mipango ya muda mrefu. Wanadhani kuwa wao wana akili nyingi mno huku wakiwadhanika waumini walio na imani isiyotetereka juu ya Mwenyezi Mungu na Akhera na hivyo kujiandaa vyema, kuwa hawana busara. Hii ni moja ya njia pevu itumiwayo na shetani katika kumghilibu Mwanadamu. Mwenyezi Mungu anatutaka tuzingatie hali hii ya kughilibiwa katika aya zifuatazo:-

‘Anawaahidi na anawatumainisha; kwani shetani hawaahidi ila udanganyifu. (An-nisaa:120).

Kwa hakika wale wanaorudi kimgongomgongo baada ya kuwabainishia uongofu, shetani amem danganya; na (Mwenyezi Mungu) anawapa muda (Muhammad:25).

Wakitafuta kujikusanyia mali, jaha na mengineyo, katika dunia hii kama kwamba maisha haya ni ya milele, makafiri huyachulia maisha kama mashindano. Katika uhai wao wote, hujivunia mali na watoto. Majivuno haya huwapa utukufu wa kujitengezea ambao huwahamisha kabisa kifikra na hivyo kuacha kufikiria Akhera. Hata hivyo aya zifuatazo zinadhahirisha walipoegemea kwa sababu ya upotofu wao:-

‘Je wanafikiri ya kuwa yale tunayowapa mali na watoto ndio tunawatangulizia katika kheri? Hapana, lakini hawatambui.’ (Muuminuun: 55-56).

Mwanadamu yampasa kuendeleza mali na watoto na kuvijaalia ndio vivutio vyake vikuu ya maisha. Allah anatoa onyo hili kwa kusema:-

‘Yasikufurahishe mali yao wala watoto wao. Anataka Mwenyezi Mungu awaadhibu kwa hayo katika maisha ya dunia, na zitoke roho zao, na hali ya kuwa ni Makafiri.’ (At-tawbah:55).

Mwenyezi Mungu amepa mwanadamu maonyo na ujumbe mwingi ili kwa huo atanabahi juu ya kifo na Akhera. Katika aya moja, Mwenyezi Mungu anatutaka tuzingatie majaribu au mitihani tunayoipata kama ni sehemu ya kuonywa.

Je hawaoni kwamba wanatiwa mitihani kila mwaka mara moja au mbili? Kisha hawatubu wala hawakumbuki (At-Tawb:126)

Kwa hakika watu wengi hupata mitihani, ili waweze kuomba msamaha mara kwa mara na kujichunga kwa kurejea. Haya yanaweza kutokea mara chache pengine mara moja au mbili katika mwaka kama ilivyobainishwa katika aya. Badala yake, inaweza ikawa ni mikiki mikiki au matatizo ya

kila siku. Mwanadamu anashuhudia ajali, vifo au majeruhi. Magazeti na vyombo vingine vya habari hutoa taarifa nyingi kuhusu kifo na rambirambi. Katika muonekano wa matukio kama hayo, mwanadamu anapaswa akumbuke kwamba majanga yanaweza kutokea wakati wowote na muda wowote ule. Pia mtihani wake unaweza ukafikia mwisho. Kuchukua hadhari kama hizo humfanya mja kumuelekea Mola wake kwa moyo mkunjufu, huku akiomba kinga kutoka kwake na akiomba msaada wa kusamehewa kutoka kwake kadhalika.

Mafunzo Muumini anayoyapata kutokana na majanga anayokumbana nayo ni yenye kuendelea. Hata hivyo, matukio hayo hayo huwa na athari tofauti kwa mtu ambaye hana imani (kafiri). Kwa kuhofishwa na fikra juu ya kifo, hujaribu kujisahaulisha na kifo. Kwa kufanya hivyo hutafuta nafuu. Hata hivyo njia hii ya kujilaghai, humsababishia maangamizi na madhara. Hiyo ni kwa sababu, Mwenyezi Mungu huwaokoa na kuwapa muda hadi muda maalum uliowekwa. Na muda huu kinyume na wanavyo fikiri, huwadhuru wao. Mwenyezi Mungu anasema:

‘Na lau Mwenyezi Mungu anawatesa watu kwa sababu ya maasi yao; asingalimwacha hata mnyama mmoja juu ya ardhi; lakini anawaakhirisha mpaka muda uliowekwa. Na unapofika muda wao hawawezi kukawilia saa moja wala hawawezi kuutangulia. (An-Nahl”61)

Katika aya nyingine Qur’an inabainisha:

‘Wala wasidhani wale waliokufuru kwamba huu muda tunaowapa ni bora kwao. Hakika tunawapa muda na wanazidisha madhambi. Na itakuwa kwao adhabu ya kuwadhalilisha. (Al-Imran: 178)

Mtu aliyeghafilika ambaye hupata mafunzo hata pale kifo kinapomchukua mtu aliyekaribu naye, anakuwa mwaminifu kwa kumuelekea Mwenyezi Mungu pale yeye mwenyewe anapokuwa katika misikosuko ya kifo.

Saikolojia hii inaelezwa ndani ya Qur’an kama ifuatayo:-

‘Yeye ndiye anayekuedesheni katika bara na bahari. Hata mnapokuwa katika majahazi na yanakwenda nao kwa upeo mzuri na wakafurahi zao; mara upepo mkali unayajia na mawimbi yanawajia kutoka kila upande, na wanaanza kufikiri ya kwamba wametingwa. (Hapo ndipo) wanapomuomba Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia utii. Ukituokoa katika haya, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru. (Yuhus:22).

Akiwa ni mwenye kukata tamaa, mwanadamu hujaribu tena kufanya kama hayo wakati wa kufa. Wakati huo muda uliokadiriwa kwake umekwisha wadia.

Na ungaliwaona waovu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao, ‘Mola wetu’ Tumekwisha kuona na tumekwisha kusikia, basi turudishe, tutafanya vitendo vizuri; hakika tumeyakinisha’. Na tungalitaka tungempa kila mtu uongofu wake, lakini imehakikika kauli iliyotoka kwangu. Kwa yakini nitaijaza Jahannam kwa wote hawa; majini na watu. ‘Basi ionjeni (adhabu) kwa sababu ya kusahau makutano ya siku yenu hii. Na sisi tutakusahauni.; na onjeni adhabu idumuyo kwa yale mliyokuwa mkiyatenda. (As-Sajidah:12-14).

‘Nao humo watapiga kelele, ‘Mola wetu! Tutoe humu! Tutafanya vitendo vizuri visivyokuwa vile tulivyokuwa tukifanya.’ “Hatukukupeni amri ya (kuweza) kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Mwonyaji. Basi onjeni (adhabu) madhalimu hawana wa kuwanusuru (Al-Fatir:37).

Juhudi hizi zisizotia matumaini huko akhera na mwisho huo uumizao ni matokeo ya kupuuza kwa mwanadamu na kukosa shukurani kwa kutozingatia lengo halisi la kuwepo kwake hapa duniani na thamani yake. Yeyote asiye na imani hawezi kupata mafundisho kutokana na matukio yanayaomzunguukia; hawezi kusikiliza maonyo yanayotoka kwa Mwenyezi Mungu, akijisingizia ujinga juu ya yale ambayo moyo wake unayajua au kwa makusudi akakanusha na akaona kifo kuwa hakiwezi kumtokea. Anakubaliana na matakwa ya upande dhaifu wa nafsi yake kuliko kupata ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Yote hayo hatimae hujitokeza wakati kifo chake kimewadia na hivyo kushikwa na bumbuaazi na kuwa mwenye kukata tamaa na kujikuta katika hali iliyoelezwa katika aya hapo juu. Hivyo, kifo kabla hakijamkabili yeyote, lazima mja aamke katika lindi la usingizi wa kughafilika (kukosa mwelekeo), kwani wakati wa kukata roho itakuwa fursa hiyo haipo tena. Hii ni kutokana na kuchelewa kuamka na kuzindukana na hivyo uwezekano kufifilika.

Na toeni katika yale tuliyokupeni, kabla mmoja wenu hayajamjia mauti, kisha akasema, ‘Mola wangu! Huniakhirishi muda kidogo nikatoa sadaka na nikawa miongoni mwa watendao mema? Lakini Mwenyezi Mungu haiakhirishi nafsi yoyote inapokuja ajali yake: Na Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda. (Al-Munafiquun: 10-11).

Mtu yeyote mwenye akili muda wote anawaza juu ya kifo kuliko kujiepusha na fikra juu ya kifo. Ndipo tu anaweza kupata ridhaa ya Mwenyezi Mungu na kuepushwa na udhaifu wa nafsi na pia vitimbi vya shetani katika kumhadaa na maisha haya yadanganyayo. Kwa hakika, kuyafanya maisha ya dunia hii ndilo lengo pekee la maisha ni hatari kubwa kwa mwanadamu. Mtume Muhammad (SAW)amea amewakumbusha hili wafuasi wake katika dua yake:

‘Usitujaalie maisha ya dunia hii yawe ndio ya kutushughulisha zaidi kuliko yale tunayoyafahamu. (imesimuliwa na Abdallah bin Umar - *At-tirmidh*, 783).

KUJIANDAA KWA KIFO

Ulimwengu huu ni mahali ambapo mwanadamu anafundishwa. Mwenyezi Mungu amempa majukumu mengi na kumfahamisha mipaka aliyomuwekea. Endapo Mwanadamu atachunga mipaka hii, atafuata maamrishi yake na kuacha makatazo yake, atafikia hali ya ukomavu na hali bora ya utambuzi na busara. Kwa kupata sifa hizo, muumini huonyesha subira ya hali ya juu bila kujali yanayomsibu; humuelekea Mwenyezi Mungu tu na kumuomba yeye peke yake msaada. Hizi ndio njia pekee za kumtukua Mwenyezi Mungu na kuhisi hasa kujisalimisha kwake kutoka ndani ya nafsi na imani isiyo na ukomo juu yake. Kwa kujua thamani halisi ya neema alizopewa na Mwenyezi Mungu hudhihirisha shukurani za dhiti kwa Mwenyezi Mungu na kujisikia yuko karibu naye.

Matokeo yake, anakuwa Muumini muadilifu akitunukiwa sifa nzuri za busara na tabia njema. Si hivyo tu, anakuwa aina ya mtu anayestahili kuingia peponi, mahali palipotimia kwa Uzuri na Ubora.

Lakini endapo mtu hatapata Elimu juu ya hakika ya dunia hii, atashindwa kuonesha mwenendo mzuri na japo hali bora kutokana na mtazamo wa kivotu utawekwa mbele yake, atabakia katika hali zote za mtu mwenye kushindwa. Kwa hakika nabii Adam (amani iwe juu yake) ameletwa duniani kupokea mafunzo na akapewa mtihani maalum ulioandikwa na Mwenyezi Mungu kumuandaa kwa maisha yake ya milele. Mwishoni, akaibuka kuwa mtu mpevu katika tabia njema na mwenendo mzuri wa kupigiwa mfano ndani ya Qur'an. Mwanadamu huyu anaendelea kujaribiwa kwa matukio mengi juu yake. Endapo atafaulu katika kuyaendea atapata malipo mema ya kuendelea huko Akhera, lakini atakapofeli, malipo yake akhera itakuwa kuadhibiwa milele. Hakuna mwanadamu hata mmoja ajuae mwisho wa kujaribiwa kwake itakuwa ni lini. Kwa maneno ya Qur'an:-

‘Na nafsi yoyote haitaweza kufa ila kwa amri ya Mwenyezi Mungu kwa ajali iliyowekwa. Na anayetaka malipo ya duniani tutampa, basi, hapa; na anayetaka malipo ya Akhera tutampa huko, na kwa yakini tutawalipa wanaoshukuru. (Al-Imraan: 145).

Kipindi hiki kinaweza kuwa kirefu, na vile vile kinaweza kuwa kifupi. Ukweli ni kuwa, hata kama kinakuwa kirefu, ni mara chache kuvuka miaka 70 au 80. Ndio maana, kuliko kujitumbukiza katika kutengeneza mpango wa muda mrefu, mwanadamu, anatakiwa aongozwe na Qur'an na aishi kwa kanuni ya hiyo Qur'an, kwa kujua kwamba, atakwenda kuwasilisha hesabu yake huko Akhera.

Kinyume chake, kushindwa kufanya maandalizi kwa ajili ya Akhera, ni kukosa nafasi moja ya pekee aliyotunukiwa na lengo hili, na hivyo kustahiki kutumbukizwa motoni milele. Haya yatakuwa majuto ya hali ya juu, yenye kuumiza. Isisahaulike kwamba kukosa kuingia peponi milele hakuna sehemu nyingine ya kuingia isipokuwa motoni. Ndio maana kila sekunde inayopotea katika mchezo katika dunia hii ni hasara kubwa na hatua potofu iliyofuatwa kuelekea kwenye maangamizi na mwisho mbaya. Kwa kuwa hivi ndivyo ilivyo, ukweli huu utangulizwe kwa hilo linalotaka kufanywa hapa ulimwenguni. Kama vile mwanadamu afanyavyo maandalizi ya kukabiliana na yale yanayokuja kutokea mbeleni hapa duniani, vivyo hivyo inapasa kutumia juhudi zaidi katika kufanya maandalizi kwa ajili ya

maisha yajayo. Hii ni kwa sababu wale watakaokufa si wengine bali ni binadamu hawa hawa. Mwanadamu atashuhudia kila kitu kitakachotokea baada ya kufa kwake. Hivyo somo hili linamhusu kila mwanadamu, kwa maneno mengine kila nafsi. Kwa wale wanaotafuta ukombozi wa milele, Mwenyezi Mungu anaamrisha yafuatayo:-

‘Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu; na kila mtu aangalie anayoyatanguliza kwa ajili ya kesho; na mcheni Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu anazo habari za yote mnayoyatenda. Wala msiwe kama wale waliomsahau Mwenyezi Mungu, na akawasahaulisha nafsi zao. Hao ndio maasi makubwa. (Al-Hashir:18-19).

KUFUFULIWA

Qur’an inafahamisha kuwa:-

‘Lakini mtu anataka tu kuyakataa yaliyombeke yake. Anauliza,’ Itakuwa lini hiyo siku ya kiama? Wakati litakapoparama jicho. Na mwezi utakapopatwa. Na jua na mwezi vikapokutanishwa. Mtu atasema siku hiyo pa wapi mahali pa kukimbilia?’ Hakuna mahali pa kukimbilia!’ Siku hiyo marejeo ni kwa Mola wako. (Al-Qiyamah:5-12).

IMANI JUU YA MAISHA YAJAYO

Imani juu ya maisha baada ya kufa ni moja katika nguzo muhimu za Imani. Katika sura ya kwanza ya Qur’an, Surat Fat-ha, baada ya sifa yake Mwenyezi ‘Mwingi wa Rehema’ na ‘Mwingi wa Ukarimu’, Mwenyezi Mungu anaeleza kuwa ‘Yeye ni Mfalme wa Siku ya Malipo’. (Al-fatha 3). Katika aya ya tatu ya sura inayofuata, inaeleza kuwa moja ya Sifa za waumini ni ‘... Wale wenye kuamini ghaibu (yasiyoonekana)...’ (Al-Baqarah:3).

Hii dhana ya ‘ghaibu - visivyoonekana’ pia inajumuisha kufufuliwa baada ya kufa, siku ya kiama, pepo na moto. Kwa muhtasari kila linalohusiana na maisha baada ya kufa. Kwa hakika katika aya ya nne ya Surat Baqarah maneno ‘... wana hakika juu ya akhera; msisitizo maalum umewekwa kuhusu imani juu ya maisha baada ya kufa. Imani juu ya visivyoonekana ni alama juu ya Imani ya Akhera ua Kiama na kwa hakika ni muhimu mno. Aina ya imani juu ya akhera kama ilivyoainishwa ndani ya Qur’an inatoa ushahidi wa uaminifu na ukweli wa Muumin. Aliye na imani juu ya Akhera tayari ameweka imani yake isiyo na pingamizi kwa Mwenyezi Mungu, katika kitabu chake na kwa mtume wake. Mja kama huyo anajua kwamba Mwenyezi Mungu ana uwezo juu ya kila kitu na kwamba maneno yake na ahadi zake ni kweli. Matokeo yake, kamwe hawezi kuwa na shaka juu ya Akhera. Kabla ya kuona na kushuhudia hakika hii, aliweka imani yake kwa viwili hivi (uwezo na ahadi ya

Mwenyezi Mungu) kama kwamba tayari amekwisha Dua. Haya ni matokeo yanayopatikana kutokana na Imani na matarajio aliyoweka kwa Mwenyezi Mungu na busara aliyotunukiwa.

Zaidi ya hayo, imani isiyotetereka juu ya Akhera, hutakasa aina zote za mashaka, yanayohusishwa na imani juu ya kuwepo Mwenyezi Mungu na pia katika sifa zake, kama iliyofafanuliwa katika Qur'an, na matarajio timilifu kwake na kujisalimisha kwake. Imani hii pia humfanya mtu amjue Mwenyezi Mungu na amkubali katika uhalisia wa kumkubali. Aina hii ya Imani Mwenyezi Mungu huichukulia kuwa ni yenye thamani mno. Katika kurasa za mbele itadhihirika kuwa ushawishi mkubwa katika kuridhika kwa mwanadamu ni kwa kutegemea kuleleka kwenye imani ya kweli juu ya maisha baada ya kufa.

Sehemu nyingi ndani ya Qur'an, zipo rejea kuwa makafiri ukanushaji wao juu ya akhera na kutotoa uamuzi juu ya kuthibitika kwake, ndiko kunakowafanya wazidi kuangamia. Kwa hakika wengi katika makafiri wanaamini juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu - Lakini kinachowapoteza wengi wao si suala linalohusu kuwepo kwa Mwenyezi Mungu bali ni kuhusu sifa zake. Miongoni mwao huamini kuwa awali Mwenyezi Mungu huumba kila kitu na kuwaacha viumbe wawe wanatenda kutokana na waonavyo wao. Wapo baadhi ambao hushikilia kuwa Mwenyezi Mungu Amemuumba Mwanadamu, lakini ni mwanadamu mwenyewe anayeamua hatima yake. Pia lipo kundi lingine ambalo hushikilia kuwa Mwenyezi Mungu hajui mawazo ya ndani na siri za watu. Wengine huamini juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, lakini hupinga wazo la kuwepo kwa dini au mfumo wa maisha aliyoweka Muumba ambao wanaadamu hutakiwa kuufuata. Kundi hili la mwisho linaelezwa na Qur'an kama ifuatayo:-

‘Na hawakumhishimu Mwenyezi Mungu kama inavyotakiwa kumhishimu, waliposema: “Mwenyezi Mungu hakuteremsha chochote juu ya binadamu yeyote: (Al-Anam:91).

Matokeo yake, badala ya kukanusha moja kwa moja kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, ‘Hawampi Mwenyezi Mungu kipimo chake halisi na hivyo basi, huishia katika kukanusha akhera na kuishi bila ya imani. Kwa hakika, kundi linalokanusha moja kwa moja kuwepo kwa Mwenyezi Mungu ni dogo na kundi kubwa hupendelea kutilia shaka katika kushawishika na yale wasiyoamini. Ndio maana Qur'an haizungumzii sana juu ya wale wanaokanusha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu. Badala yake zitaonekana rejea nyingi juu ya watu wanaomshirikisha Mwenyezi Mungu na wanaokanusha kufufuliwa, siku ya hukumu, pepo, moto na yale yote yanayohusiana na imani juu ya Akhera. Japo akhera ni hakika ambayo milango mitano ya fahamu haiwezi kuthibitisha, Mwenyezi Mungu ameumba mifano mingi ambayo fikra za mwanadamu zinaweza kuelewa. Ni ukweli usiopingika kwamba hitajio tangulizi ili mtu afaulu mtihani hapa ulimwenguni, lazima afahamu ukweli huu, si kwa kupitia milango ya fahamu, bali busara na maumbile.

Mtu yeyote wa kawaida, baada ya kutafakari, kwa wepesi tu hugundua kwamba vyote vinavyomzunguuka, akiwemo yeye mwenyewe havitajitokeza kwa bahati nasibu bali ni kutokana na Mwenye Nguvu za hali ya juu kabisa, mdhibiti na mwenye utashi yaani Muumba. Kisha, mara

huzingatia na kufahamu kuwa kuumbwa kwa akhera ni jambo jepesi mno kwa Mwenyezi Mungu. Zaidi ya hapo atatambua kwamba, kutokana na busara na uadilifu wa Mwenyezi Mungu hufanya hitajio la kuwepo Akhera. Japo hili liko wazi mno, lakini wale wanaokanusha maamrisha ya Mwenyezi Mungu, hawapendi wazo la kuwa watafufuliwa kutoka katika wafu. Kama yule anayetumia maisha yake kuyatosheleza matashi ya nafsi yake. Hayuko radhi kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu na kupokea hesabu ya matendo yake aliyofanya katika kipindi cha uhai wake wote. Ndio maana, japo ana yakini kwamba Mwenyezi Mungu yupo, atahiyari kuchagua kwamba akandamize kila fikra inayomjengea utambuzi huo na hivyo kujichanganya mwenyewe. Katika kuweka mawazo yake kwenye ufinyu huo, kafiri huanza bila kutumia busara, kuparaganyisha na kukanusha kufufuliwa na Akhera.

‘Na akatupigia mfano, na akasahau kuumbwa kwake - akasema ‘Nani atakayeihisha mifupa na hali imesagika?’ (Yasin:78).

Hata hivyo swali hili limebuniwa kwa lengo la kukwepa ukweli na kujikweza katika kujihadaa, linajibu lililo jepesi mno.

‘Sema: “Ataihuisha yule aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni mjuzi wa kila (namna ya) kuumba. (‘Yasin: 9).

Ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu ameweka wazi kwamba milinganyo kama hiyo isiyo na mantiki ni dhana zitokanazo na makafiri:

‘(waungu) wa wale wasioamini Akhera wana mifano mibaya (ya kupigiwa). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye sifa tukufu; naye ni mwenye nguvu Mwenye hekima (Al-Nahl:60).

Wengine, kwa upande wao wamejaribu kuhalalisha misimamo yao kwa kutoa kile kinachoitwa - ufafanuzi.

‘Wanasema, “Je! Kweli tutarudishwa katika hali (yetu) ya kwanza? Hata tukiwa mifupa mibovu?’ Wanasema (kwa stihizai)” Basi marejeo haya ni yenye khasara: (Naziat: 10 - 12).

Kwa hakika, pamoja na kushawishika juu ya hilo, hawajizuilii kueleza kwamba kuwepo kwa akhera hakuendani na malengo yao ya maisha. Kafiri hujenga busara zake kwa kutegemea matamaniao ya nafsi yake. Kwa kuona udhaifu wa madai yake mwenyewe, bado huliendea suala hili kwa kulikwepa kabisa na kwenda mbali zaidi kwa kusaka namna ya kujisaidia kisaikolojia.

‘Nao (wakaapa) kwa jina la Mwenyezi Mungu kwa kiapo chao cha nguvu (kwamba) Mwenyezi Mungu hatawafufua wafao. Kwa nini? Ni ahadi iliyolazimika kwake, lakini watu wengi hawajui. (Nahl:38).

Kwa kuyachukulia matamano na fikra zao kwamba ndio miungu, watu hawa hutamka maneno ili kuondoa hisia zote kwamba kwa halali na haramu na kinyume chake wanatafuta hifadhi kwa vile walivyovijaalia kuwa ndio miungu yao.

Mwenyezi Mungu anafafanua tabia za watu hawa wanaokanusha kuwepo kwa Akhera:

‘Na bila shaka tumewaambia moto wa Jahannam wengi katika majini na wanadamu: Nyoyo wanazo lakini hawafahamu kwazo, na macho wanayo lakini hawaoni kwayo, na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika. (A’araf:179).

Katika sehemu nyingine ya Qur’an, hali ya watu hawa imefafanuliwa kama ifuatavyo:-

‘Je! umemuona yule aliyefanya yale anayoyataka yeye, kuwa ndio Miungu wake; na Mwenyezi Mungu akamuacha apotee pamoja na kuwa ana ujuzi; na akapiga muhuri juu ya masikio yake na moyo wake; na kumtia kitanga machoni pake; basi nani atamuongoza baada ya Mwenyezi Mungu? Basi je hamkumbuki? Na walisema: ‘Haukuwa (uhai) ila ni uhai wetu huu wa dunia, tunakufa na tunaishi, wala hakuna kinachotuangamiza isipokuwa (huu huu) ulimwengu; wala wao hawana ilimu ya hayo, wanadhani tu. (Al-Jathiyah: 23 -24).

HALI HALISI YA MAISHA YA KIDUNIA

Makafiri hudai kuwa huwezi kufahamu baadhi ya mambo kwa kutumia busara. Kifo, kufufuliwa na maisha ya Akhera ni miongoni mwa mambo hayo. Mwanadamu anaweza kuyahusisha matukio haya na nadharia yake ya matukio ya usingizi na njozi. Yeyote anayekazania kukanusha kwamba hawezi kufufuliwa baada ya kufa, na pia akasisitiza kuepukana na fikra za kifo, kwa hakika hana habari kwamba anaonja kifo kila usiku na pia kuonja kufufuka kila asubuhi anapotoka usingizi kama ifuatavyo:-

‘Mwenyezi Mungu hutakabadhi roho wakati wa mauti yao. Na zile zisizokufa (pia anazitakabadhi) katika usingizi wao. Basi huzizuia zile alizozikidhia mauti, na kuzirudisha zile nyingine mpaka wakati uliowekwa. Bila shaka katika hayo yamo mazingatio kwa watu wanaotafakari. (Az-zumari: 42).

Naye ndiye aliyekufisheni wakati wa usiku, na anayafahamu mnayo tenda wakati wa mchana; kisha yeye hukufufueni humo ili muda uliowekwa umalizike. Kisha, kwake tu (Mwenyezi Mungu) marudio yenu. Akwambieni (yote) mliyokuwa mkiyafanya: (Al-An-am: 60).

Katika aya hizo hapo juu, hali ya usingizi imerejewa kama ‘Kifo’. Hakuna kilichobainisha wazi kati ya ‘kifo’ na usingizi. Kipi tena kinachotokea wakati wa usingizi ambacho kinaoanishwa na kifo?

Usingizi ni kusafiri kwa roho ya mwanadamu kutoka katika mwili (kiwiliwili) ambapo hurejea mara mja anapoamka kutoka katika usingizi. Katika kuota, kwa upande mwingine, roho huwa na mwili mwingine kabisa na kuanza kupata muundo mwingine kabisa. Kamwe mwanadamu havezi kufikiri kwamba haya yanayotokea ni njozi. Anahisi woga, kujuta na maumivu. Ana hamaki au kuhisi furaha tele. Pia, anakuwa na uhakika kabisa kwamba, yale yanayojitokeza kwake ni ya kweli na mara nyingi hutoa hisia zilezile kama yuko hadhiri. Kama ingewezekana kuingilia kati kutoka upande wa nje na kumuambia mwenye kuota ndoto kwamba yale anayoyaona ni hisia na njozi tu, angeweza kudharau na kupuuzia kuwa anachezwa shere tu. Hata hivyo ukweli ni kwamba maono haya hayana uhusiano wa wazi na yale yanayotokea hapa uliwenguni na kwamba yale anayoyaona katika njozi zake ni katika jumla ya picha na mapokezi ambayo Mwenyezi Mungu ameyaelekeza katika nyoyo za wanadamu.

Nukta muhimu anayotakiwa kuzingatia kichwani ni kuwa, kanuni hiyo hiyo ndiyo inayofanya kazi katika muda ambao mwanadamu yuko macho. Mwenyezi Mungu anathibitisha kuwa njozi ziko katika milki yake na udhibiti wake. Hebu mwanadamu aangalie aya ifuatayo:-

‘(Kumbuka) Mwenyezi Mungu alipokuonesha katika usingizi wako (kwamba wao makafiri) ni wachache; Na kama angelikuonesha kwamba wao ni wengi mngalivunjika nyoyo na mngalizozna katika jambo hilo. Lakini Mwenyezi Mungu akakulindeni. Bila shaka yeye ni mjuzi wa yaliyomo vifuani. (Anfal: 43).

‘Na (kumbukeni) alipokuonesheni machoni mwenu mlipokutana kwamba wao ni wachache (ili mjasirike kupigana nao), au akakufanyeni ninyi kuwa wachache (mno kabisa) machoni mwao (waone upuuzi kupigana kwa hima na watu wachache kama ninyi, Mwenyezi Mungu amefanya hayo) ili alitimize jambo aliloamrisha litendeke. Na mambo yote hurejeshwa kwa Mwenyezi Mungu. (Anfal:44).

Hutoa ushahidi ulio wazi kuwa kanuni hiyo hiyo inayofanya kazi hapa duniani katika maisha ya kila kitu. Uhakika kwamba tunayoyapokea na picha tulizonazo kuhusu maada kwa ujumla wake hutegemea kutaka na kuumba kwa Mwenyezi Mungu na kwamba mbali na hayo, hakuna kuwepo kwa ulimwengu wa nje. Haya yameelezwa katika aya ifuatayo:

‘Hakika imepatikana alama kubwa kwenu (ninyi) katika yale makundi mawili yaliyokutana; kundi moja lilipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na jingine makafiri. (Makafiri) wakawaona (Waislam) zaidi kuliko wao mara mbili kwa kuona kwa macho, na Mwenyezi Mungu humtia nguvu, kwa nusra yake, amtakae. Kwa yakini katika hayo yamo mazingatio (makubwa) kwa wenye busara. (Al-Imran: 13).

Kama ilivyo katika njozi, kile kinachoonekana katika taratibu za kila siku na yale yanayodhaniwa yapo katika ulimwengu katika sura yake ya nje ni picha zilizopandikizwa katika nafsi za wanadamu toka kwa Muumba wao, sanjari na hisia alizowafanyia wazipokee kwa wakati mmoja. Picha na vitendo

vinavyofanywa na miili ya wanadamu sawa na zile za viumbe wengine, vipo kwa kuwa Mwenyezi Mungu ameumba picha zinazooana na kupokezana hatua kwa hatua. Ukweli huu umebainishwa katika Qur'an:-

Hamkuwaua ninyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaua, na hutupa wewe (mtume) ulipo tupa walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyeutupa. Aliyafanya haya Mwenyezi Mungu ili awape walioamini hidaya nzuri itokayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye. (Anfal:17).

Kanuni hiyo hiyo ya Mwenyezi Mungu ndiyo inayotumika katika kuumbwa kwa Akhera na picha na maono yanayohusiana. Wakati kifo kinapowadia, uhusiano wote kuhusu ulimwengu huu na mwili hukatika. Roho hata hivyo ni ya milele kwa sababu Mwenyezi Mungu ameipulizia. Kila kitu kihusianacho na uhai, kifo, kufufuliwa na maisha ya akhera inajumuisha mitazamo kadhaa inayoonwa na roho ya milele. Ndio maana, kutokana na hoja za msingi hakuna tofauti kubwa kati ya kuumbwa kwa ulimwengu huu na ile ya pepo au moto. Vivyo hivyo, mpito kutoka dunia hii kuelekea akhera hauna tofauti na kuamka kutoka usingizini na kuendelea na maisha ya kila siku.

Kwa kufufuliwa, maisha mapya huanza huko akhera akiwa mja na mwili mwingine. Mara hisia zihusuzo pepo au moto zinapodhihirishwa kwenye nafsi, mja huanza kuhisi hayo (ya peponi au motoni). Mwenyezi Mungu, Muumba wa picha zisizo na ukomo vivuli, sauti, harufu, vionjo vihusavyo maisha haya, pia, kwa utaratibu kama huo, utaumba picha zisizo na ukomo na hisia za peponi hali kadhalika za motoni. Kwa Mwenyezi Mungu, uumbaji, huo ni rahisi mno:-

‘Yeye ndiye) Muumba wa mbingu na ardhi pasi na ruwaza; na anapotaka jambo basi huliambia tu, ‘kuwa’; nalo huwa (Al-Bawarah: 117).

Hoja nyingine ya kuzingatia ni kwamba, kama ilivyo maisha katika ulimwengu huu yanaonekana kuwa yako wazi na mepesi kuliko ndoto, vivyo hivyo Akhera ikilinganishwa na maisha ya dunia hii. Pia, kama ndoto zilivyofupi kulinganisha na maisha ya dunia hii) ndiyo ilivyo kwa maisha ya dunia hii ukilinganisha na maisha ya Akhera. Kama inavyofahamika, muda au wakati haukutulia kama dhana ya awali ilivyokuwa, sayansi leo hii imethibitisha hili kuwa kuna nadharia ya mvutano (*Theory of Relativity*). Katika ndoto, tukio linaweza kudhaniwa kuwa kimechukuwa saa kadhaa kumbe limechukuwa sekunde chache tu. Hata ile njozi inayoonekana imetumia muda mrefu, hudumu kwa dakika chache tu. Hata hivyo yule aliyeota hudhani ametumia muda wa masiku au miaka kadhaa akiwa katika njozi hiyo.

Kuhusu muda, na kuonesha kuwa ni suala la kulinganisha na tukio; Qur'an inafafanua:-

‘Malaika na Jibril hupanda kwake katika siku ambayo muda wake ni miaka elfu hamsini. (Al-Maarij: 4).

Anapitisha mambo yote yaliyo baina ya mbingu na ardhi, kisha yanapanda kwake kwa siku moja tu ambayo kipimo chake ni myaka elfu mnyotumia ninyi katika kuhesabu kwenu (As-Sajdah: 5).

Mtu anayemaliza miaka mingi katika uliwengu huu, ukweli ni kwamba ameishi muda mfupi sana kulinganisha na nadharia ya muda ya Akhera. Majadiliano yafuatayo katika siku ya hukumu ni mfano mzuri:-

‘Atasema: ‘Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka? Watasema. ‘Tulikaa siku moja au sehemu ya siku’. Basi waulize wafanyao hesabu’. Atasema, ‘Ninyi hamkukaa ila kidogo tu, laiti mngalikuwa mnajua.’ Je mlidhani Tumekuumbeni bure na ya kwamba ninyi kwetu hamtarudishwa?’ (Al-Muuminun:: 112 - 115).

Kwa vile hali ni hii, ni dhahiri kuwa kupuuzia maisha ya milele kwa ajili ya kuendeleza maisha ya dunia hii ambayo ni ya muda tu ni uchaguzi mbaya. Hii itakuwa wazi zaidi pindi mja anapotafakari ufupi wa maisha ya dunia hii ikilinganishwa na akhera.

Kwa majumuisho, vitu vinavyoitwa maada na kuvijaalia kuwa vipo kwa uhalisia, si chochote bali ni hisia za mwanadamu alizopandikiziwa na Mwenyezi Mungu katika nafsi yake. Mtu anaamini kwamba mwili ni mali yake. Hata hivyo, mwili wenyewe ni kivuliau picha ambayo Mwenyezi Mungu ameipandikiza katika nafsi ya mwanadamu huyo. Mwenyezi Mungu anaweza kuibadili pindi akipenda kufanya hivyo bila kipingamizi chochote. Wakati mwili unapotoweka, ghafla nafsi huanza kuona picha mpya. Kwa lugha nyingine, wakati mtu anapokufa, pazia juu ya macho yake huondolewa na hivyo mtu kugundua kuwa kifo sio kutoweka kama mmoja wao alivyoamini. Haya yamebainishwa katika Qur’an kama ifuatayo:-

Na kutoka roho kutakapomjia kwa hali. (Hapo ataambiwa): ‘Haya ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.’ Na itapulizwa parapanda (Baragumu); hiyo ndio siku ya makamio. Na itakuja kila nafsi pamoja na mchungaji (wake) na Shahidi (wake). (Aambiwe) “Kwa hakika ulikuwa umo katika ghafla na jambo hili. Basi tumekuondolea (leo) pazia yako; kuona kwako leo kumekuwa kukali (Qaf:19-22).

Makafiri hapo watafikia kilele cha kufahamu vizuri ukweli:

‘(Na huku) wanasema: ‘Ole wetu! Nani aliyetufufua malaloni petu?’ (waambiwe) ‘Haya ndiyo yale aliyokuahidini (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema na waliyoyasema kwa haki mitume: (Tasin: 52).

Kuanzia hapo na kuendelea, makafiri watakuwa ni wenye kujuta kusikokuwa na mfano.

KUFA KWA ULIMWENGU

Ndani ya Qur'an, imeelezwa kuwa mbali na viumbwa vyote, ulimwengu pia utafikiwa na umauti. Si mwanadamu pekee aliye na uhai na umauti. Wanyama na mimea pia hufa. Pia sayari na nyota hufa. Kifo ni jambo linalotokea kwa kila kiumbe. Katika mpango wa Mwenyezi Mungu, watu wote, viumbe vyote vyenye uhai, dunia, jua mwezi na nyota, kwa muhtasari, ulimwengu wote wa maada utatoweka. Katika Qur'an, siku hii inaitwa 'Siku ya kufufuliwa.'

'... Siku watakaposimama watu (wote) mbele ya Mola wa walimwengu wote: (Al-Mutasffin: 6).

Kama vile ambavyo kifo cha mtu kinavyotisha, ndivyo hivyo hivyo kwa kifo cha ulimwengu. Katika siku ya kufufuliwa, wale ambao hawakuwa na imani, watakuwa, kwa mara ya kwanza, na hisia nzito juu ya Ukubwa wa Mwenyezi Mungu na nguvu zake. Ndio sababu siku ya kufufuliwa ni siku ya majuto, ya adhabu, ya kujuta, ya machungu, ya kuhangaika, ya kuchanganyikiwa kukubwa kwa makafiri. Mtu anayeshuhudia siku ya kufufuliwa atakuwa na woga kweli kweli. Woga huu usioelezeka ni mara mia moja uzito wake na zaidi kuliko woga wote mtu anaoweza kuhisi katika dunia hii. Qur'an inaeleza kwa undani hatua kwa hatua ya kile kitakachotokea siku ya kufufuliwa. Namna tukio hili kubwa litakavyokuwa na litakavyotokea kwa watu siku hiyo yamefafanuliwa kwa namna inayogusa moyo.

KUPIGWA PARAPANDA KWA MARA YA KWANZA

Siku ya kufufuliwa huanza baada ya parapanda kupulizwa. Hii ni alama kuwa mfumo wa dunia na ulimwengu wote unabadilika. Unakuwa mfumo mwingine. Mwisho wa maisha ya dunia hii ndio mwisho. Wakati huo huo mwanzo wa maisha mengine umewadia. Hii ni nukta muhimu kuwa hakuna kurejea tena katika mfumo huu ambao tayari umekwisha vurugwa na kuharibiwa kabisa. Hii ni sauti inayotambulisha kwamba maisha ya duniani hapa yamekoma kwa viumbe vyote na kwamba maisha halisi yameanza. Hii ni sauti ya mwanzo inayoamsha woga usio na mazongezongwe, kitisho na kuchanganyikiwa katika nyoyo za makafiri. Sauti hii inaashiria mwanzo wa masiku magumu ambayo yataendelea hivyo bila ukomo. Katika Surat Maddaththir, siku hii imerejewa kama ifuatavyo:-

'Hapo tarumbeta litakapopulizwa, siku hiyo itakuwa ngumu, hakuna nafuu kwa makafiri. (Maddaththir: 8 - 10).

Sauti ya tarumbeta kwa hakika itasababisha mtetemeko mkubwa na kukosekana utulivu miongoni mwa makafiri. Hali ya milio isiyoelezeka na kufikirika bila ya chanzo kilicho wazi itakapopenya ulimwengu wote bila kusalia sehemu. Hivyo kila mtu atajua kuwa Mwanzo wa 'Kitu fulani umewadia'.

Kukosekana kwa utulivu huo kutasababisha kafiri aanze kuchanganyikiwa na kuhamaki. Mfuatano wa matukio baada ya kupulizwa kwa parapanda kutaikuza hofu kwa kiwango kikubwa kisichomithilika.

KUHARIBIWA KWA ULIMWENGU

Kufuatia sauti ya parapanda na khofu kubwa iliyotawala, matokeo mazito yatatokea. Kwa wakati huu, itawathubutikia watu kwamba, wanakabiliana na janga kubwa. Ni dhahiri kuwa ulimwengu na maisha haya vinakaribia kwisha kabisa. Ndio sababu kila kitu kilicho juu ya ardhi wakati huo kitapoteza thamani kwa muda mfupi tu. Hata sauti ya siku ya kufufuliwa yenyewe inatosha kuvunja uhusiano wa kidunia miongoni mwa watu. Hakuna fikra inayoweza kumzonga mtu katika ubongo wake kwa muda huo zaidi ya kujiepusha na kujiokoa yeye mwenyewe. Woga utakuwa umepanda mno na katika siku hiyo kila mtu atakuwa ni mwenye kufikiria mambo yake tu.

“Basi itakapokuja sauti kali iumizayo masikio, siku ambayo mtu atamkimbia nduguye, Na mamaye na babaye, Na mkewe na wanawae, Kila mtu miongoni mwao siku hiyo atakuwa na hali itakayomtosha mwenyewe. (Abasa: 33-37).

Baada ya mtikisiko mkubwa, ardhi itatoa mizigo yake na itadhihirisha siri zake, hakuna kitakachokuwa na thamani siku hiyo na siku zinazofuatia.

“Wakati ardhi itakapotikiswa mtikisiko wake. Na ardhi ikatoa mizigo yake. Na akauliza Mwanadamu. ‘Hii ina maana gani? Siku hiyo ardhi itaeleza habari zake kwa sababu Mola wako ameipa Wahy. (Az-zilzalah: 1 - 5).

Sauti ya kutisha itakayofuatiwa na majuto mazito, pia kutakuwa na mlipuko wa ndani kwa ndani ambao utaharibu kila ambacho Mwanadamu alikuwa akikiona ni chenye thamani kubwa. Kwa mfano, watu huthamini nyumba zao, ofisi zao, magari yao, na maeneo yao ya mashamba na mabustani. Baadhi ya watu huchukulia kuwa nyumba ndio lengo lao kuu la maisha. Hata hivyo, thamani ya nyumba yake huyeyuka mara moja katika siku ya kufufuliwa. Utajiri wa vitu, ambao watu huashiria ndio malengo yao ya maisha, utatoweka ndani ya sekunde chache. Malengo ya yule aliyefanya juhudi ili apandishwe cheo katika kampuni kama hitajio lake kuu la maisha itakuwa wakati huo imekosa thamani. Ama mwingine aliyetumia muda wote katika maisha akipigania madaraka katika nchi yake atakakumbana na hali hiyo hiyo ya kushitua. Kwa uchungu atashuhudia nchi yake ikipotea...

Kila kitu kitapoteza thamani yake ... isipokuwa yale yaliyofanywa ili kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Haya yamebainishwa katika Qur’an,

‘Basi itakapofika hiyo balaa kubwa (ya kiama), Siku ambayo mtu atakumbuka kila alilolifanya. Na moto mkali utaoneshwa kwa kila aonaye. (An-Naziat: 34 - 36).

KUSAGIKA SAGIKA KWA MILIMA

Maangamizi yatakayotokea siku ya kufufuliwa yamepituka katika fikra za yoyote. Milima, inayoaminika kuwa madhubuti na isiyoyumba katika ardhi, itaendeshwa. Itanyanyuliwa kutoka kwenye mizizi yao na kisha kusaga sagwa. Hata mtetemesho kidogo wa ardhi hueneza hofu katika nyoyo za watu na kuathiri nyoyo zao kuona kuwa hakuna usalama. Huwafanya wayaache majumba yao na kutumia usiku wote katika mitaa wakiwa wanaranda randa kwa khofu. Kwa hivyo ndivyo, aina ya maangamizi yatakayopelekea milima kupeperushwa inathibitisha kuwa tukio hili si la kuvumilika hata kidogo. Ndani ya Qur'an, milima siku hiyo imeelezwa hali yake kama ifuatayo:-

‘Na litakapopulizwa baragumu pulizo mmoja tu. Na ardhi na milima ikaondolewa na ikavunjwa mvunjo mmoja. Siku hiyo hilo tukio litakuwa limekwisha tokea. (Al-Haqqah: 13 - 15).

Kwa hakika siku ya hukumu imewekewa wakati maalum. Siku itakapopigwa parapanda nanyi mtafika makundi makundi. Na mbingu zitafunguliwa ziwe milango milango. Na milima itaondolewa itakuwa kama mangati (mlenga) kama maji akiona kwa mbali. (Nabai: 17 - 20).

‘Na milima itakapoendeshwa (angani kama vumbi). Na ngamia wenye mimba pevu watakapoachwa, Na wanyama mwitu watakapokusanywa. (At-kakwyr: 3 - 5).

‘Siku ambayo watu watakuwa kama madumadu (watoto wa nzige) waliotawanywa. Na milima itakuwa kama sufi zilizochambuliwa (ziikawa zinapeperuka). (Al-Qaariah: 4 - 5).

Siku hiyo kutakuwa na matukio ambayo nguvu kuu isiyozuilika, kubwa kiasi cha kufanya milima, majabali, ardhi vipeperushwe kama sufi. Watu watajua hakika kuwa tukio hili ni la kipekee lisilo na mfano. Watashuhudia kuwa asili kuu ambayo hapo zamani walikuwa wakiibabu kama masanamu na vile ambayo walidhania kuwa vinao uwezo, kuu siku hiyo haviwezi kujikinga visiwe ni vyenye kukaribiwa kabisa. Wakati huo ni wakati ambao hisia za kujazwa na uhalisia wa yule mmiliki wa ulimwengu utakuwa umewadia. Pamoja na uthibitisho huo, hakuna lolote litakalowafanya makafiri waone kuwa ni lenye kuwanufaisha. Na ukweli ni kuwa kujua kwao siku hiyo hakutawasaidia chochote. Wakati huo watakuwa wamezingirwa na nguvu hii kubwa ambayo awali walipokuwa katika maisha ya dunia walikuwa wakiikwepa kuifikiria. Watajua hakika ya mambo ambayo walishindwa katika uhai wao wote kuipokea kama njia ya busara na hekima. Tishio lililoumbwa na Nguvu isiyo na mipaka kamwe haliwezi kuelezeka ila kwa yule atakayelishuhudia mwenyewe. Hali hiyo inaenea kila kiumbe, chenye uhai na kisicho na uhai. Hufanya basi kila kitu kuwa katika mwelekeo wa kudhibitiwa. Wanadamu, wanyama na maumbile asili vyote vitasagwasagwa katika huo mtetemesho. Milima haitakuwa tena vigingi, bahari haiwi tena isiyo na mipaka na mbingu haziwi tena mbali kama ilivyokuwa awali. Jua, nyota na ulimwengu wote vimezunguukwa na khofu ya siku ya kufufuliwa vyote vinarejea kwa Muumba wao. Kama ilivyo kwa milima kuwa itakunjakunjwa kama changarawe

jangwani, mwanadamu naye bila kujitambua atakunjwa kufuatia milima, nyota na bahati vyote vikipitia hatua ya kuharibiwa kabisa kabisa.

KULIPULIWA KWA BAHARI

Kwa vipawa alivyonayo Mwanadamu leo hii, ni vigumu kwa fikra zake kuweza kupokea na kuelewa vitisho vya siku hiyo ya kufufuliwa.

‘Na bahari zitakapowashwa moto. Na roho zitakapounganishwa (na viwiliwili vyake). (Tawyr: 6 - 7).

(Na bahari zitakapopasuliwa. *Infiar: 3*). Kuharibiwa huko kutakuwa katika Qadar ya Mwenyezi Mungu na Uwezo wake. Hali hii hutoa picha ya ukubwa wa jambo lenyewe.

KUHARIBIWA KWA MBINGU

Katika siku ya hukumu, sio dunia tu itakayoharibiwa, bali anga na Ulimwengu mzima utaharibiwa. Mkakati wa kwisha kwa ulimwengu utagusa anga, mwezi jua, sayari na pia dunia na kila kilichomo ndani yake, milima na bahari. Qur’an inabainisha kwamba siku hiyo:

‘Hakika haya mnayoahidiwa, bila shaka yatatokea. Wakati nyota zitakapofutwa (nuru yake). Na mbingu zitakapopasuliwa. Na milima itakaposagwa sagwa. (Al-Mursalat: 7 - 10).

Siku hiyo, viumbe vyote vilivyonasibishwa na umilele vitaanguka na kuharibiwa na kuwa si cho chote si lolote. Huu ni ukweli pia kuhusu mbingu. Tangu mwanadamu adhihiri ulimwenguni, huona mbingu kama paa linalomlinda. Hata hivyo siku ya kufufuliwa, paa hili litaanguka na kupasuka vipande vipande. Hewa na anga ambavyo vinamzunguka mwanadamu na kumpa pumzi ya kupumuwa vitakuwa kama chuma kilicho yeyushwa. Qur’an inaeleza hivyo:

‘Siku mbingu zitakapokuwa kama shaba iliyoyeyuka. (Al-Maany: 8).

Na pia vitapasuka kwa kishindo kikubwa. Hewa itajaza mapafu ya mwanadamu si kwa ajili ya kuhuishwa bali kwa ajili ya kuunguzwa.

Ulinganisho unaoweza kuletwa kati ya woga wa majanga yanayotokea katika dunia hii na vitisho vya matukio ya siku ya kufufuliwa unaweza kutoa mwanga halisi wa siku hiyo itakavyokuwa. Matetemeko ya ardhi na milipuko ya volkano ni miongoni mwa majanga ambayo yanamuogopesha mwanadamu zaidi. Miamba ya ardhi inapasuka kwa tetemeko la ardhi au milipuko ya volkano

hupelekea hali ngumu ya maisha ya kila siku kwa muda mfupi tu! Hali hii humfanya mwanadamu atanabahi kuhusu ardhi anayokanyaga juu yake kwa majivuno kwamba si chochote si lolote.

Pamoja na yote hayo yanayomuumiza Mwanadamu hutokana na matetemeko ya ardhi na milipuko ya volkano hutokea mara chache mno na hudumu kwa kipindi kifupi tu. Vidonda huona, na maumivu husahaulika baada ya muda fulani. Lakini siku ya kufufuliwa, sio kama tetemeko la ardhi au milipuko ya volkano au majanga mengine. Uzito na mfuatano wa matukio haya ya kuangamiza kila kitu hutoa taswira kwamba kila kitu kimefikia hatua ya kutorudi nyuma tena. Kwa mfano, tukio ambalo hakuna anayelifikiria hali yake halisi kwamba ‘Mbingu zitapasuka na kuanguka vipande vipande’. Hii ni kuonesha kwamba ‘kanuni za maumbile’ zinazojulikana zitakuwa zimefikia ukomo wake. Mbingu na ardhi nazo kwa mamailioni ya miaka kadhaa iliyopita vimeonekana vitu madhubuti, lakini siku hiyo vitapondwa pondwa na yule aliyeutengeneza mara ya kwanza.

‘Mbingu zitakapasuka. Na nyota zitakapopukutika. Na bahari zitakapasuliwa. (Inftar: 1 - 3).

Inaelezea siku ya kufufuliwa hali itakavyokuwa, kwamba mbingu zitapasuka na kutengana, nyota zitapukutishwa, na bahari zitajaa na kufurika. Pia katika aya nyingine:

‘Mbingu zitakapasuka. Na zitakapokinga sikio kwa Mola wake (kusikiliza amri) na zimepasiwa (na kusikiliza). (In-Shiqaq: 2 - 2).

Kila mwanadamu anachokiona kina thamani siku hiyo kitakuwa kimefikia ukomo. Kila kilichoko mbinguni kitakufa kimoja baada ya kingine.

‘Jua litakapokunjwa kunjwa. Na nyota zitakapopukutishwa. (At-Takwyr: 1 -2).

Jua ambalo ni chanzo cha mwanga kwa mamilioni ya miaka litakunjuwa kunjwa, likifanya lifanyalo chini ya kimaya yake. Hadi wakati huo wa tukio, miongoni mwa wanadamu waliojenga dhana kuwa nyota ni vitu ambavyo viko mbali sana na kwamba haviwezi kufikiwa kwa umbali na kustaajibisha, lakini katika siku hiyo, nyota zitapukutishwa kama mchezo wa mwanasesere. Milima isiyotetereka kama vigingi itasogezwa, bahari isiyo na mipaka nayo itaanza kuchemshwa. Kwa matukio yote haya, yule ambaye ni mmiliki halisi, mwenye nguvu aliyejuu ya kila kitu, ataeleweka vyema kwa kila mmoja. Uwezo wa Mwenyezi Mungu ni mpango wake vitatimia na hivyo mwanadamu kwa uchungu kabisa atatanabahishwa kuwa kule kukosa kwake muelekeo siku hiyo hakuna wa kumnusuru na kumsaidia. Sababu kubwa ya kukosa kwake muelekeo ni kule kushindwa kwake kupambanukiwa na nguvu za Mwenyezi Mungu wakati bado kifo kilikuwa hakijamkuta, Siku hiyo alama ya mmiliki halisi wa Ulimwengu na maisha atadhihiri na kujulikana.

‘Na hawakumheshimu Mwenyezi Mungu heshima ipasayo. Na siku ya kiama ardhi yote itakuwa mkononi mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume. Ameepukana na upungufu na yu juu kabisa kuliko yale wanayo mshirikishia. (Az-Zumari: 67).

HALI YA WATU ITAKAVYOKUWA

Hofu yote hii na kuchanganyikiwa katika siku ya malipo itatokana na makafiri kukosa muelekeo. Jinsi mwanadamu anavyozidi kuchupa mipaka kwa kughafilika, ndivyo atakavyozidi kujawa na wasiwasi na woga. Hali ya woga na maangamizi ambayo huanzia kwenye kifo haitakwisha milele. Kila tukio litakuwa chanzo cha woga. Kila tukio lililofichika linalomkabili pia huchochea kumuogopesha usoni. Woga huu unakuwa mzito kiasi kwamba inabadilisha rangi ya nywele za mtoto kuwa kahawia.

‘Basi ninyi mkikufuru, mtawezaje kujihifadhi na (balaa ya) ambayo itawafanya watoto kuwa wenye mvi (wazee)? Mbingu zitapasuka siku hiyo; ahadi yake (Mwenyezi Mungu) itatekekezwa tu (Al-Muzzammil: 12 - 13).

Hao wanaodhani kuwa Mwenyezi Mungu hana habari na yale wanayofanya watagundua wakati huo kuwa Mwenyezi Mungu anaakhirisha hukumu hadi siku ya kufufuliwa viumbe. Hili linafafanuliwa kama ifuatayo:-

‘Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na wanayoyafanya madhalimu. Hakika yeye anawaakhriisha tu mpaka siku ambayo macho yatakodoka (Ibrahim: 42).

Katika aya nyingine, hofu inayohisiwa na makafiri inafafanuliwa kama ifuatavyo:

‘(Msiba) ugongao nyoyo! (Msiba) ugongao nyoyo ni upi huo? Ni jambo gani litakalo kujulisha ni upi huo (msiba) ugongao nyoyo? Siku ambayo watu watakuwa kama madumadu. (watoto wa nzige) waliotawanywa. Na milima itakuwa kama sufi zilizochambuliwa (zikawa zinapeperuha): (Al-qaariah: 1-5).

Uhusiano mzito wa dunia hii ni mapenzi na hisia za mama kumlinda mwanawe. Uzito wa siku ya kufufuliwa, utavunja hata uhusiano huu mzito vilevile. Mitikisiko itasababisha kila kitu kiwe katika himaya. Mtikisiko huo utasababisha Mwanadamu kutaharuki na kupoteza fahamu. Wakati wamechaganyikiwa na kushtuka, watakimbia huku na kule kama walevi. Kinachowafanya wapoteze fahamu ni kutokana na uzito wa adhabu za Mwenyezi Mungu.

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu, hakika mtetemeko wa kياما ni jambo kubwa. Siku mtakapokiona (hicho kياما) - kila mwanamke anyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataizaa mimba yake (kabla ya wakati kufika). Na utawaona watu wamelewa; kumbe hawakulewa, lakini ni adhabu ya Mwenyezi Mungu (tu hiyo) iliyo kali: (Al-Hajj: 1 - 2).

Mbali na kuogopesha na kuhamaki, hisia nyingine iliyokuwa ngumu mno kwa watu itakuwa ile ya mwanadamu kukata tamaa. Mwanadamu huchukuwa hadhari za makusudi ili kujilinda dhidi ya majanga yenye kuweza kutokea, na dhidi ya njaa, matetemeko ya ardhi, mafuriko, vimbunga au hata vita vya kutisha kama nuklia. Mwanadamu hutafuta njia ya kujilinda na kujenga majumba. Hata hivyo, katika siku hiyo, hakuna kitakachosalia ambacho mwanadamu ataona kuwa ni salama kwake endapo anaweza kutafuta hifadhi. Hatapata msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Pia, hakuna yeyote au mamlaka ambayo itatoa msaada. Awali, mwanadamu akitafuta msaada na mwongozo kupitia sayansi na teknolojia. Lakini kwa wakati huo, kanuni zote za sayansi zimevunjika. Hata kama teknolojia imeendelea kiasi kwamba imemuwezesha mmoja kwenda mbali upenuni katika ulimwengu huu, bado ghadhabu za Mwenyewe Mwenyezi Mungu zitamfuata huko huko. Hiyo ni kwa sababu siku ya kufufuliwa imeenea ulimwengu mzima. Si dunia tu aliyoishi kwa salama bali vile vile nyota zilizoko mbali kabisa zitarejea kufuatana, na apendavyo Mwenyezi Mungu; Likiwemo jua.’ (Takwir: 1 - 2).

Kukata tamaa kutakakomsibu mwanadamu, kunaelezwa vizuri katika aya zifuatazo:-

‘Na Mwezi utakapatwa, Na jua na Mwezi vitakapokutanishwa. Siku hiyo Mwanadamu atasema, “Nitakimbilia wapi? Hapana! Hakuna mahali pa kukimbilia. Siku hiyo ni kwa Mola wako (tu). (Al-Qiyaam: 8-12).

PARAPANDA LA PILI NA KUFUFULIWA VIUMBE

Wakati baragumu (parapanda) litakapopulizwa kwa mara ya kwanza, mbingu na ardhi vitavunjwa vinjwa na ulimwengu wote utafika kikomo. Hakuna nafsi itakayoachwa hai. Kwa maneno ya Qur’an:

(Ikimbukeni) siku ambayo ardhi hii itabadilishwa kuwa ardhi nyingine, na mbingu; nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu, Mmoja, Mwenye nguvu. (Ibrahim: 48).

Haya mazingira mapya yameandaliwa kwa ajili ya hukumu ya Mwisho. Ufafanuzi wake ni:

‘Na wanakuuliza habari za milima. Waambie: “Mola wangu ataivunja vunja. Na ataiacha (ardhi yote kama) uwanda uliokaa sawa. Hataona humo mdidimo wala kuinuka. (Taha: 105 - 107).

Huu ndio wakati ambao watu watafufuliwa, na kukusanywa na kusubiri hesabu ya matendo yao. Pia, hapo ndipo watakapojifunza kuwa wanaelekea wapi. Wakati umewadia kwa watu kufufuliwa na

kuhudhurishwa kwa Mola wao, Al-Wahid, mwenye nguvu. Na ndipo baragumu litapulizwa kwa mara ya pili. Wale watu waliokanusa akhera na kufiliwa katika dunia hii, watafufuliwa kutoka makaburini mwao.

Hili ni jambo ambalo hawakuwa wanafikiriwa kuwa litatokea kweli. Qur'an imebainisha juu ya matukio haya kuwa:

‘Na litapigwa baragumu watoke roho watu waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule amtakaye Mwenyezi Mungu. Tena litapigwa mara nyingine. Hapo watafufuka; wawe wanatazama. Na ardhi itang’ara kwa nuru ya Mola wake: (Az-Zumar: 68 - 69).

KUTOKEA KWA WAFU KUTOKA MAKABURINI MWAO

Mwenyezi Mungu anaelezea kwa undani juu ya hali halisi wakati wafu watakapofufuka makaburini na kila sehemu walizofia. Kama ilivyotanabahishwa ndani ya Qur'an, tukio hili kubwa litatokea, hivyo, hadi wakati tarumbeta litakapopulizwa kwa mara ya pili watu wataitwa tokja walikozikwa au walikofishwa ambako ndiko makaburi yao:

‘Macho yao yatainama chini; wanatoka katika makaburi kama kwamba ni nzige waliotawanyika. (Al-Qamar: 7). ‘Na katika ishara zake ni kuwa mbingu na radhi vimesimama; kwa amri yake. Kisha atakapokuiteni wito mmoja tu, mtatoka ardhini. (Ar-rum: 25).

‘Siku itakapo wapasukia ardhi, (watoke) humo upesi upesi, huo ni mkusanyiko rahisi kwetu (Qaf:44).

Kama vile wanashambulia golini, watamfuata muitaji ambaye atawaita huku shingo zao zikielekezwa kwake. Wito huu utakuwa si wenye kufafana na wa aina yoyote uliyopata kusikika.

“Siku watakapotoka makaburini kwa wepesi kama kwamba wanakimbilia mfunda (mede), (mfundo wao wanaposhindana) (Ma’arij: 43).

‘Basi jiepushe nao. Na (wakumbushe) Siku atakapoita muitaji huyo kuliendea jambo zito (hilo la kiama) (Al-Qamar: 6).

‘Siku hiyo watamfuata muitaji asiye na upotofu. Na zitanyenyekea Sauti kwa Mwingi wa Rehema na hutasikia mchakato ila wa miguu (Tahr: 108).

Wale ambao wamechupa mipaka ambayo ameiweka Mwenyezi Mungu, ambao hawakumtii Mwenyezi Mungu, wakikazania taratibu zao wenyewe za maisha, waliomkanusha Mwenyezi Mungu,

na wakaendelea kuwa jeuri, watakuwa ghafla watiifu na kunyenyekea kwake punde watakapotolewa makaburini mwao. Bila kuuliza swali wataitikia wito huu. Kwa sababu majaribio au mitihani katika dunia hii imekwisha, hawatakuwa na chaguo lingine zaidi ya kuthibitisha lile walilolitenda. Hata kama wangependa kufanya hivyo, hawawezi tena kufanya kinyume chake. Hawawezi tena kujenga matumano kama hayo. Hawana uwezo wa kuhimili wito huo. Ndio maana, uono wao uliojengeke katika hisia kali utakuwa, hii ‘Ni siku isiyo na pa kupenya.’

Macho yao yatainama chini, wanatoka katika makaburi kama kwamba ni nzige waliotawanyika. Wanamkimbilia muitaji huyo na huku wanasema hao makafiri: ‘Hii ni siku ngumu (kabisa, haina pa kupenya) (Al-Wamar:7-8).

Hivyo makafiri watakimbia mbele. Kila mmoja atadhihirisha utiifu wake. Siku hiyo kitu pekee ambacho watu watakuwa nacho kilicho muhimu ni Imani. Hata hivyo makafiri watakosa imani. Ndio maana nyoyo zao ni tupu. Tunafahamishwa katika Qur’an:-

(Wawe) wanakwenda mbio, vichwa juu, na macho yao hayapepesi, na nyoyo zao tupu (haziko, wanahemkwa mbio, mapepe): (Ibrahim: 43).

Tanafahamishwa kuwa watakuwa wanaelekea mahali maalum katika makundi ‘Siku itakapopigwa parapanda (baragumu), nanyi mtafika makundi makundi (An-Nabaa:18).

‘Na kisha litapigwa parapanda (bagagumu) (la kufufuliwa) tahamaki hao wanatoka makaburini kwenda mbiombio kwa Mola wao’ Watasema: ‘Ole wetu! Nani aliyetufufua malaloni petu?’ (Waambiwe) ‘Haya ndio yale aliyoahidi (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema na waliyoyasema kwa haki Mitume. (Yasin: 51-52).

Maneno ‘Ah majuto yetu’ au ‘Ole wetu!’ ni kuonesha kuchanganyikiwa kukubwa na kukata tamaa. Kafiri ambaye atashuhudia kufufuliwa kwake atatambua kuwa Mitume ya Mwenyezi Mungu ambao walifikisha ujumbe huu katika kipindi chote cha uhai wake walisema kweli. Atagundua kwamba ataingizwa katika adhabu ya milele ambayo mitume waliwahofisha makafiri juu yake. Muda huo, atafunika aina zote za mashaka na kubakisha ukweli uchukuwe mkondo wake ya kuwa hakuna kitu kinachoitwa ‘Usingizi wa Milele’. Kukatishwa kwake tamaa kutazidishwa kwa matumaini ya kuokolewa kuyoyoma kutokana na adhabu iliyo mbele yake. Makafiri watajawa na hofu, woga na kukata tamaa. Hali yao kwa ujumla ni ya kuchanganyikiwa. Mwenyezi Mungu katika Qur’an anasema:

‘Nyuso nyingine zitakuwa na mavumbi yaike. Giza totoro litazifunika. Hao ndio makafiri watenda mabaya (Abasa: 40 - 42).

‘Na siku ya kiama utawaona wale waliomsingizia uongo Mwenyezi Mungu nyuso zao zitakuwa nyeusi. Je, si katika Jahannam makazi ya wale wanaotakabari? (Az-Zimar” 60).

Mwenyezi Mungu atawafufua makafiri katika siku hiyo hali yakuwa ni vipofu? Anasema:

‘Na atakayejiapushe na mawaidha yangu (hayo), basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na siku ya kiama tutamfufua hali ya kuwa ni kipofu. Aseme, ‘Ee Mola wangu! Mbona umenifufua kipofu, na hali nilikuwa nikiona?’” (Mwenyezi Mungu) Atasema: ‘Ndio vivyo hivyo, zilikuja aya zetu ukazisahau, (ukazipuuzwa), na kadhalika leo utasahauliwa (utapuuzwa). (Taha: 124 - 126).

Na ambaye Mwenyezi Mungu amemuongoa, basi yeye ndiye aliyeongoka; na anaewachia kupotea, basi wewe hutawapatia walinzi wasiokuwa yeye (Mwenyezi Mungu). Na tutawakusanya siku ya kiama, hali yakuwa wanakotwa juu ya nyuso zao na hali yakuwa vipofu na mabubu na viziwi. Makazi yao ni Jahannam. (Na) kila ukifanya kusinzia kidogo tutauzidishia mwako. (Bani Israil: 97).

Pia sehemu nyeupe ya jicho itafanywa kuwa buluu. Rangi hii ya macho itazidisha kuchanganyikiwa na sura ya kutisha kwa makafiri. Mwenyezi Mungu anabainisha kuwa:

Siku itakapopigwa Baragumu na tukawakusanya wakosa siku hiyo, hali macho yao yatakuwa kibuluu (kwa khofu) (Bani Israil: 102).

Kwa hali hii ya kuchukiza na ya kuvunja hadhi ya makafiri, itawatofautisha na waumini tangu awali. Huu ndio mwanzo wa Mwisho wa kundi la watu waliokuwa wanapinga aya za Mwenyezi Mungu na wakabakia kuwa jeuri.

HAKUTAKUWA NA URAFIKI, UDUGU NA USHIRIKIANO

Siku hiyo Mwanadamu atakuwa ametengwa mno kiasi cha kutojali wengine. Atamuacha hata mama yake, baba yake, mke na watoto pia. Kubwa litakalo mshughulisha kutokana na uzito na tishio ambalo halielezeki katika siku hiyo ya kufufuliwa ni kuhusu yale mambo yake aliyoyatanguliza Mwenyezi Mungu anaelezea siku ya kufufuliwa kama ifuatavyo:-

‘Na ni nini kitakachokujulisha siku ya malipo ni siku gani hiyo! Tena ni nini kitakachokujulisha siku ya malipo ni siku gani hiyo! Ni siku ambayo nafsi haitamiliki nafsi (nyingine) chochote; na amri siku hiyo itakuwa ya Mwenyezi Mungu tu. (Al-Infitar: 17-19).

‘Basi itakapokuja Sauti kali iumizayo masikio (Sauti ya baragumu la Kiama); siku ambayo, mtu atamkimbia nduguye, na mamaye na babaye, na mkewe na wanawe. Na kila mtu miongoni mwao, siku hiyo atakuwa na hali itakayo mtosha mwenyewe. (Abasa: 33-37).

Na uhusiano wa kijamii utakosa thamani siku hiyo na utaakuwa na mwisho wa uchungu. Mtikisiko wa siku hiyo utasababisha uhusiano wa kindugu usiwe na maana. Kitu pekee chenye thamani kitakachobaki ni Imani.

‘Basi litakapopulizwa Parapanda, hapo hautakuwepo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana. Ama wale ambao mizani ya amali zao (nzuri) itakuwa nzito, hao ndio waliozitia hasarani nafsi zao, na katika Jahannam watakaa muda milele (Al-Muuminuun: 101 -103).

Uhusio wa kifamilia utavunjika kiasi ambacho watu watakuwa radhi kuwatoa wawapendao katika watoto wake, ndugu na hata ndugu zao wote ili wao wapate kujiokoa. Hakuna rafiki mzuri atakayeuliza juu ya rafiki yake, japo wanaweza kuonana. Muovu atatamani ajitakase na adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa watoto wake au mke wake, au ndugu yake au familia yake iliyomhifadhi au yeyote katika dunia, kama hicho ndicho kitakachofaa kumuokoa.

‘Wala Jamaa hatumuuliza jamaa (yake). (Ingawa) watafanywa waonane. Mwenye kosa atatamani ajikomboa katika adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa watoto wake. Na mkewe na nduguze,. Na jamaa zake waliomzunguka kwa kila upande, Na kuvitoa vyote vilivyomo katika ardhi, kisha aoko. Lakini wapi! Kwa hakika huo ni moto uwakao barabara. (Al-Ma’anj: 10-15).

‘Ofa’ hii kwa kweli ni alama juu ya kukosa shukurani na mawazo finyu ya makafiri wakati manufaa ya yanapotetereka. Ofa hii pia inatoa funzo juu ya yale yanayopiganiwa katika dunia hii. Mara nyingi Mwanadamu hushindana kutafuta yale malengo yanayoonekana; na kwa ajili ya fedha atafanya kazi maisha yote. Hata hivyo kama Qur’an inayotufahamisha, katika juhudi zake ambazo tayari zimemkatisha tamaa za kutaka kujikomboa, mtu atakuwa radhi kulipa, sio mwanamke mmoja tu, bali wanawake wote ulimwenguni au vitu vyote alivyonavyo ili tu aweze kuokoka. Hizi zote ni juhudi zisizo na matunda. Mwenyezi Mungu ndiye ambaye mkononi mwake imo miliki ya kila kilichopo ulimwenguni. Ukombozi kwa Upande mwingine, hubaki nyuma, katika maisha ya kidunia. Kwa wakati huo, mtu atakuwa amekwishachelewa. Kama ilivyokwishaahidiwa, moto umekwisha kokwa tayari ukisubiri.

KUKUSANYWA KWA WATU ILI WOTE HESABU YA MATENDO YAO

Qur’an inaelezea maana halisi ya Maisha:

‘Ewe Mtu! Hakika wewe unajikusuru kusuru (katika kufanya mambo yako) mpaka (siku utakayokutana na) Mola wako; basi (amali zako hizo) utazikata (Al-Inshiqaq:6)

Bila kutazama lipi analofanya katika maisha yake aya, mwishowe atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu. Lengo kuu la maisha haya ni kuwa mtumwa wake. Muda muhimu, kwa upande Mwingine, ni siku ya kufufuliwa, wakati mwanadamu atakapotoa hesabu juu ya vitendo vyake katika maisha yake ya dunia hii. Kila siku inavyopita ndivyo mtu anavyoisogelea siku hii na wakati huu. Kila siku inayopita ndiyo mtu anavyoisogelea siku hii na wakati huu. Kila siku inavyopita ndivyo mtu anavyoisogelea siku hii na wakati huu. Kila saa ipitayo, dakika au hata sekunde ni hatua kuelekea kifo, kufufuliwa na muda wa kuhesabiwa. Maisha kama mshale wa saa, hutembea bila kusimama kuelekea huko. Hakuna njia ya kuusimamisha muda, au kuurejesha nyuma. Watu wote hufuata mkondo huu:-

‘Hakika marejeo yao ni kwetu. Kisha, bila shaka, hisabu yao ni kwetu. (Al-ghashujah: 25 – 26).

Kuna takriban watu bilioni sita katika ardhi leo hii. Ukiongeza idadi ya wale walioishi kabla itakupa picha juu ya msongamano wa watu watakaokusanyika siku hiyo ya kufufuliwa. Watu wote, tangu wakati wa Nabii Adamu (juu yake amani), mtu wa kwanza hapa duniani hadi mtu wa mwisho asiyeamini ambaye ameishi katika dunia hii watakuwepo siku hiyo bila kusahauliwa hata mmoja. Kundi hili la watu litaonesha picha ya kustajabisha. Hata hivyo, wakati hayo yakijiri, kwa hakika itakuwa hali ya kutisha kweli kweli. Hali ya watu wote mbele ya Mwenyezi Mungu imeelezwa katika Qur’an kama ifuatavyo:-

‘Siku hiyo watamfuata mwitaji asiye na upotofu. Na zitanyenyekea sauti kwa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema na hutasikia ila mchakato tu wa miguu. Siku hiyo hautafaa uombezi (wa yeyote) ila wa yule aliyemruhusu Mwingi wa Rehema na kuiridhia kauli (yake). (Mwenyezi Mungu) anajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala wao hawawezi kumjua (Mwenyezi Mungu) vilivyo. Na nyuso nyingine zitadhalilika (siku hiyo) mbele ya Mwenyezi Mungu aliye wa milele daima, anayepitisha mambo yote. Na watakuwa wenye kuharibikiwa kila mwenye kufanya dhuluma. (Taha: 108 = 111).

Muda wa kutoa hesabu, ambao makafiri walikanusha muda wote wa uhai wao, ambapo waumini walijitahidi kujiandaa kwao, umewadia. Mahali patukufu pameandaliwa kwa ajili ya mahakama hii. Kwa mujibu wa Qur’an, siku hiyo:=

‘Na mbingu zitapasuka, basi siku hiyo, zitakuwa dhaifu kabisa. Na malaika watakuwa kandoni mwake (hizo mbingu) na malaika wa namna nane watachukuwa kiti cha enzi cha Mola wako juu yao. (Al-Haqqah: 16-17).

Siku ambayo zitasimama roho (za viumbe wote) na malaika safusafu: Hatasema siku hiyo ila yule ambaye (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa Rehema amempa idhini (ya kusema) na atasema yaliyo sawa. (An-Nabaa: 38).

Mola wa mbingu na ardhi, atahitaji hesabu ya matendo ya waja wake. Chanzo cha mateso yenye kuwasiliana, utukufu na nguvu zake, vyote vitadhihirika. Moto uwakao utaendelea kuwaka huko Jahannam. Mwenyezi Mungu, aliyeumba kila kitu kwa namna ya kipekee, ameandaa adhabu iumizayo kwa makafiri. Hakuna yeyote awezaye kuadhibu mfano wa kuadhibu kwake siku hiyo, kabla na baada yake.

Katika Qur'an Mwenyezi Mungu anasema:="

'Sivyo hivyo! (Kumbukeni) itakapovunjwa ardhi vipande vipande. Na kufika (amri ya) Mola wako, na malaika safu safu. Basi siku hiyo italetwa Jahannam. Siku hiyo mwanadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini? Atasema: "Laiti ningalitanguliza (wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo)." Basi siku hiyo hataadhibu yeyote namna ya kuadhibu kwake (Mwenyezi Mungu). Wala hatafunga yeyote jinsi ya kufunga kwake (Mwenyezi Mungu). (Al-Fajr: 21-26).

Kama mwanadamu atashindwa kumtumikia Mola wake katika dunia hii na kujiandaa kwa siku iliyokuu, basi ataambulia majuto. Atatamani arejeshwe kuwa udongo kuliko kufufuliwa. Hata hivyo, kujuta kwake huko hakutamsaidia lolote. Kinyume chake, itakuwa ndio chanzo cha huzuni na kuongeza sehemu ya adhabu iliyoandaliwa huko motoni.

"...Siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake miwili, na kafiri atasema: Laiti ningalikuwa udongo(An-Nabaa 40)

KUDHIHIRISHWA KWA VITABU NA MIZANI YA HAKI

Kabla ya kupata fursa ya kushinda mitikisiko iliyosababishwa na kufufuliwa, wanadamu watakuwa wamepigwa na hofu kubwa na kutetemeka mno. Hii ni kwa sababu watatoa hesabu ya matendo yao mbele ya Mwenyezi Mungu. Matendo yao yote waliyoyafanya wakati wa uhai wao na pia fikra zao zote zitadhihirishwa. Hakuna hata jambo linaloonekana dogo litakalosahauliwa. Aya ifuatayo inafafanua hilo kwa uwazi:="

Ewe Mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Mwenyezi Mungu atalileta (amlipe aliyefanya); bila shaka Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa mambo yaliyofichikana; (wa) ni mjuzi wa mambo yaliyo dhahiri. (Luqman:16).

Hiki ni kipindi karibu kabisa na peponi au motoni. Watu wataona waliyoyatanguliza kwa ajili ya maisha yao ya milele. Hili ameelezwa katika Qur'an kama ifuatavyo:="

'Siku hiyo watu watatoka (makaburni) vikundi vikundi ili waoneshwe vitendo vyao. Basi anayefanya wema (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yae.(Az-zilzahah: 6-8).

Kama ilivyobainishwa katika Qur'an, makafiri watapewa madaftari yao kwa mkono ya kushoto, wakati waumini watapewa madaftari yao kutoka kuliani. Hali ya watu wa kuliani inafafanuliwa tena ifuatayo.

'Siku hiyo mtadhihirishwa - haitafichika siri yenu yoyote. Basi ama yule atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa mkono wake wa kuume (kulia) atasema (kwa furaha); Haya! Someni daftari langu (nililopewa sasa hivi). Hakika nilijua ya kuwa nitapokea hisabu yenye (kwa vizuri, kwani nitafanya mazuri)." Basi yeye atakuwa katika maisha ya raha katika pepo tukufu. Vishada vya matunda yake vitakuwa karibu. (Waambiwe) 'Kuleni na mnywe kwa furaha kwa sababu ya vitendo mliyofanya katika siku zilizo pita: (Al-Haqqah: 18-24).

Sauti na furaha na bashasha ya Waumini, makafiri wao watakuwa katika hali ya majonzi makubwa kabisa. Watatamani kufa au kutoweka kabisa. Hali yao ya kukata tamaa inabainishwa kama ifuatavyo:-

'Walakini atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kushoto basi yeye atasema" "Oo! Laiti nisingalipewa daftari langu." "Wala nisingalijua ni nini hisabu yangu." Laiti (mauti) yangemaliza (kila kitu changu)." "Mali yangu haikunifaa." Usultani (ukubwa) wangu umenipotea." (Al-Haqqah: 25 - 29).

'Lakini atakayepewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake, Basi yeye atayaita mauti (yamjie, ili afe apumzike, wala hayatamjia), Na ataingia Motoni. Maana alikuwa na furaha (za maasia) pamoja na watu wake. (Na) alidhani kuwa hatarejea (kwa Mwenyezi Mungu). Kwanini (asirejee)? Mola wake alikuwa akimuona; (Inshiqaq: 10 - 15).

Matendo yanayohifadhiwa katika vitabu yatapimwa kwa uadilifu. Haya yanabainishwa katika aya ifuatayo:-

‘Nasi tutaweka mizani ya uadilifu siku ya kiama, na nafsi yoyote haitadhulumiwa hata kidogo. Na hata kama ilikuwa (jambo hilo lina) uzito mdogo wa chembe ya hardali nalo tutalileta; Nasi tunatosha kuwa wajuzi (wazuri kabisa) wa hisabu. (Anbiyaa: 47)

Kila tendo lililofanyika katika maisha haya japo liwe la kiwango kidogo, litawekwa katika mizani. Alama katika mizani itaonesha ama mtu atatumbukizwa motoni kwenye adhabu ya milele au atakuwa katika furaha ya ukombozi wa milele. Kama mizani itaelemea kwenye uzito ina mema, mja atahukumiwa amefuzu na hivyo kuingizwa peponi. Kama haikuwa hiyo, basi atahukumiwa kuwa yeye ni mtu wa motoni. Hakuna yeyote, wala hakuna nguvu itakayomsaidia:-

‘Basi yule ambaye mizani yake itakuwa nzito. Huyo atakuwa katika maisha yanayompendeza. Na yule ambaye mizani yake itakuwa nyepesi, Hayo maskani yake yatakuwa katika Hawiya. Na jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) ni nini hiyo (Hawiya)? Ni moto uwakao kwa ukali (kwelikweli). (Al-Qariyah: 6-11).

Kisha, watu wote tangu kuumbwa kwa dunia watatoa hesabu ya mmoja baada ya mwingine. Hapa, nafasi na vyeo vya duniani havitakuwa na thamani. Rais wa nchi au mtu wa kawaida watakuwa sawa. Wanapata huduma inayofanana mbele ya Mwenyezi Mungu. Hapa, wataulizwa katika maswali yaliyo magumu, yasiyopendezesha, kuonesha kama amemtumikia au hakumtumikia Mola wake na kutii amri zake. Dhambi zote, vitendo viovu na fikra za ndani za makafiri, zitadhihirishwa:-

‘Siku zitakapodhihirishwa Siri. Basi hatakuwa na nguvu wala msaidizi. (Tariq: 9-10).

Utaratibu huu unaudi kwa wale ambao hawakuishi kwa kufuata sheria za Mwenyezi Mungu bali walifuata matamano ya nafsi zao au kwa kufuata sheria zilizopindishwa, imani na kanuni za jamii. Katika aya ifuatayo Mwenyezi Mungu anaeleza hali halisi itakavyokuwa siku hiyo iliyokuu:-

‘Na mtoto mwanamke aliyelikwa hali ya kuwa yuhai atakapoulizwa. Kwa makosa gani aliuawa. Na madaftari (ya amali) yatakapokunjuliwa (kila mtu akapewa lake). Na utando wa mbingu utakapotanduliwa. Na Jahannam itakapochochewa. Na peo itakaposogezwa karibu, (wakati huo), kila nafsi itajua ilichokihudhurisha. (At-Takwyr: 8-14).

Mtumwa hana fursa ya kukanusha yale aliyoyatenda mbele ya Mwenyezi Mungu. Matendo yake yote mema na mabaya yatadhihirishwa. Hata kama atakanusha, watakuwepo mashahidi watakaoeleza ukweli. Watu waliomshuhudia katika wakati wa uhai wake wataletwa mbele kutoa ushahidi:

‘Na ardhi (siku hiyo) itang’ara kwa nuru ya Mola wake, madaftari (ya vitendo) yatawekwa; na wataletwa manabii na mashahidi na wengine ambao hawakutegemewa dhidi ya makafiri. Masikio, macho, na ngozi ya mwanadamu vitapewa uwezo wa kuzungumza kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na kutoa ushahidi dhidi yao. Kuumbuliwa kwa mwanadamu na viungo vyake alivyoviona kuwa ni mali

yake hapa duniani, kunaongeza huzuni ambayo itakuwa kwa kafiri siku hiyo. Ukweli huu unaelezwa na Mwenyezi Mungu kwa maneno yafuatayo:-

Na (wakumbushe) siku watakapokusanywa maadui wa Mwenyezi Mungu katika moto, wakawa wanatengwa makundi mbalimbali. Hata watakapoujia (huo moto), hapo ndipo masikio yao, na macho yao na ngozi zao (viungo vyao vingine) zitakapotoa ushahidi juu yao kwa yale waliyokuwa wakiyatenda. Na wao waziambie (hizi) ngozi zao: “Mbona mnatushuhudia?” Nazo ziwaambie: “Mwenyezi Mungu aliyekitamkisha kila kitu ndiye aliyetutamkisha, naye ndiye aliyekuumbeni mara ya kwanza. Na kwake (hivi sasa) mnarudishwa. Na hamkuwa mkijificha hata masikio yenu na macho yenu na ngozi zenu (viungo vyao vyengine) zisiweze kutoa ushahidi juu yenu, bali mlidhani ya kwamba Mwenyezi Mungu hayajui mengi katika (hayo) mnayofanya. Basi hiyo ni dhana yenu mliyokuwa mkimdhania Mola wenu. imekuangamizeni; na mumekuwa miongoni mwa wenye kukhasirika. Basi wakistahamili, moto ndio maskani yao (ya wakitostahmili pia moto ndio maskani yao); Na kama wakitoa udhuru hawatakuwa miongoni mwa wanaokubaliwa nyudhuru zao.’ Haa mym (Sajidah: 19-24).

Makafiri watajuta mno kwa kumuasi Muumba wao aliyemuumba na kumjaalia maisha yakawezekana juu yao. Ndio maana katika siku ya kufufuliwa hawataruhusiwa kujitetea wenyewe. Hakuna fursa itakayotolewa kwao kunyanyua sauti zao. Wakiwa taabani na wenye majonzi, watataraji wapewe nafuu, lakini Mwenyezi Mungu anafafanua hali itakavyokuwa:

Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha! Hii ni siku ambayo hawatasema (kitu). Wala hawatapewa ruhusa (kutoa udhuru) wakapata kutoa. Ole wao siku hiyo hao wanaokadhibisha! (Waambiwe) “Hii ni siku ya hukumu, tumekukusanyeni ninyi na wale waliotangulia. Hivyo kama kuna ubishi wowote, ufanyeni sasa hivi mbele yangu’ (Mursalat: 34 - 40).

Kwa hakika wale waliokufuru watanadiwa (wataambiwa) ‘Bila shaka kukuchukieni Mwenyezi Mungu ni kukubwa kuliko kujichukia ninyi nafsi zenu. (Kumbukeni) mlipokuwa mnaitwa katika Uislamu na ninyi mkakufuru: (Al-Muumin: 10).

KUKATA TAMAA KWA MAKAFIRI

Siku hiyo kafiri atataka kuridhia amri zote, bado, hataweza kufanya hivyo. Hii ni kwa sababu, hana tena uwezo wa kufanya au kukanusha chochote. Wakati atakapoitwa arukuu, atataka kufanya hivyo. Hata hivyo hatafanikiwa kuweza kufanya hivyo. Kama vile mtu aliyeota njozi mbaya, atataka aiondoshe lakini hawezi. Kamwe hawezi kusogeza mguu au mkono. Hofu, uoga na kukata tamaa vitamuacha kiasi cha kuonekana amepata ganzi.

(Na nawalete) hiyo siku kutakayokuwa na mateso makali, na wataitwa kusujudu lakini hawataweza. Macho yao yatainama chini, unyonge utawafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa kusajudu walipokuwa salama (na walikataa). (Al-Qalam: 42-43).

Kumuita asiyeamini asujudu inatimiza lengo: Yaani kuzidisha majuto na majonzi anayohisi kutokana na kutokubaliana na wito huo alipokuwa duniani; na kumkumbusha kuwa kutotii huko, leo hakuwezi kufidiwa na hivyo kuwa chanzo cha majuto na kukosa matumaini milele. Inajulikana wazi kwa Mwenyezi Mungu kuwa kafiri hawezi kusujudu tena. Ni kwake tu, kama Mwenyezi Mungu alipenda, kuwa hawawezi kusujudu, kuabudu na kuwa watumwa wake. Hali kadhalika, waumini wametunukiwa imani. Hii ni kutokana na kupenda na kutaka kwake Mwenyezi Mungu. Qur'an pia inatuelezea juu ya namna waumini na makafiri watakvyoonekana siku hiyo. Furaha ya ndani kabisa watakvoyokuwa nayo waumini itaonekana katika nyuso zao zitakazong'ara kweli kweli. Makafiri kwa upande wao; watagundua juu ya kukosa kwao shukurani na kukosa kwao busara katika vitendo vyao. Wataanza kusubiri adhabu iliyoandaliwa kwa ajili yao. Kinyume na furaha inayoonekana katika nyuzo za waumini, makafiri nyuso zao zitakuwa nyeusi na zilizokunjamana”-

‘Sivyo! Bali ninyi mnapenda maisha ya hapa duniani. Na mnaacha (kuyashughulikia) maisha ya Akhera. Nyuso (nyingine siku hiyo zitang'ara (kweli kweli). Zinamtazama Mola wao (au neema alizowapa). Na nyuso nyingine siku hiyo zitakunjana zitajua kuwa zitafikiwa na msiba uvunjao uti wa mgongo. (Qiyamah: 20 - 25).

KUONA MOTO

Inaaminiwa na wengi kwamba ni makafiri tu ndio watakaona moto. Hii, kwa hakika, ni sehemu tu ya ukweli. Mwenyezi Mungu anatufahamisha katika Surat Maryam kwamba watu wote, waumini na makafiri, watakusanywa kuuzunguuka moto wakiwa wamepiga magoti.

Na (baadhi ya) wanadamu husema, “Je! Nitakapokuwa nimekufa, kweli nitafufuliwa mara ya pili kuwa hai (mara ya pili)?” Je! Mwanadamu hakumbuki ya kwamba tulimuumba (kabla yake hii), hali hakuwa chochote?

Basi naapa kwa Mola wako kwa yakini tutawakusanya wao pamoja na mashetani, kisha tutawahudhurisha pembezoni mwa Jahannam, wapige magoti (hapo). Kisha kwa yakini tutawatoa, katika kila Taifa, wale miongoni mwao waliomuasi zaidi (Mwenyezi Mungu) mwingi wa Rehema. Tena hakika sisi tunawafahamu sina wanaostahiki (Wanaostahili) zaidi kuunguza humo. Wala hakuna katika ninyi ila ni mwenye kuifikia (hiyo jahannam). Na wajibu wa Mola wako uliokwishahukumiwa. Kisha tutawaokoa wale wamchao (Mwenyezi Mungu); Tutawacha madhalimu huko wamepiga magoti. (Maryam: 66 - 72).

Kama tunavyoona katika aya hizi hapo juu, katika siku ya kufufuliwa, watu watakusanywa kuuzunguka mtoto wa jahannam, wakiwa wamepiga magoti. Makafiri na Waumini wote watasikia Sauti ya kutisha na yenye kutokota ya moto wa Jahannam kwa pamoja huku wakishuhudia picha za kutisha. Hata hivyo waumini wataokolewa baada ya kipindi fulani na makafiri wataachwa hapo wakiwa wamepiga magoti. Kisha watatumbukizwa katika moto wa Jahannam.

Ili kuelewa vizuri ghadhabu za Mwenyezi Mungu na kuwa na shukurani kwake, inaweza kuchukuliwa kuwa ni moja ya sababu ya kuwepo Waumini katika kundi lililokusanywa karibu na moto. Muumini kwa kushuhudia namna moto unavyofanana, ataelewa ni kwa kiwango gani ametunukiwa neema ya imani na Mola wake. Kwa kuwa motoni ni sehemu inayotosha, hata kule kuokolewa kutokana na adhabu hiyo huwa na maana ya rehema kwa mwanadamu.

Kwa kushuhudia moto, Muumini ataweza kulinganisha na hivyo kuelewa vyema na kuridhia Pepo, mahali penye Rehema ambapo yatakuwa makazi yake milele. Hata katika maisha haya, jambo kubwa mwanadamu analolifurahia ni kuepushwa na maumivu. Kwa mfano, mtu anayekabiliwa na hatari ya kuganda katika mabarafu mlimani hupata faraja pale anapopata kijibanda kikuu kuu chenye sehemu ya kuwashia moto. Atakichukulia kibanda hiki kama chumba cha hoteli kilichosheheni vitu vya anasa. Kwa yule ambaye anajua hajakula chochote kwa siku kadhaa, kipande cha mkate kwake ni sikukuu. Mwisho wa maumivu ni furaha isiyo na kifani, amani na kushukuru kusiko na kifani pia. Muumini anayeona moto jirani yake na kuokolewa nao hufikia daraja la juu zaidi la furaha kuliko hili. Zaidi ya hilo, kule kuzawadiwa Pepo hufikia daraja la ushindi aliloainishiwa katika Qur'an. Kwa kuona hali ya kutosha ya adhabu ya motoni, muumini ataelewa vizuri thamani ya pepo ambayo imeshenehi rehema. Kwa muda wote uliobakia milele, kama hatasahau kwamba Jahannam (motoni) kukoje na hivyo kuwa mwenye furaha zaidi huko peponi.

Katika siku ya hukumu, watu watasikia maneno yafuatayo kwa wale watakaowafahamu waumini na makafiri katika nyuso zao. Kutakuwa na ukuta unaotenganisha kati yao na katika muunuko kutakuwepo watu watakaowatambua kila mmoja, kwa anavyoonekana. Watawaita watu wa peponi 'Amani iwe kwenu! Lakini bado hawajaingia humo japo wangependa kufanya hivyo. Watakapogeuzwa nyuso zao upande mwingine wa wale watu wa motoni; watasema: Ee Mola wetu, usitutumbukize na kutufanya pamoja na watu waovu hawa.'

Watu waliopo kilimani watawaita watu waliowatambua kwa alama zao watawaita watu wa peponi 'Assalaam Alaykum' Wao wenyewe bado hawajaingia humo wanatumai. Na macho yao yanapogeuzwa kwenye watu wa motoni, husema; 'Mola wetu usituweke pamoja na watu madhalimu; Na hao watu wa sehemu iliyonyanyuka watawaita watu wanaowafahamu kwa Alama zao waseme 'Haukukusaidieni wingi wenu wala mlivyokuwa mkijivunia. "Je hawa sio wale mliokuwa mkiwaapia kwamba Mwenyezi Mungu hatawafikishia Rehema? (Sasa wameambiwa) Ingieni peponi, hakuna khofu juu yenu, wala hamtahuzunika." (Al-A'araf: 46:49).

Huu ni wakati ambapo waumini, viumbe bora kabisa ‘(Al-bayyinah: 7) na makafiri ‘Viumbe dhalili kabisa’ (Al-Bayyinah: 6) watakapotenganishwa. ‘Na mitume watakapokusanywa, Kwa siku gani hiyo wamewekwa muda huo? Siku ya hukumu. Na nini kitakachokujulisha siku ya hukumu? Ole wao siku hiyo hawa waaokadhibisha! Je, hatukuwaangamiza (watu) wa zamani (kabisa)? Kisha tukawaandamizia (watu) wengine. Basi hivi ndivyo tutakavyowafanya wakosa (wengine). Ole wao siku hiyo anaokadhibisha! (Al-Mursalat: 11-19).

Siku ya hukumu, huanza kwa kifo, kisha kuendelea kwa kufufuliwa na kuhesabiwa na kumalizika kwa watu kupelekwa kwenye makazi yao ya kudumu. Katika Surat Qaf, safari ya waumini na makafiri kuelekea kwenye makazi yao ya kudumu imefafanuliwa katika aya zifuatazo:-

‘Na kutoka roho kutakapomjia kwa haki, (Hapo ataambiwa), hayo ndiyo uliyokuwa ukiyakimbia.” Na itapulizwa parapanda; hiyo ndio siku ya makamio, Na itakuja kila nafsi pamoja na mchungaji (wake) na shahidi (wake). (Aambiwe) ‘Kwa hakika ulikuwa umo katika ghafla na jambo hili. Basi tumekuondolea (leo pazia), kuona kwako leo kumekuwa kukali. Na yule aliyekuwa pamoja naye atasema ‘Hayo ndiyo yaliyowekwa tayari kwangu (yameandikwa na malaika). (Wakati huo kutasemwa), Mtupeni katika Jahannam kila kafiri aasi Atakatazae kheri, arukaye mipaka, aliyekuwa akijipa shaka. Aliyeweka miungu mingine pamoja na Mwenyezi Mungu, basi mtupeni katika adhabu kali.” ‘Mwenzake asema “Ee Mola wetu! Sikumpoteza mimi bali yeye mwenyewe alikuwa katika upotofu wa mbali kabisa: Aseme (Mwenyezi Mungu). ‘Msigombane mbele yangu. Nilikwisha kukutangulizieni onyo (langu). Kauli yangu haibadilishwi kwangu, wala mimi siwadhulumu waja wangu. Siku tutakapoiambia Jahannam. “Je! Umejaa?” Nayo itasema, “Je! Kuna zaidi?” Na pepo italetwa karibu, kwa wamchao Mwenyezi Mungu haitakuwa mbali (nao). Haya ndiyo mnayoahidiwa kwa kila aelekeaye (kwa Mwenyezi Mungu), ajilindae (na maasia). Na anayemuogopa (Mwenyezi Mungu) Mwingi wa kurehemu, hali ya kuwa hamuoni, na akaja kwa moyo ulioelekea (kwa Mwenyezi Mungu). (Waambiwe) ‘Ingieni (Peponi) kwa salama.” Hiyo ni siku ya kukaa daima (katika starehe za huko peponi). (Qat: 19-34).

‘JAHANNAM

Hakika yeye alifikiri na akapima (la kusema kuitukana Qur’an. Basi ameangamia. Namna gani alivyo diriki (katika kuitukana kwake) Tena ameangamia. Namna gani alivyodiriki (katika kuitukana kwake). Kisha akatazama. Kisha akakunja kipaji (chake) na akafinya uso. Kisha akaipa mgongo (haki) na akatakabari (akajivuna). Na akasema: “Hayakuwa haya (aliyokuja nayo Muhammad) ila ni uchawi ulionukuliwa (kwa wachawi wakubwa kabisa wa zamani). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni kauli ya binadamu”. Karibuni hivi nitamtia katika moto (unaowaka kweli kweli). Na nini kitakachokujulisha moto huo? Haubakishi wala hausazi. Unababua ngozi mara moja. Na juu yake wako (walinzi) kumi na tisa. (Al-Muddathir: 18 - 30).

UDANGANYIFU NA UHAKIKA

Mahali ambapo makafiri watabakia milele, pameumbwa maalum ili kuwapa machungu katika miili yao na katika nafsi zao. Hiyo ni kwa sababu makafiri watajutia kwa makosa yao makubwa na wakati huo huo uadilifu wa Mwenyezi Mungu hupelekea kundi hili liadhibiwe vikali. Kwa kukosa kwao shukurani na kumuasi kwao Muumba wao, ambaye amempa mwanadamu nafsi, hilo ni kosa kubwa kuliko jingine lolote linaloweza kufanya hapa ulimwenguni. Hivyo basi, Akhera kutakuwa na adhabu iumizayo kwa kosa kubwa la aina hii. Hilo ndilo lengo la kuumbwa kwa Moto. Mwanadamu ameumbwa ili amtumikie Mwenyezi Mungu. Kama atakanusha lengo kuu la kuumbwa kwake, kwa hakika atakachopata ndio stahiki yake. Mwenyezi Mungu amebainisha katika moja ya aya za Qur'an:

‘Na Mola wenu anasema: Niombeni nitakujibuni. Kwa hakika wale wajivunao kufanya ibada yangu, bila shaka wataingia Jahannam, wadhalilike. (Al-Muumin: 60).

Kwa kuwa watu wengi wataingia motoni mwishoni, na adhabu humo ni ya kudumu, lengo kuu, na haja ya msingi kwa mwanadamu, iwe ni kuepuka moto. Jambo linalomtisha mno Mwanadamu ni Moto. Na hakuna jambo kubwa zaidi kwa mtu kama kuikinga nafsi yake na huo moto. Pamoja na hili, takriban watu wengi katika ardhi wanaishi katika hali ya kutokuwa na habari na huo moto. Wanajishughulisha na matatizo mengine katika maisha yao ya kila siku. Kwa miezi, miaka, dahari wanashughulika na mambo ambayo ni madogo madogo, huku wakiacha kufikiri juu ya jambo kubwa linalotisha, hatari iliyokuu kwa maisha ya milele. Jahannam iko pambizoni mwao, lakini ni vipofu hawaoni.

‘Imekaribia watu hisabu yao, nao wamo katika mghafala; wanakengeuka tu. Hayawajii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao ila huyasikia, na hali wanafanya mchezo. Zimeghafilika nyoyo zao. Na wanasemezana kwa siri wale waliodhulumu (nafsi zao). ‘Ni nani huyu (Muhammad) isipokuwa ni binadamu tu kama ninyi? Je, mnafika katika uchawi (mnakiendea kiini macho) na hali ninyi mnaona?’ (Al-Anbiyaa: 1- 3).

Watu wa aina hiyo wamejitumbukiza katika mambo ya upuuzi. Wanatumia muda wao wote katika malengo yasiyo na uzio. Muda mwingi malengo yao yamepandishwa chati katika kampuni, ndoa, kufurahia maisha ya familia, kuchuma mabilioni ya fedha au kuwa wahubiri au waenezaji wa itikadi zisizo na maana. Wakati haya yanafanyika, watu hawa hawana habari juu ya majuto yalio mbele yao.

Jamii isiyo na Elimu juu ya Muumba wao ambayo ina watu wa aina hiyo hutamka neno ‘Moto’ bila ya kuwa na ufahamu kamili juu ya maana yake. Hapa na pale, somo hili huwa sehemu ya mzaha. Hata hivyo, hakuna hata mtu mmoja aliyelipa fikra za kutosha kama inavyostahiki. Kwa watu hawa, Moto ni kitu kilichozushwa na ni cha kufikirika tu. Kwa hakika, Moto ni kitu halisi zaidi kuliko dunia hii. Ulimwengu utakoma kuwepo baada ya muda fulani, lakini moto utabakia milele. Mwenyezi

Mungu, Muumba wa ulimwengu na dunia, na vyote vilivyomo ndani yake, vivyo hivyo ameumba akhera, pepo na moto. Adhabu kali iumizayo imeahidiwa kwa wote Makafiri na wanafiki.

Motoni, mahali pabaya pa kufikia ambapo huwezi kufikiria, ni chanzo cha mateso makubwa kabisa. Mateso haya na maumivu hayafanani na aina yoyote ya mateso katika dunia hii. Ni mahali zaidi kuliko maumivu ya aina yoyote au mateso ambayo yeyote amewahi kuyakabili hapa duniani. Kwa hakika hiyo ni kazi ya Mwenyezi Mungu, aliyetukuka katika busara.

Uhakika wa pili kuhusu Jahannam ni kwamba, kwa kila mmoja, mateso haya ni ya kudumu na hayana kupumzika. Wengi katika watu wa jamii hii ya kijahili wana aina moja ya kutokuelewa vizuri nadharia ya Jahannam. Wanadhani wanaweza ‘kutumikia hukumu yao huko motoni kwa muda na kisha baada ya hapo wakasamehewa. Hii ni kujipa matumaini tu. Imani hii imesambaa hata miongoni mwa ambao hujiita waumini huku wakipuuza kueleza majukumu yao kwa Mwenyezi Mungu. Wanadhani hakuna mipaka kiasi kwamba wanajiingiza katika mambo ya kidunia kuwastarehesha. Kutokana na imani hiyo hiyo, wataingia peponi baada ya kupata adhabu ya muda mfupi huko motoni. Hata hivyo, mwisho unaowasubiri ni wenye kuumiza zaidi kuliko wanavyotarajia. Jahannam ni mahali pa adhabu pasipo na ukomo. Hapafai hata kwa kukaa sekunde moja tu. Katika Qur’an imekuwa ikisisitizwa kwamba adhabu kwa makafiri haipungui wala kuongezwa na ni ya milele. Aya ifuatayo inatilia mkazo ukweli huu kwa uwazi kabisa:

“Na wataishi humo milele” (An-Nabaa:23).

Matamshi yao kwamba, ‘Nitatumikia adhabu yangu kwa muda na kisha nitasamehewa’ ni fikra zilizozalishwa na baadhi ya watu ili kujifurahisha. Kwahakika Mwenyezi Mungu ametutahadharisha na fikra za namna hii kwenye Qur’an kwa kutuonesha kuwa ni fikra ambazo hata Mayahudi walikuwanazo:

Na walisema hautatugusa moto (wa Jahannam) isipokuwa kwa siku chache tu.

Sema: “Je mmeapa ahadi ya Mwenyezi Mungu? Kwa hiyo hata khalifu

Ahadi yake, au mwamsingizia Mwenyezi Mungu mambo msiyoyajua”

Naama, wanaochuma ubaya – na makosa yao yatawazunguuka –

Hao ndio watu wa motoni; watakaa humo milele. (Al-Baqarah: 80 - 81).

Kitendo cha mwanadamu cha kuacha kumshukuru Mola wake na badala yake akadumu katika kumuasi Muumba ambaye ‘amempa (mwanadamu) kusikia, kuona, akili na huba (Rejea an-Nah: 1:78).

Kunastahiki mwanadamu huyo aadhibiwe, adhabu isiyo na mpaka. Dharura zitokewazo na mmoja wa wanadamu haziwezi kumuepusha na moto. Hakuna nafuu kwa waliokadhibisha dini ya Mwenyezi Mungu na kuendeleza unyama zaidi kwa wanadamu wenzao.

‘Na wanaposomewa aya zetu zilizo wazi, utaona chuki juu ya nyuso za wale waliokufuru. Hukaribia kuwashambulia wale wanaowasomea hizo aya zetu. Sema: ‘Je! Nikuambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni moto wa Mwenyezi Mungu aliowaahidia wale waliokufuru, na ni marejeo mabaya hayo’. (Al-Hajj: 72).

Wale waliodumu katika ujeuri dhidi ya Mwenyezi Mungu na wakazidisha uadui dhidi ya waumini, wataishia maneno yafuatayo katika Siku ya hukumu:-

**Kwa hivyo ingieni milango ya Jahannam kwa kukaa humo milele.
Basi ni mabaya kabisa makazi ya wafanyao kiburi’.** (An-Nahl: 29).

Katika moja ya mambo yanayoogopesha zaidi kuhusu moto ni ile tabia yake ya umilele. Mara utakapoingizwa motoni hakuna kurejeshwa tena. Jambo lisilo na shaka kuhusu moto na adhabu nyingine ni ile hali ya mja kubakia katika majuto milele. Mwanadamu hana matarajio mengine. Kila uchao ni adhabu juu ya adhabu kwa kiwango cha makosa yake: Qur’an inaifafanua hali hii katika aya ifuatayo:-

‘Na wale waliofanya uovu, makazi yao ni motoni, watakapotaka kutoka humo watarudishwa mumo humo na wataambiwa: Onjeni adhabu ya moto ambayo mlikuwa mkiikadhibisha – (As - Sajidah: 20).

‘ Watataka (kila namna) watoke katika moto, lakini hawatotoka humo, na watakuwa na adhabu inayodumu (kwao). (Al-Maidah: 37).

ADHABU ZA KUSWAGWA KUELEKEA MOTONI

Jahannam (Motoni)... Hii ni sehemu ambayo sifa za Mwenyezi Mungu, al-Jabbar (MtenzaNguvu), Ali-Qahhar (Mwenye Kushinda), al-Muntaqim (Mwenye kuliizakisasi), zitadhihiri kwa muda wote milele lengo likiwa kukithirisha maumivu kwa mwanadamu. Katika Qur’an Jahannam imetajwa kama vile ni kiumbe hai. Kiumbe hiki kina chuki na kutaka kulipa kisasi kwa makafiri.

Juu ya kiu ya Jahannam iliyonayo dhidi ya makafiri haiwezi kutoshelezwa hata kidogo. Kuwachukia kwake makafiri, Jahannam inaonekana kama iliyopandwa na uwendawazimu. Wakati itakapokutana na makafiri ghadhabu zake zitaongezeka. Kuumbwa kwa moto, ni kutimiza lengo moja tu, kuchochea adhabu isiyovumilika. Kwa hakika itatekeleza majukumu yake ya adhabu isiyovumilika kwa kutoa maumivu makali mno kama itakayokadiriwa na Muumba wake.

Baada ya hukumu ya makafiri kumalizika mbele ya Mwenyezi Mungu, makafiri watachukuwa vitabu vyao kutoka upande wa kushoto. Huu ndio muda watakaongozwa kuelekea motoni milele. Kwa

makafiri, hakuna fursa ya kukwepa. Kutakuwa na mabilioni ya watu, bado kundi hili halitatoa fursa kwa makafiri kutoroka au kupuuzwa asishughulikiwe. Hakuna awezaye kujificha katika kundi hili. Wale watakaopelekwa Motoni watakuwa na shahidi na mwingine atakayeichukuwa nafsi yake.

‘Na itapulizwa parapanda (Baragumu); hiyo ndio siku ya makamio, (Siku ya kiama). Na itakuja kwa nafsi moja na mchungaji (wake) na shahidi (wake). (Aambiwe) ‘Kwa hakika ulikuwa umo katika ghafla na jambo hili. Basi tumekuondolea (leo) pazia yako; kuona kwako leo kumekuwa kukali’. Na yule (Malaika) aliyekuwa pamoja naye (akiandika amali zake) atasema (kumuambia malaika wa adhabu) “Hayo ndiyo yaliyowekwa tayari kwangu (ya amali zake mbona hizi).” (Wakati huo kutasemwa).” Mtupeni katika Jahannam kila kafiri asi.” “Akatazaye kheri, arukaye mipaka, aliyekuwa akijipa shaka (zisizokuwa na sababu). Aliyeweka Mungu mwingine pamoja na Mwenyezi mungu, basi mtupeni katika adhabu kali.” (Qaf: 29 – 26).

Makafiri wataswagwa (kuendeshwa) kuelekea kwenye makazi haya ya kutisha. Katika maneno ya Qur’an, wataendeshwa kwa makundi.’ Hata hivyo, njiani kuelekea Jahannam, woga utazidishwa katika nyoyo zao. Sauti ya kutisha na kali kutoka motoni itasikika toka mbali.

‘Watakapotupwa humo watasikia rindimo (magurumo) lake, na hali ya kuwa inafoka. Unakaribia kupasuka kwa hasira (yake juu ya wabaya) walinzi wake watawauliza: ‘Je! hakukufikieni muonyaji? (Al-Mulk: 7–8).

Kutokana na aya hizo, ni wazi kuwa wakati watakapokumbwa tena (yaani watakapofufuliwa), makafiri wote wataelewa kile kilichowaangamiza. Wakati peke yao; hakutawa na marafiki, ndugu, au wenye kuwaunga mkono watakaowasaidia Makafiri hawatakuwa na ujasiri wa kuwa jeuri na watatazama kwa macho ya huruma (yaliyoinamishwa). Moja ya aya imeelekezea tukio hili kwa maneno yafuatayo:

‘Na atawaona wanapelekwa (kwenye moto), wamekuwa wanyonge kwa dhila; wanatazama (yanayopita) kwa mtazamo wa kificho. Na walioamini watasema: “Kwa hakika wapatao hasara ni wale waliohasirika nafsi zao na watu wao siku (ya leo hii) ya Kiama.” Bila shaka madhalimu watakuwa katika adhabu inayoendelea : (Ash-shuura: 45).

KUINGIA MOTONI NA MILANGO YA MOTONI

Mwishowe makafiri watafika katika milango ya motoni. Qur’an inaelezea tikio hili kama ifuatavyo:-

‘Na waliokufuru watapelekwa katika Jahannam makundi - makundi, mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake, na walinzi wake wataambia, “Je hawakuwajieni mitume miongoni mwenu wakikusomeeni aya za Mola wenu na kukuonyeni juu ya makutano ya siku yenu hii?” Watasema: ‘Kwa nini? (wametujia)! Lakini limethibiti neno la adhabu juu ya wale walio kanusha (Neno ndio sisi).’ Itasema: ‘Ingieni milango ya Jahannam mkakae humo”. Basi ni ubaya ulioje wa makazi ya wanaotakabari.” (Az-Zumar: 71 – 72).

Kwa kila kundi mlango maalum wa motoni umeumbwa kwa ajili yao. Kutegemea ni kiasi gani walimuasi Mola wao, watu watatengwa kwa madaraja. Makafiri watawekwa kila mmoja na sehemu yake kutegemea madhambi waliyoyafanya. Imeelezwa katika Qur’an:

‘(Atasema (Mwenyezi Mungu siku ya Kiama awaambie): ‘Ingieni motoni pamoja na uma zilizopita kabla yenu; za majini na watu.” Kila utakapoingia Umma utawalaani wenzao. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa nyuma wao (wale waliofuata) watasema kwa ajili ya wa kwanza wao (waliowafuata hata wakapotea) ‘Mola wetu! Hawa ndio waliotupoteza basi wape adhabu ya moto maradufu (yaani zaidi kuliko sisi).

Atasema: “Itakuwa kwenu ninyi nyote (adhabu) mara dufu, lakini ninyi hamjui tu (bado). (Al-Aaraf: 38).

Aya nyingine zinaeleza kwa undani kuhusu moto. Kwa mfano aya ifuatayo zinasema:

Na bila shaka Jahannam ndipo mahali pao walipoahidiwa wote. Ina milango saba, na kwa kila mlango uko sehemu yao iliyogawanywa (ya kuwa hii ya mlango wa fulani na hii ya mlango wafulani). (Al-Hijr: 43 – 44).

Ambao wamewekewa adhabu iumizayo zaidi ni Wanafiq. Hawa ni watu ambao hutenda kama vile ni Waumini, hapo hawana hata chembe ya imani katika nyoyo zao: ‘Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yoyote). (Annisai: 145)

Moto wa Jahannam ni wa kuogopwa, njaa ya makafiri kamwe haitaweza kuondoka (kushiba). Pamoja na kuingizwa watu wengi mno humo, bado inauliza kama kuna nyongeza:

‘Siku tutakayoimbia Jahannam: ‘Je! Umejaa?’ Nayo itasema: ‘Je kuna zaidi? (Zaidi na ije tu!)’ (Qaf: 30).

Mara unapompokea unamhifadhi humo milele. Mwenyezi Mungu anaifafanua Jahannam katika Qur’an kama ifuatavyo:

‘Karibuni hivi tutamtia katika moto (unaowaka kweli kweli). Na nini kitakachokujulisha moto huo? Haubakishi wala hausazi. Unababua Ngozi mara moja. (Muddaththir: 26 – 29).

‘Na Jahannam itadhihirishwa kwa wapotevu. Na wataambiwa: ‘Wako wapi mliokuwamkiwaabudu (Badala ya Mwenyezi Mugu). Je wanaweza kukusaidieni au kujisaidia wenyewe (Nafsi zao)? Basi watatupwa humo wao na maasi (wengine) Na majeshi ya ibilisi yote (Ash-Shu’ara: 91 – 95)

MAISHA YA KUDUMU NYUMA YA MILANGO ILIYOFUNGWA

Mara baada ya makafiri kuwasili Jahannam, milango itafungwa nyuma yao. Hapa, wataona sehemu inayotisha kupita kiasi. Watagundua mara moja kwamba wamefikishwa motoni, mahali ambapo watabakia humo milele. Kufungwa kwa milango kunaashiria kwamba hakuna ukombozi humo. Mwenyezi Mungu anaelezea hali ya makafiri kama ifuatavyo:- (Al-Balad: 19–20).

Adhabu ya motoni imeelezwa katika Qur’an kwa majina kadhaa:-

‘Adhabu kali’ (Imran: 176); ‘Adhabu Ngumu’ (*Imran: 4*), ‘Adhabu iumizayo’ (*Imran: 21*). Ufahamisho uliotolewa hautoshi kutoa picha halisi na pia hautoshi kutoa ufahamu kamili juu ya adhabu ya Jahannam. Kushindwa kuvumilia japo katika adhabu ndogo ya kuchomwa hapa duniani, mtu hawezi kuelewa hasa hali ya kuwekwa katika adhabu ya motoni milele. Zaidi ya hayo, Maumivu yapatikanayo kwa moto hapa duniani kamwe hayawezi kulinganishwa walau chembe na adhabu isiyokifani ya Jahannam. Hakuna mfano wa maumivu wa yale ya Jahannam. (*Fajr: 25 – 26*).

Kuna maisha ndani ya Jahannam. Lakini ni maisha ambayo kila muda unavyopita ndivyo adhabu inavyozidi kupamba moto. Katika maisha haya kila aina ya adhabu ya kimwili, kiakili na kisaikolojia, pamoja na aina mbalimbali za maumivu na kukoseshwa kuangaliwa kwa rehema yote yatakuwa yakijiri. Haiwezekani kulinganisha na matatizo ya aina yoyote hapa duniani. Watu huko motoni watakuwa wanapata maumivu kwa kupitia njia zote tano za milango ya fahamu. Macho yao yataona picha za kutisha mno na za kuchukiza; Masikio yao watasikia sauti zenye kukera, zikinguruma na vilio, pua zao zitahisi harufu ya kuchukiza na mbaya mno; ndimi zao zitaonja maonjo yasiyo vumilika. Wataihisi Jahannam katika kila chembe hai iliyo mwilini mwao. Hii ni hali anayochochea maumivu makali na kumfanya mtu aonekane kama mwendawazimu kiasi ambacho hali hiyo haiwezi kufikirika katika ardhi hii. Ngozi zao, viungo vyao vya ndani na mwili wao mzima utakuwa unapata machungu. Watu wa motoni watakuwa wanastahamili mno maumivu na hawatakufa. Hivyo, kamwe hawawezi kujiokoa kutokana na adhabu. Ngozi zao zitarudishwa upya kila zitakapounguzwa; adhabu hiyo hiyo ikiendelea milele; ukali wa adhabu kamwe hautapungua. Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Qur’an: (*At-Tur: 16*).

Hakuna kupata maumivu ya kutisha huko motoni zaidi ya yale ya kimwili na kiakili. Watu wa motoni watazidi kujuta, wakiangalia kukata tamaa, wakiwa hawana matumaini na wakiendelea hivyo zama na zama wakijuta. Kila upande, kila mahali katika Jahannam pametengenezwa, ili kutoa machungu ya kiakili. Machungu haya ni ya milele. Kama itakoma baada ya miaka milioni au bilioni kadha, hata kipindi kirefu kama hicho kitatoa hisia za matumaini na kuwa ndio hoja kubwa yenye nguvu ya matumaini na furaha, bado, hali ya adhabu ya milele itachochea aina ya kukosa matumaini ambayo haiwezekani kulinganishwa na aina yoyote ya hisia katika dunia hii. Kutokana na Qur'an Jahannam ni mahali ambapo maumivu yasiyo na kifani huonekana. Ni nyembamba, yenye kelele, yenye moshi na ngurumo, ichocheayo hisia na kukosa usalama katika moyo wa mwanadamu. Ni mahali palipo na tabia ya kuwa na harufu ichukizayo, moto uunguzao ndani ya moyo, chakula na kinywaji kibaya, nguo za moto na kinywaji kichungu. Hizi ndizo tabia za msingi za Jahannam. Hata hivyo, kuna maisha yanayoendelea katika mazingira haya ya kutisha. Watu wa motoni wana hisia kali. Wanasikia, wanazungumza na kuhoji, na wanajaribu kutoroka kutoka katika maumivu. Wanaungana katika moto, wanapatwa na kiu na kuwa na njaa, na kuhisi majuto. Kilicho muhimu zaidi, wanataka machungu yaondolewe yasiwepo tena wapate nafuu. Watu wa motoni wataishi maisha ya milele katika daraja la chini zaidi kuliko wanyama katika mazingira haya machafu na ya kuchukiza. Kilicho mbele yao chenye kuyapamba mazingira ni matunda makali ladha yake, yenye miiba na miti ya Zaqqum. Vinywaji vyao kwa upande mwingine ni damu na usaha. Wakati huohuo, moto umewazunguka katika kila upande.

Huku wakibadilishwa ngozi, nyama ikiunguzwa na damu ikitiririka mwili wote, watakuwa wamefungwa minyororo na kuchapwa. Mikono ikiwa imefungwa katika shingo zao, watatumbukizwa katikati ya Jahannam. Malaika wa adhabu kwa wakati huo wakiwaweka wale wakosaji katika vitanda vy moto, na mashuka yao yakiwa ni moto. Makafiri kila wakati watatamani waokolewe kutoka katika hali hiyo. Na badala yake, wanazidi kupata adhabu iumizayo na maangamizi. Wataachwa peke yao. Hali hii yote itakuwa kweli. Ni hakika. Ni hakika zaidi kuliko maisha yetu haya.

(Al-Hajj: 11)

(Imran: 24)

Wale wanaofanya kutengeneza pesa, vyeo, utukufu na mambo mengine ya kidunia kama ndio malengo makuu ya maisha na hapohapo wakadharau/wakapuuzwa mambo mazuri ya Mwenyezi Mungu; wale wanaobadili maamrisha ya Mwenyezi Mungu kutokana na kupenda kwao na kutemani kwao, wale wanaotafsiri Qur'an kwa matakwa yao, wale waliopotea njia kutoka katika njia iliyonyooka – Kwa muhtasari:– Makafiri wote na wanafiqi wote wataingia motoni, isipokuwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewasamehe. Hili ndilo hitimisho la Mwenyezi Mungu katika maneno yake.

Na kwa hakika itakuwa hivyo.(As-Sajida: 13)

Watu hawa tayari wamekadiriwa kuwa ni wa motoni:- (As-A'raf: 179)

ADHABU YA MOTO

Katika maisha ya Jahannam, kubwa kabisa na la msingi kabisa katika adhabu hapana shaka ni kuchomwa moto. Kinyume na aina nyingine za adhabu moto, ni aina ya kipekee ya Jahannam, kwani haisazi chochote katika mwili wa Mwanadamu.

Ni adhabu ipenyayo mwili wa mwanadamu hadi kwenye kiini. Watu wa Jahannam watatupwa katika huo moto uwakao kwelikweli.’ (Al-Ma’arij: 15)

Unachoma katika ‘Moto Ufokao’ ambao ni ‘Moto Ubabuao’ (Al-layl: 14)

Pia angalia aya za Qur’an, katika Al-Qariah: 8 – 11)

Kutokana na aya hizo; Mwanadamu anaelewa kwamba moto uwakao kweli kweli ni katika Jahannam yote. Katika ufupi huu, hakuna eneo ambalo linaweza kuhifadhika na moto. Moto ukifika kila pembe ya Jahannam. Wakati adhabu za aina mbali mbali za kimwili na kiakili zikiendelea, bado mwanadamu atakuwa hana uwezo wa kukwepa moto. Utakuwa unamuunguza mfululizo. Jahannam Moto wake ni mkubwamno. Katika Qur’an inaelezewa miale ya moto kuwa ni sawa na miale mikubwa sawa na kundi la nzige na kundi la ngamia wa manjano kuonesha ukubwa na uzito wa moto. (*Al-Mursalat: 28 – 33*)

Wasioamini (Makafiri na Washirikina) watatumia nguvu zao zote kujiepusha na miale (ya moto), lakini haitaruhusiwa. Ni moto ambao:-

‘Ambao unawaita wote wanaogeuzwa migongo yao na wanaokimbia’ – (Al-Maarij: 17).

Aya nyingine inafahamisha hatima ya wanaokanusha kwamba (As-Sajida: 20)

Makelele na mitetemo ya wale walioingizwa motoni, itasikika kila upande. Hata hii mitetemo na makelele yenye kuogofya ni miongoni mwa vyanzo vya adhabu kwa makafiri.

Kutakuwa na vilio kwa ajili yao – (An-Nbiyaa: 100).

Ama kwa wale waliokadhibisha, watakuwa motoni, ambamo watatetemeshwa na kufungwa. (Hud:106).

Jahannam ina maumivu yasiyovumilika. Wanadamu hawawezi kustahili maumivu kama ya moto wa ujiti wa kibiriti. Hiyo kwa haya ni zaidi. Hata hivyo maumivu yoyote tunayohisi katika dunia hii ni kidogo mno ukilinganisha na yale yatokanayo na moto wa Jahannam. Hakuna anayebakishwa katika moto wa duniani kwa muda mrefu. Ama atakufa baada ya Sekunde 5 hadi 10 au asikie maumivu kwa

kipindi kifupi tu. Hata hivyo moto wa Jahannam unatisha, unaleta maumivu endelevu. Watu wa motoni watakuwa kwenye moto na watabakia humo milele. Kujua kwao kwamba adhabu hii haina ukomo, huwafaya wale walioingizwa humo kuwa katika kipindi cha majonzi na kukosa matumaini. Huhisi kukata tamaa na hivyo kuwa katika hali ya kuhisi maangamizi ya milele.

Kuunguzwa uso ni moja ya mambo ambayo hayafakiriwi na yeyote. Hii ni kwa sababu uso au wajiji ni kiungo muhimu ambacho Mwanadamu anajivunia. Unampa mwanadamu kutambulika na ndio unaoonesha waziwazi kile tunachoiita ‘Mimi’. Mara nyingi, umbile la kuwa unachukiza au unapendeza huhusishwa zaidi na uso. Kwa kuona picha ya mtu aliyeungua vibaya usoni mwake, huanza kunywea na hatimae mara moja hurejea kwa Mola wake ili alindwe/akingwe dhidi ya majanga kama haya. Hakuna hata mmoja anayetamani apigwe na dhoruba kama hiyo. Hata hivyo makafiri wameghafilika juu ya jambo moja; wanaelekea kwenye hatima inayofanana hivyo; na kwa hakika mwisho huo ni mbaya zaidi. Maumivu yatokanayo na moto wa Jahannam hupenya na kuenea mwili nzima wa mwanadamu. Hata hivyo pindi uso utakapooni moto, yatakuwa ni maumivu yasiyoweza kuvumilika. Macho, masikio, pua, ulimi na ngozi, kwa muhtasari kila kiungo cha fahamu kimo katika sehemu hii ya mwili. Jambo lolote baya katika uso, hata liwe dogo kiasi gani, hutoa hisia kali kwa mwanadamu. Hata hivyo kwa Jahannam, uso ndio utakaogeuzwa geuzwa. Kwa namna hiyo, sehemu muhimu mno ya mwili wa mwanadamu itakuwa imedhurika vibaya sana. Adhabu hii imetajwa katika aya kadhaa, Miongoni mwa hizo i:-

‘Siku nyuso zao zitakapogeuzwa geuzwa katika moto, watasema, ‘Majuto yetu, kama tungemtii Mola wetu na tukamtii Mtume’ (Al-Ahzab: 66).

Nguo zao za lami na nyuso zao zilifunikwa na moto (Ibrahim: 50).

Moto utaunguza nyuso zao, na humo watakuwa ni wenye kutisha, midomo yao ikiondolewa kutoka mahali pake. (*Al-Muumin: 104*). Ikimaanisha kuwa meno yao yatakuwa nje, baada ya midomo yao kuondolewa.

KUNI ZA JAHANNAM NA MAJI YENYE KUCHEMKA

Katika Qur’an, maelezo kuhusu njia ambayo makafiri watachomwa katika moto ni kuwa; kwanza, makafiri wenyewe watakuwa ndizo kuni za huo moto. Kuchomwa kwao hakufanani na kuchomwa kwa kitu kingine katika moto. Makafiri watakuwa ndio mafuta ya moto.

‘Lakini wale wanaokufuru, hawatakuwa chochote ila mafuta (kuni) za moto wa Jahannam.’ (Al-Jinn: 15).

Kuni zinazowasha moto huungua kwa muda mrefu zaidi kuliko kitu kingine chochote na kwa mwako mzito zaidi. Vivyo hivyo makafiri watakuwa kuni za moto huu ambao awali waliukanusha. Uhakika huu unabainishwa wazi katika aya zifuatazo:-

‘Enyi Mliamini! Jiokoeni nafsi zenu na jamaa zen na moto ambao kuni zaken i watu na mawe... (Tahrim: 6).

‘Wale waliokanusha Imani (Makafiri), mali zao na watoto wao hawawezi kuwasaidia chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Wao hawatakuwa kingine zaidi ya kuwa kuni za moto. (Al-Imran:10).

‘Kwa hakika ninyi (makafiri), na vile mnavyoviabudu kinyume na Mwenyezi Mungu, mtakuwa kuni za Jahannam! Kwahakika humo mtaingizwa tu! (An-Biyaa: 98).

Pamoja na watu kutumika kama kuni, pia zipo kuni halisi katika kuchochea moto. Hivyo, hali hii nayo ni chanzo kingine cha adhabu. Makafiri ambao awali walikuwa karibu zaidi duniani, kwa mfano mke na mume, watachukuwa kuni kila mmoja kwa ajili ya moto wa mwenzake.

‘Imeamgamia mikono ya Abu Lahab na ameamgamia. Hakikumsaidia chochote katika mali yake na kila alichokichuma. Hivi karibuni ataingizwa katika moto uwakao. Na mke wake (mchukuzi wa) kuni kwa kamba zilizosokotwa za majani ya mtende katika shingo yake.’ (*Lahab: 1- 5*).

Huu ndio mwisho wa uhusiano wa aina zote katika dunia hii. Makafiri ambao walikuwa na tabia ya kusema wanapendana mno na huku wakimuasi Mola wao kwapamoja, watakuwa kuni za mmoja dhidi ya mwingine huko Jahannam. Mke kwa mume au mume kwa mke, ndugu wa karibu na marafiki wote na kati ya watakuwa maadui. Mahandaki hayatajua mipaka. Moto uliokokwa kwa kuni hai na zile zisizo hai, pia zitachemsha maji ambayo yatawaunguza makafiri. Ngozi; ambayo ni moja kati ya viungo vya thamani katika mwili wa mwanadamu iliyotanda juu ya mwili wote wa huyo mwanadamu na unene wake si zaidi ya milimita kidogo tu, huwa ni kiungo muhimu katika mawasiliano baina ya binadamu na dunia ya nje kwa hisia za kugusa. Pamoja na viungo vya sehemu za siri, viungo vingine vya mwili kama vile uso, mikono, vitanga vya mikono, miguu, viungo ambavyo kila mtu huvichukulia kwa uzito wa hali ya juu kabisa, vimefunikwa na ngozi. Pamoja na ukweli kuwa inachukuliwa kama kiungo mja anachojivunia, kutokana na unyeti wake, sasa ngozi itakuwa chanzo kikubwa cha maumivu. Ngozi itakuwa maalum kwa kubabuliwa na moto na maji yanayochemka. Huku moto ukiibabua ngozi, maji nayo hufanya kazi ya kuiivisha na kuinyumbua nyumbua. Maji hayo yachemkayo yatakwangua ngozi yote; ni vigumu kusalia sehemu yoyote ya ngozi ambayo haitaathirika. Awali, ngozi hii nyembamba itavimba na kisha itakuwa inaunguzwa na hivyo hutoa maumivu makali. Hakuna utanashati, utajiri wa mali, nguvu, ujasiri na kwa muhtasari, hakuna kikwazo kutokana na maumivu yaliyofanywa na maji yachemkayo kweli kweli. Kwa maneno ya Qur’an

‘... Watakuwa na maji yachemkayo kweli kweli kwa ajili ya kunywa’ (Al-An’am: 70).

Katika aya nyingine imesemwa:

‘Na kama atakuwa miongoni mwa waliokadhibisha na wakatenda maovu, kwake yeye kuna ukaribishwaji kwa maji ya moto yanayochemka na kuunguzwa kutoka Jahannam. Kwa hakika, hii ndio kweli na hakika. (Al-Waqiah: 92–95).

Aya nyingine imeelezea aina hii ya adhabu kama ifuatavyo:-

(Sauti itasikika): ‘Mkamateni na msukumeni mpaka katikati ya Jahannam. Kisha mmiminieni kichwani mwake adhabu ya maji yachemkayo. (Aambiwe) ‘Onja hii! Wewe ulikuwa mwenye nguvu, mheshimwa. Kwa hakika hii ni katika yale uliyoyatilia shaka. (Ad-dukhan: 47 – 50).

Mbali na hizi adhabu zilizotajwa juu, pia zipo aina nyingine za adhabu zitokanazo na moto. Miongoni mwao ni kupigwa chapa. Watu wa motoni watapigwa chapa kwa chuma cha moto kilichofikia wekundu. Hata hivyo, vyuma hivi ni machuma ya makafiri kutokana na vile ambavyo Mwenyezi Mungu ameshirikishwa navyo hapa duniani.

‘...Kwa wale waliokuwa wakichuma dhahabu na fedha kisha wakazitumia katika njia ambayo si ya Mwenyezi Mungu. Wape habari juu ya adhabu iumizayo. Siku ambayo moto utatolewa katika vile walivyovichuma katika Jahannam, na kwa vitu hivyo watapigwa chapa katika paji la uso, mabegani na migongoni mwao. (Waambiwe) ‘Hii ni ile (mali) uliyoizika kwa ajili yenu. Onjeni! kisha, katika vile mlivyochuma (mlichoijilimbikizia). (At-Tawbah: 34 – 35).

AINA NYINGINE ZA ADHABU

Kinyume na inavyochukuliwa na wengi, Jahannam sio tu kwamba ni ‘jikokubwa’ ambamo watu wa motoni wataingizwa. Hii ni kweli. Hata hivyo, adhabu ya Jahannam haikufungika na kuchomwa tu. Watu wa motoni kadhalika watazingirwa na adhabu za aina nyingine za kimwili na kinafsi. Njia nyingi na vifaa vingi hutumika kumuweka mmoja katika adhabu hapa duniani. Mara nyingi adhabu humfanya awe kilema yule anayeadhibiwa. Wakati mwingine hufariki dunia kutokana na maumivu. Wale ambao wamepona wengine huwa mataahira. Bado, ukweli unabaki kuwa mbinu zinazotumika kutoa adhabu katika ulimwengu huu kimlinganisho ni dhaifu au ni ndogo mno kulinganisha na zile za motoni. Watu wa motoni wataadhibiwa kwa njia tofauti kabisa na hizi zitumikazo hapa duniani. Kwa yule ambaye anaadhibiwa kwa kutumia mitambo ya Umeme – umeme wenyewe pamoja na machungu yote ayapatayo mwanadamu kutokana na mitambo na maumivu ya umeme, vyote ni vimeumbwa na Mwenyezi Mungu. Aina nyingine nyingi zisizojulikana za vyanzo vya maumivu na udhaifu wa

mwanadamu, vyote vinajenga sehemu ya Elimu iliyokamili, isiyo na upogo. Vivyo hivyo Mwenyezi Mungu ataadhibu kwa namna ambavyo hakuna mfano wake. Hii ni kanuni ya Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu (Al-Wahhad. Katika maneno ya Qur'an, katika Jahannam, kuna adhabu kila mahali. Hakuna ahueni ya kutoadhibiwa, itawaenea watu wa motoni kutoka kila upande. Hawawezi kupewa ahueni wala wao wenyewe kuikwepa adhabu.

‘Wanakuuliza juu ya kuharakishwa adhabu. Lakini, kwa hakika Jahannam itawazunguka makafiri wote. Siku hiyo adhabu itawafikia kutoka juu yao na kutoka chini yao. Na (sauti) itasema: ‘Onjeni (matunda) ya vitendo vyenu. (An-Kabuut: 54 – 55).

Mbali na hayo, vyanzo vingine huko motoni ni vile vilivyobainishwahapa chini:-

‘Jahannam – watachomwa humo – kitanda kibaya (kwa hakika kulala humo)! Wana maskani mabaya Humu! Kisha wataonja, maji yachemkayo, kinywaji cheusi, kilichooza (usaha) na chabaridi kweli kweli na adhabu nyingine mfano wa hizo. (Sad: 56 – 58).

Kutokana na aya hii na nyingine, Mwanadamu atafahamu kuwa kuna aina nyingine za adhabu huko motoni. Zilizo wazi zaidi ni kama vile moto (kuunguzwa), kusimangwa, hizi zimerejewa sana katika Qur'an. Hata hivyo, watu wa motoni hawana kinga kwamba wasiadhibiwe kwa aina nyingine ya adhabu. Kwa mfano, kuna kushambuliwa na wanyama mwitu, kutumbukizwa katika shimo la wadudu, ng'e na nyoka, kuumwa na panya, kuuguza vidonda vitokanavyo na minyoo, na aina nyingine nje ya fikra za mwanadamu ambazo zinaweza kama kuwakabili watenda maovu kwa wakati mmoja.

JOTO KALI, GIZA TOTORO, MOSHI NA WEMBAMBA

Sehemu nyembamba, yenye joto na ambayo ni chafu huudhi mno mtu kuwemo humo katika dunia hii. Mvuke na joto husababisha hali ya kukosa raha; hali ngumu ya upumuaji. Jambo ambalo ni muhimu kwa mwili wa mwanadamu huwa gumu katika mahali ambapo mvuke wake ni mwingi. Kushindwa kupumua, husababisha kulegea viungo, kifua kupandishwa juu na kushushwa. Hata kivuli hakiwezi kutoa nafuu au ahueni katika sehemu yenye joto kali na mvuke mwingi. Hewa nzito ambayo haionekani iliyoenea husababisha kukosa raha. Pia kiwango cha joto na mvuke katika siku za kiangazi ni vigumu kustahmili (au kuvumilika). Hali hii tete, ndiyo itakayoenea Jahannam yote. Mwanadamu ambaye amechukuwa tahadhari aina kwa aina ili kuzuia kuwa katika joto kali hapa duniani, atahisi kukata tamaa huko motoni. Jahannam ni joto kuliko jangwa lolote na chafu zaidi na sehemu ya ukandamizaji kuliko sehemu yoyote inayoweza kufikiriwa. Joto hupenya mwili wa mwanadamu, itaweza kuhisiwa katika kila chembe ya uhai mwilini. Kwa makafiri hakuna uwezekano wa kupata nafuu au joto kupozwa humo. Katika Qur'an, hali ya watu wa motoni imebainishwa kama ifuatavyo:

‘Na watu wa kushoto – Ni akina nani hao watu wa kushoto? (Watakuwa) katikati ya moto uwakao wa Jahannam na katika maji yachemkayo. Na katika kivuli cha moshi mweusi. Hakuna (humo) kupumzika wala kustarehe. (Al-Waqiah: 42 – 44).

“Ole wao siku hiyo! Wale wanaokadhibisha! “(Itasemwa)” Ondokeni muendee kile mlichokuwamkikanusha mkidhani ni uongo. Kiendeeni kivuli (cha moshi) kilicho katika mihimili mitatu. (ambacho hutoa) kivuli kisicholeta baridi, na kisichopunguza joto. (Al-Mursalat: 28–31).

Katika mazingira hayo, na kuwemo katika sehemu nyembamba inathibitisha aina nyingine ya adhabu. Aina hii ya adhabu imeainishwakama ifuatavyo:-

‘Na wakati watakapotupwa, wakafungiwa pamoja, katika sehemu iliyo njembamba humo, watalilia waangamizwe humo na kisha (isemwe) ‘Siku ya leo msiombe kuangamizwa mara moja tu, ombeni kuangamizwa kwenye kujirudia rudia (mara nyingi). (Al-Furqaan: 13 – 14).

Kufungiwa sehemu nyembamba katika dunia hii, humfanya mtu awe kichaa (aharibikiwe kifikra). Kuwekwa katika Selo kwa wafungwa gerezani (tena nyembamba) ni moja ya adhabu mbaya kabisa kwa wafungwa. Kubakia katika mgandamizo wa gari mara baada ya ajali, au kuwa katika vifusi vya majengo yaliyoporomoka mara baada ya tetemeko la ardhi, huchukuliwa kama ni miongoni mwa majanga makubwa. Hata hivyo mifano kama hiyo ni kiwango cha chini mno ukilinganisha na matukio kama hayo huko motoni. Tangu hapo, mtu anayekuwa katika vifusi au mikandamizo mingine, mara nyingi hupoteza fahamu na kufa au kuokolewa hai baada ya muda fulani. Katika hali zote mbili maumivu hutoweka baada ya muda fulani.

Hali si hivyo kwa Jahannam. Hakuna mwisho wa maumivu katika moto na hivyo hakuna matumaini. Katika uchafu, unaonuka, uliooza, sehemu yenye fukuto na moshi uliojaa. Makafiri hali ya kuwa mikono yao imefungwa katika shingo zao na kuwekwa katika chumba kidigo, watakuwa kwenye kuadhibika kikweli kweli. Watajitahidi, kupambana ili wapate ukombozi, lakini wapi! Hawezi japo kusogea. Mwishowe, ataomba aruhusiwe kupotea, kama ilivyoelezwa katika aya, na kutamani japo awe amekufa. Ombi hili litarejeshwa kwake. Katika shimo hilo dogo alimowekwa atabakia kwa miezi, miaka na pengine mamia ya miaka. Kukosa amani kutajaza moyo wake, wakati akiomba zaidi ya mara elfu ili atoweke. Mara ataondolewa si kwa kupata wokovu bali atakuwa anahamishiwa katika kituo chengine cha adhabu mumo humo motoni.

CHAKULA VINYWAJI NA MAVAZI

Ulimwengu umesheheni aina mbalimbali za vyakula. Viko ambavyo ni vitamu na vyenye vimea vinavyohitajika mwilini. Vingine ni vichachu, vichungu na vikali, vyote vikihitajika kwa mpangilio maalum mwilini. Kila kimoja ni katika Rehema ya Mwenyezi Mungu. Aina mbalimbali za nyama,

matunda na mbogamboga vyenye rangi mbalimbali, ladha na harufu, maziwa na vilivyosindikwa kutokana na maziwa, asali na aina nyingi katika vimea vya vyakula vinavyozalishwa na wanyama na viungo vya aina zote, vyote hivi vimeumbwa maalum na Mwenyezi Mungu na kwa uungwana akapewa Mwanadamu kutokana na dhima aliyopewa tangu kuumbwa kwa ulimwengu huu. Zaidi ya hayo, hisia za mwanadamu zimeumbwa kwa namna ambayo zinaweza kupokea vyakula hivi vyenye ladha ya aina yake. Kwa kupelekwa wahy (ufunuo) na Mwenyezi Mungu, Mwanadamu anapata hamu katika vyakula visivyo na uvundo na wakati huohuo akikereka kwa vyakula vilivyooza na kunuka, usaha na kadhalika. Huu nao ni aina ya wahy toka kwa Mwenyezi Mungu.

Upendeleo, mkubwa zaidi ya huu hapa duniani, umewekwa maalum katika Pepo, na kutokana na huo waumini watawuna manufaa hayo milele. Hii ni zawadi ya Mwenyezi Mungu ambaye hutoa Rehema na Utukufu. Wakazi wa motoni kwa upande wao, kutokana na vitendo vyao vibaya walivyofanya katika dunia hii, watawekwa mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu, ambaye ni Al-Razzaq, hivyo yote watayokabiliana nayo ni adhabu.

Ni katika siku ambayo watapelekwa mbele ya moto ‘Mmepata vitu vyenu vizuri katika maisha ya ulimwenguni. Na mmepata faraja kutokana nayo; lakini leo mtalipwa adhabu idhalilishayo kwa vile mlikuwa Jeuri katika ardhi bila ya kutenda uadilifu, na kwamba mlizidi katika kuchupa mipaka. (Al-Ahqaf: 20).

Hakutakuwa tena na upendeleo kwao. Hata kule kukutana na mahitaji muhimu inakuwa adhabu. Chakula maalum kimeambwa na Mwenyezi Mungu kama sehemu ya adhabu. Kuleta maumivu. Chakula pekee kilichoandaliwa kwa ajili yao ni pamoja na matunda makali yenye miiba na mti wa Zakkum, ambao kamwe haunenepeshi wala hauondo njaa. Bali hutoa machungu, kuchana midomo, shingo, matumbo na kutoa ladha na harufu yenye kuchukiza. Katika Qur’an tunaona ufafanuzi wa sehemu zote mbili, wa peponi palipo na uzuri uliotukuka na vyakula vizuri, na ule wa motoni wa vyakula visivyovumilika kwa ajili ya watu wa motoni.

‘Je! Karibisho la namna hii silo bora au kupata mti wa Zakkum? Kwa hakika tumeufanya kuwa jaribio kwa watenda maovu. Hakika ni mti ulioota toka chini kabisa ya Jahannam. Matunda yeke ni kama kichwa cha shetani. Bila shaka wao watakula katika huo wajaze matumbo yao: (As-Saaffat: 62 – 66).

Hakuna chakula kitakachokuwepo kwa ajili yao ila miiba michungu. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa. (Al-ghaashiyah: 6 – 7).

Watu wa motoni kwa kuwa kwao waasi na wasiomshukuru Mwenyezi Mungu wanastahili adhabu hiyo. Kama adhabu, wanakabiliana na karibisho la aina hiyo. Katika Surat Waqi’ah, karibisho hili limeelezwa kama ifuatavyo:-

‘Hakika wao kabla ya haya walikuwa wakiishi maisha ya anasa. Na walikuwa wakishikilia madhambi makubwa makubwa. Na walikuwa wakisema ‘Nini! tutakapokufa na kuwa udongo na mifupa kweli tutafufuliwa? Na wazee wetu wa zamani?’ Sema, Bila shaka, wa mwanzo na wa mwisho. Wote kwa hakika watakusanywa katika mkutano wa siku maalum. Kisha, ninyi mliopotea na kukadhibisha, kwa hakika mtaonja mti wa Zaqqum, kisha mtajaza matumbo yenu. Na mtakunywa maji yachemkayo juu yake: Kwa hakika mtakunywa kama ngamia mgonjwa aliye na kiu sana. Hiyo ndio karamu yao ya siku ya malipo. (Al-Waqi’ah: 45 – 56).

Hapa ulimwenguni, mara kadhaa, mtu anaweza akaugua kutokana na kuvimba na kuumwa mno koo au maumivu ya tumbo. Hata hivyo katika Jahannam, kamwe hakuna muda utakaopita bila maumivu kutokana na aina hizi za maumivu. Vyakula wanavyotakiwa kula vyenyewe vinakera. Kama watadiriki kumeza, wataona kama walivyokula matumboni mwao vyuma vilivyo yeyushwa.

‘Bila shaka mti wa Zaqqum. Ni chakula cha (kuliwa na) maasi. (Kwa umoto wake ni) kama shaba iliyoyeyushwa; huchemka matumboni kama mchemko wa maji ya moto kabisa. (Kuambiwe): Mkamateni (huyu asi) na mumtupe katikati ya Jahannam. Kisha mwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji ya moto. (Aambiwe) ‘Onja! Ulikuwa wewe ni mwenye nguvu, Mheshimiwa. Hakika hii ndio ile mliyokuwa mkibishana, (mkitilia shaka). (Ad-Dukhan: 43 – 50).

Kamwe hakishibishi. Katika hali kama hii, watu wa motoni wataumia milele, kwa njaa ya ajabu. Adhabu hii si kwamba inatokea mara moja tu. La! Hii ni adhabu ya kujirudia rudia milele. Watu wa motoni watahisi njaa kwa kiwango cha hali ya juu. Watu hawa watajaribu mara kwa mara wapatiwe msaada, haupatikana msaada kwao ila kupewa matunda ya miiba yaliyo machungu yanayofanya wachanganyikiwe kwa uchungu. Kisha wanakimbilia maji yachemkayo. Na maji haya kamwe hayawezi kuyeyushwa.

Kama ilivyobainishwa katika aya hapo juu, watayabugia kama wanywavyo ngamia waliochanganyikiwa kwa kiu. Ili adhabu hii ifanywe kali zaidi, makafiri wataswagwa kuingizwa motoni hali yakuwa ni wenye kiu kweli kweli. Hayo, tunafahamishwa katika aya ifuatayo:-

‘Na tutawachunga waovu (kuwapeleka) katika Jahannam, hali ya kuwa wana kiu kubwa. (Mariam: 86).

Mbali na maji yachemkayo, kinywaji kingine chenye kuchukiza kwa ajili ya watu wa motoni ni usaha. Maji haya (usaha) yanatokana na mwasho, moja katika vinavyotoka katika mwili wa Mwanadamu hali yakuwa na harufu mbaya kabisa, ni chaguo la pili la makafiri. Usaha watapewa makafiri pamoja na damu. Katika aya nyingine, inaainishwa kuwa usaha utapewa makafiri pamoja na maji yachemkayo, ili makafiri waonje ladha mbaya ya usaha na wapate ukali wa maji ya moto katika ufahamu wao wote. Pamoja na kule kuumiza kwake na kutovumilika, bado makafiri watakunywa ili kutosheleza mahitaji yao kuonesha hamu yao ya kunywa ili kukata kiu. Mara watakapoonja adhabu hii

watakimbilia nyingine. Hali hii pia itaendelea milele. Kutokana na kutokatika kwa kiu, watu wa motoni watakuwa wanahaha katika kusaka vya kuondosha kiu yao.

‘Hawataonja humo baridi wala kinywaji; Ila maji yachemkayo sana na usaha. (An-Nabaa: 24 – 26).

‘Basi leo hapa hana rafiki mpenzi: Wala hana chakula ila maji ya usaha: Hawakili hicho isipokuwa wakosa – (Al-Haqqah: 35 – 37).

Makafiri watafanya juhudi kutaka kuumeza huu mchanganyiko, lakini haitaleta nafuu. Damu na usaha utawakereketa lakini hawafi:

‘Ambaye mbele yake kuna Jahannam na atanyweshwa maji ambayo ni usaha. Awe anayagugumiza lakini hawezi kuyameza. Na (sababu za) mauti zitamjia kutoka kila mahali, lakini hatakufa. Na mbele yake kuna adhabu kali vile vile. (Ibrahim: 16 – 17).

Katika hali hii ya kukata tamaa, kwa njia ya majadiliano maalum, wakazi wa motoni watawaona watu wa peponi. Watashuhudia neema mbalimbali za kustaajabisha walizoruzukiwa. Hili nalo litazidisha machungu yao. Wakati huohuo, watu wa motoni wataomba sehemu katika vile walivyopewa watu wa peponi. Lakini hili nalo litatupiliwa mbali:-

‘Na watu wa motoni watawaita watu wa peponi, (kuwaambia): ‘Tumiminieni (Tumwagieni) maji au (kitu) katika vile alivyokupeni Mwenyezi Mungu.’ Waseme (watu wa peponi), ‘Hakika Mwenyezi Mungu ameharamisha vyote viwili hivyo kwa makafiri.’”(Al-Aaraf: 50).

Mbali na fursa hizo, nguo za watu wa motoni pia zimetengenezwa kwa ajili yao tu. Ngozi ya mwanadamu ni yenye hisia kali; hata kugusa jiko la mafuta lililopata joto au pasi kwa sekunde moja hutoa maumivu yasiyo na kifani. Katika hali kama hiyo aliyeungua hupata maumivu kwa muda wa masiku kadhaa, hali kidonda kikioza na kuvimba au kupona. Jahannam, kwa upande wake, kuna mavazi ya moto kuliko chuma kilichoyeyushwa, ambacho hugeuka kuwa miale ambayo hufunika ngozi na kuuguza kabisa kabisa.

“... Basi wale waliokufuru watakatiwa nguo za moto na watamiminiwa juu ya vichwa vyao maji yachemkayo. Kwa maji hayo vitayeyushwa vilivyomo matumboni mwao na ngozi zao (Pia). (Al-Hajj: 19 – 20).

‘Na utawaona wakosa siku hiyo wamefungwa katika minyororo. Nguo zao zitakuwa za lami, na moto utazijia nyuso zao (uzibabue). (Ibrahim: 49 – 50).

‘Watakuwa na magodoro ya moto wa Jahannam; na nguo zao za kujifunikia (pia). Na hivi ndivyo tunavyowalipa madhalimu. (Al-Araf: 42).

MALAIKA WA ADHABU

Pamoja na adhabu yote hiyo itakayowakabili makafiri; hakuna hata nafsi moja itakayoweza kutoa msaada kwa watu wa motoni. Hakuna nafsi itakayoweza kuuokoa kutoka katika adhabu. Kwa kutekelezwa huku, kutawapa uchungu mkubwa wa upweke. Kwa madhalimu, Mwenyezi Mungu anasema katika Qur’an: ‘Hivyo, hii leo, hana rafiki.’ *(Al-Haqqah: 35).*

Miongoni mwao kuna ‘Malaika wa adhabu ambao ataadhibu kikweli kweli. Hawa ni wakali, wasio na huruma, walinzi wanaotisha, wasio na jukumu lingine zaidi ya kuwaadhibu waovu. Madhumuni ya kuwepo kwao ni kulipiza kisasi kwa wale walio muasi Mwenyezi Mungu, na wanatekeleza jukumu lao hilo kwa ustadi mkubwa na tahadhari.

‘Enyi Mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na watu wenu na moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali; wenye nguvu, hawamuasi Mwenyezi Mungu kwa amri zake na wametenda waliyoamrisha’. (At-Tahym: 6).

‘Sivyo hivyo! Kama haachi, tutamkokota kwa nywele za utosi. Utosi muongo, wenye Madhambi. Basi na awaite wanachama wenzake. Na sisi tutawaita malaika wa motoni. Sivyo!, Usimtii, bali Sujudu na uwe karibu – (Al-A’laq: 15 – 19).

Malaika hawa wa adhabu huwafanya makafiri wahisi laana ya ghadhabu za Mwenyezi Mungu kupita kiasi, na yenye kutesa mno. Nukta moja hapa inahitaji mazingatio; Malaika wa motoni (wa adhabu) kamwe hawawezi kufanya ukatili au kutokuwa waadilifu. Kazi yao wao ni kutekeleza adhabu kwa kiwango ambacho makafiri wanastahili. Malaika hawa wenye kudhihirisha uadilifu mkubwa wa Mwenyezi Mungu, ni viumbe watakatifu ambao hutekeleza majukumu yao kwa ridhaa na unyenyekevu mkubwa kwa Mwenyezi Mungu.

ADHABU YA KIROHO HUKO JAHANNAM

Hadi hapa, sehemu kubwa ya adhabu zilizoainishwa ni zile za kimwili tu. Hata hivyo pamoja na adhabu hizi za kimwili pia zipo adhabu nyingine za kinafsi. Miongoni mwa hizo ni kujuta, kukosa matumaini, kusikitika, kuhisi kutendewa vibaya (kuonewa), kuadhirika na kukata tamaa. Hisia hizi huibuka kutokana na adhabu mbalimbali anazopata:-

Moto unaopenya hadi kwenye moyo

Kwa namna moja au nyingine, kila mmoja huonja adhabu za kiroho hapa ulimwenguni. Kwa mfano, kumpoteza jamaa yake wa karibu rafiki, mke au mume, mtoto au mtu ambaye ukaribu wake na mtu huyo humtegemea sana, husababisha majonzi katika moyo ambayo hayawezi kuelezeka. Majonzi haya kwa hakika ni aina maalum ya adhabu toka kwa Mwenyezi Mungu aliyoipandikiza katika moyo wa mtu kutokana na kumfanya kwake mtu huyo ni wa kutegemewa kutokana na kupotea kwake au kumuasi kwake Mwenyezi Mungu. Yampasa mwanadamu kudhihirisha mbele ya Mwenyezi Mungu hisia za mapenzi, kuridhika, kunyenyekea, kumuogopa, kumtegemea na urafiki wa hali ya juu. Kushindwa kufanya hivyo na badala yake kuyaelekeza haya kwa asiyekuwa yeye, ambaye pia ameumbwa na Mwenyezi Mungu na hivyo kuhitajia, kwa maneno mengine, humshirikisha na Mwenyezi Mungu na viumbe vyake, husababisha adhabu hii.

Waabudu masanamu pia huonja adhabu hii, hivyo kuweza kupata fundisho kutokana nayo, na hivyo hutarajiwa kuomba msamaha na kurejea kwa Mwenyezi Mungu kabla mauti hayajamkuta. Vipo viumbe vyengine ambavyo mwanadamu amevijengea dhana sawa na masanamu. Miongoni mwa hivyo ni kumiliki vitu, fedha, bahati, jeuri; kwa muhtasari, kitu chochote au dhana yoyote ambayo inaabudiwa kinyume na Mwenyezi Mungu yaweza kufanywa sanamu. Uchungu kwa kupoteza hayo masanamu ambayo huingizwa katika nyoyo za mmoja wao katika dunia hii ni kidogo kulinganisha na adhabu kali itakayowakabili watu katika jahannam. Kwa maana yake halisi, huwa ni onyo. Katika Jahannam, machungu yatakuwa ni halisi na yasiyo na ukomo yakiwasubiri walioabudu masanamu. Wakati mwingine hii adhabu ya kiroho inakuwa kubwa kiasi kwamba, mwingine angeomba adhabu ya kimwili kuliko hii.

Hata kujiua huchukuliwa ni ukombozi. Moto unaopenya hadi kwenye moyo'.

Adhabu kali itamthubutikia kila mwenye kuramba kisogo, msengenyaji. Ambaye amekusanya mali na kuyahesabu. Anadhani ya kuwa mali yake itambakisha milele. Hasha! Bila shaka atavurumizwa katika hutama. Na ni jambo gani litakalokujulisha ni nini hutama? Ni moto wa Mwenyezi Mungu uliowashwa. Ambao unapanda nyayoni. Hakika watafungiwa humo. Kwa magogo marefu marefu. (Humazali: 1–9).

Pia maumivu makali kupita kiasi katika dunia hii hutoweka, Mabaki yake yanaweza kusalia kwa muda, lakini muda huyafanya yatoweke yale makali yake ya wazi. Katika Jahannam, maumivu makali zaidi hupenya katika nyoyo za makafiri kama vile hasira na kubakia hivyo milele. Mbali na hili, adhabu ya kiroho hutoa hisia ambazo ni kati ya kukata tamaa na kufedhehesha, ghadhabu na bughdha. Adhabu za aina zote mbili, yaani za kiroho na kimwili zitasheheni huko Jahannam zikimsubiri kila aliyechupa mipaka ya Mwenyezi Mungu, kafiri.

ADHABU YA FEDHEHA

Aya nyingi zinazohusu motoni, zinatufahamisha kwamba adhabu za kudhalilisha na kufedhehesha zinawasubiri makafiri huko. Watapa adhabu hizi kutokana na jeuri na kujivuna kwao.

Katika dunia hii, moja katika malengo ya makafiri ni kuwafanya wengine wawatukuze na kufurahia hadhi zao katika jamii na utanashati wao. Fani za kipekee, watoto, ulimbwende, magari na vitu vingine vya kidunia huwa na maana zaidi endapo ndivyo vitakavyotangulizwa mbele yao. Hakika, katika Qur'an, kujitukuza kwa utajiri na vitu, vimeelezwa kama mapambo ya kidunia. Hii hali, hubadilika huko akhera na kuwa adhabu ikiwa ni kudhalilishwa pamoja na machungu ya kimwili. Hii ni kwa sababu, makafiri wanasahau juu ya 'Mwenyezi Mungu, mwenye kusifiwa' (*Al-Baqarah: 267*), na badala yake wakafanya matamano ya nafsi zao kuwa miungu yao:

'Je! Umemuona yule aliyefanya matamano yake, (kile anachokipenda), kuwa Mungu wake? Basi je, utaweza kuwamlinzi wale? (Al-furqan: 43).

Kwa sababu hii muda wake mwingi, umejishughulisha katika kuchuma, kushukuriwa na kusifiwa yeye Mwenyewe, kuliko kumsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu. Amejijengea katika maisha yake kupata furaha toka kwa watu badala ya kutafuta chumo la namna ya kukubaliwa na Mola wake. Hii ndio sababu inayompelekea mwanadamu huyu achukie mno kama atafedheheshwa mbele ya watu wengine.

Kitu kingine kinachomnyongesha kafiri ni kudhalilishwa na kutohaminiwa mbele ya watu. Wapo pia miongoni mwao ambao wengatamani afadhali kufa kwa ajili ya kutukuzwa kuliko kitendo cha kupuuzwa. Hali ya motoni imebeba ujumbe wa aina hii katika kiini chake. Hali hii ngumu ya wakazi wa motoni msingi wake ni kutokana na ujeuri wao. Kama kabla ya hapo hawakuwa wakipuuzwa. Aya nyingi zinathibitisha juu ya ukweli huu.

"Na siku watakapowekwa waliokufuru mbele ya moto. "Mlipoteza vitu vyenu vizuri katika maisha yenu ya dunia. Ninyi mlifurahisha navyo; leo mtapewa adhabu ya fedheha kwa sababu ya kule kujivuna kwenu bure duniani; na kwa sababu ya kule kuasi kwenu. (Al-Ahqaf: 20).

Wala wasidhani wale waliokufuru kwamba huu muda tunaowapa ni bora kwao. Hakika tunawapa muda na (inatokea ya kuwa) wanazidi madhambi (katika muda huo). Na itakuwa kwao adhabu ya kuwadhalilisha. (Al-Imran: 178).

Makafiri watakuwa katika maelfu ya aina mbalimbali za kushushwa hadhi. Na pengine chini zaidi kuliko hali iliyonayo wanyama hapa duniani. Nyundo za chuma, majambia na minyororo (makongwa pia). Kwa hakika, kudhalilisha ndio msingi mkuu wa adhabu zote za motoni. Kwa mfano, atakapokuwa anatumbukizwa motoni, atakuwa anashushiwa hadhi. Hali hii ya kupuuzwa huanzia

tangu pale kafiri atakapokuwa anafufuliwa na kuhukumiwa kuingia motoni. Zaidi ni kwamba adhabu haitapunguzwa. Miongoni mwa mabilioni ya watu, kafiri atachukuliwa na Malaika na kukamatwa kwa kisogo chake na miguu.

Katika maneno ya Qur'an:

'Siku hiyo hataulizwa mtu kwa dhambi zake wala jini... Watajulikana waovu kwa alama zake; basi watakamatwa kwa nywele zautosi na kwa miguu. (Al-Rahman: 39,41).

Katika moto, makafiri watakwenda kwa makundi kwa aina ya adhabu mbaya zaidi kuliko ile ya wanyama wanayopata hapa duniani. Kwa kukamatwa nywele za utosini, na kuburuzwa njiani kisha atakupwa motoni. Hali ya kushindwa kuzuia lolote, ataomba msaada, lakini wapi! Hakuna msaada wowote. Hali ya kukata tamaa itazidisha adhabu.

'Sivyo hivyo! Kama haachi tutamkokota kwa nywele za utosi. Utosini mwongo, wenye madhambi. Basi na awaite wanachama wenzake (wawasaidie). Na sisi tutawaita Malaika wa Motoni. Sivyo! Usimtii, lakini Sujudu na kuwa karibu (na Mwenyezi Mungu). (Alaq: 15 - 18).

Kama aya inavyobainisha; makafiri watakuwa:

'Siku watakayosukumwa katika moto wa Jahannam msukumo (wa nguvu) Na waambiwe huu ndio ule moto ambao mlikuwa mkiukadhibisha. (Attuur: 13 - 14).

Na pia watakuwa: **'Ama wale wanaokusanywa kifudifudi (wanaburuzwa kwa nyuso zao) mpaka katika Jahannam, hao watakuwa mahali pabaya, na wenye kupotea njia ya haki. (Al-Furqaani: 34).**

Hivyo hivyo: **'Na watakaoleta ubaya, basi zitasunukishwa nyuso zao motoni. (Waambiwe): "Hivi mnalipwa '(kwa mengine) mbali na yale mliyotenda)". (An-Naml: 90). "Siku watakayokokotwa motoni kifudifudi (na huku wanaambiwa) 'Onjeni Mguso wa Jahannam. (Al-Qamar: 48).**

Kudhalilishwa kunazidi mara baada ya kuingia motoni, Mbali na maumivu ya kimwili, maumivu makali yatakuwa ni hisia za kuona kuwa kudhalilika na kuona yu mtu wa chini:-

'Mkamateni mumtupe katikati ya Jahannam. Kisha mwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji ya moto. "Onja! Wewe ni Mwenye nguvu, Mheshimiwa! Hakika hii ndio ile mliyokuwa mkiitilia shaka (Ad-Dukhan: 47 - 50).

Katika kuwadhililisha makafiri, kumetayarishwa vifaa maalum; makongwa, minyororo vyote vitatumika.

'Mkamateni na mtieni makongwa. Kisha mtupeni motoni. Tena katika minyororo yenye urefu wa dhiraa sabini mwingizeni (mtatizeni). Hakika yeye alikuwa hamuamini Mwenyezi Mungu - Mtukufu. Wala hahimizi kulisha maskini. (Al-Haqqah: 30 - 34).

Katika ulimwengu huu, kabla wale waliokanusha waziwazi, hata wanyama hawafungwi minyororo. Na kwa wanadamu, ni wale tu ambao hawatendewi haki au watu hatari waliopungukiwa na akili (vichaa) ndio hufungwa minyororo au pingu. Hali ikiwa ndio hivi, wale watakaopelekwa motoni ndio watu wa chini zaidi kuliko wote. Ndio sababu wamefungwa katika 'minyororo isiyopungua dhiraa sabini' kama ilivyobainishwa katika aya hapo juu. Aya nyingine inaelezea tukio hili kwa undani zaidi namna linavyokusudiwa kumuonesha asi kuwa ni wa daraja la chini kabisa:-

'Zitakapokuwa pingu (makongwa) shingoni mwao na minyororo na wanaburuzwa, katika maji ya moto kisha wanaunguzwa motoni. Tena wataambiwa, 'Wako wapi mliokuwa mkiwashirikisha kinyume na Mwenyezi Mungu? ... (Al-Muumin: 71 - 74).

... Na kama unastaajabu (juu ya upofu wao), basi cha ajabu kabisa ni usemi wao: 'Je, tutakapokwisha kuwa udongo, kweli tutakuwa katika umbo jipya!' Hao ndio waliomkufuru Mola wao. Watu hao watakuwa na makongwa shingoni mwao. Watu hao ndio wa motoni, humo watakaa milele. (Ar-Raad: 5).

'Siku hiyo utawaona watenda maovu wamefungwa katika minyororo. Nguo zao zitakuwa za lami na moto utazijia nyuso zao. Ili Mwenyezi Mungu ailipe kila nafsi kwa yale aliyoyachuma. Hakika Mwenyezi Mungu ni mwepesi wa kuhesabu. (Ibrahim: 49 -51).' ...

'Basi wale waliokufuru watakatiwa nguo za moto na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yachemkayo. Kwa (maji) hayo vitayeyushwa vilivyomo matumboni mwao na ngozi zao (pia). Na kwa ajili yao marungu ya chuma. Kila mara watakapotaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa mumo humo na kuambiwa; 'Ionjeni adhabu ya kuungua.'" (Al-Hajj: 19 - 22).

Kusinyaa kwa nyuso zao na kuwa nyeusi ni moja ya dalili za kuwaonesha watu wa motoni watambulike. Katika dunia hii, unaweza kuwaona watu wasio na furaha au kuwa na huzuni kupitia nyuso zao. Kukosa thamani na kuwa katika daraja la chini. Aidha watu wa motoni wataonekana kama ilivyobainishwa katika aya ifuatayo:-

'Nyuso nyingine siku hiyo ni zenye kudhalilika (Al-Ghaashia: 2).

Mbali na aina mbalimbali za kudhalilisha zilizobainishwahadi sasa, tuzingatie kuwa kutakuwa na aina nyingine za adhabu zenye kudhalilisha huko Jahaanam. Katika Qur'an, neno 'dhalili' limetumika na mifano michache imetolewa ili kuliainisha. Hata hivyo, lazima izingatiwe kuwa hii ina maana kama ambavyo kwa namna yoyote isijifunge kwenye hiyo mifano michache iliyotolewa. Hisia zote, matukio yote yanayochochea udhalilishaji katika nafsi ya mwanadamu katika dunia hii imejumuishwa katika hii nadharia ya 'Udhalilishaji na yote inapatikana huko 'Jahannam'.

MAJUTO YASIYO KWISHA

Itakapofika wakati wa kufufuliwa, aliyekufuru, kwa uchungu kabisa atajua makosa aliyoyafanya. Majuto yanayotokana na makosa yake ambayo hana namna ya kuyaondoa humpa mtetemeko mbaya. Hali yake ya kukata tamaa itadhihirishwa na namna yake ya majuto. Wakati kafiri atakapokuwa anakabiliwa na matendo yake aliyoyafanya hapa duniani, atagundua kuwa hana muda tena wa kurekebisha mambo na hivyo kurejea hadhi yake aliyokuwa nayo. Bado atatamani apewe tena fursa ya kurejea dunia. Kwa mtazamo huu, atatamani kurejea katika maisha ya dunia ili arekebisha makosa aliyoyafanya. Wakati huo huo hatapenda kuwatazama jamaa na marafi zake waliokuwa wakifurahia wote maisha. Urafiki na Ujamaa mizizi yake itakuwa imekatwa wakati huo. Mtindo wa maisha na utamaduni wa watu waliokuwa nao, nyumba zao, magari yao, wake au waume, watoto, makampuni, itikadi walizokuwa nazo wakizitangaza zitakuwa hazina thamani. Jambo jepesi ni kuwa vyote vimebadilishwa na adhabu. Hali ya kutisha itakayokuwepo siku hiyo inabainishwa katika aya zifuatazo:-

'Na ungeona watakavyosimamishwa kwenye moto, wakawa wanasema "Laiti tungerudishwa (ulimwenguni); wala hatutakadhibisha (tena) aya za Mola wetu, na tutakuwa katika wanaoamini." Bali yamewadhihirikia walivyokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangelirudishwa bila shaka wangeparudia yale waliyokatazwa, na bila shaka hao ni waongo. Na walisema 'Hakuna maisha ila maisha ya dunia; wala sisi hatutafufuliwa.' Na ungeona siku ya kiama watakavyosimama mbele ya Mola wao, akawaambia "Je! Si kweli haya?" Na wao wakasema "Kwa nini? Tunaapa kwa jina la Mola wetu." Aseme (Mwenyezi Mungu) 'Basi onjeni adhabu kwa kule kukanusha kwenu - (Al-an'am: 27 - 30).

WANAVYOANGALIWA WATU WA MOTONI

Hadhi na vyeo miongoni mwa waja hapa duniani ambavyo huwa vinapewa uzito mkubwa, hupoteza thamani katika Jahannam. Hali ambayo watakuwa nayo viongozi na wafuasi wao itakuwa ni ile ya chini kabisa kiasi cha wao kwa wao kupeana laana.

'Wakati wale waliokuwa wakifuatwa watakapowakana wafuasi wao, na wamekwisha iona adhabu, na maungano kati yao yamekatwa, wale waliowafuata watasema;

"Kama tungepewa fursa nyingine,tungewakana kama wanavyotukanusha." Namna hiyo, Mwenyezi Mungu anawaonesha vitendo vyao kama sababu (au chanzo) cha kuadhibiwa na kupuuza kwao. Kamwe hawataweza kutoka motoni.(Al-Baqarah: 116 - 167).

Watasema katika siku ambayo vichwa vyao vitavingirishwa katika moto kama tungemtii Mwenyezi Mungu na tungemtii Mtume.' Na watasema 'Mola wetu tuliwatii viongozi wetu na watu wakubwa na wametupoteza kutoka katika njia iliyonyooka. Mola wetu! Wape adhabu mara mbili na walaani mara nyingi! (Al-Ahzab: 66-68).

Wakibishana wenyewe kwa wenyewe watasema:

'Naapa kwa Mwenyezi Mungu, tulipotezwa Wakati tuliokulinganisha wewe Mola wa Ulimwengu (na vijiungu wa kubuni). Ni waovu pekee waliotupoteza na sasa hatuna wa kutuombea, hatuna hata rafiki mmoja muaminifu. Na kama tungekuwa na fursa nyingine bila shaka tungekuwa miongoni mwa waumini.' Kwa hakika muna humo dalili, lakini wengi katika watu hawaamini. (Ash-Shu'ara: 96-103).

Miongoni mwa watu wa motoni wanaokabiliwa na adhabu ya milele, kusimangana kutaibuka. Kila mmoja akimlaumu mwingine yeyote. Waliokuwa marafiki katika maovu wataanza kuhojiana wao kwa wao. Chanzo kikubwa cha kuogopana huko ni urafiki walioujenga huku duniani. Walishajihishana kila mmoja kufanya maovu na kupeana ujasiri wa kukanusha. Nadharia au mitazamo yote inayohusiana na urafiki umepotea katika uso wa Jahannam na mishikamano yote iliyoimarishwa duniani imetoweka na kuvunjika. Katikati ya kundi hilo kubwa la watu, bado kila mmoja yuko peke yake akiwalaani wote waliobaki:-

"Atasema (Mwenyezi Mungu), 'Ingieni motoni pamoja na umma zilizopita kabla yenu; za majini na watu.' Kila utakapoingia Ummah, utawalaani wenzao. Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa nyuma wao watasema kwa ajili ya wa kwanza wao, 'Mola wetu! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya moto mara mbili (maradufu)". Atasema; 'Itakuwa kwenu ninyi wote mara dufu, lakini ninyi hamjui tu. Na wa kwanza wao watasema kuwaambia wa nyuma yao: 'Basi ninyi pia hamkuwa na fadhila kuliko sisi. Kwa hivyo onjeni adhabu kwa sababu ya yale mliyokuwa mkiyachuma. (Aaraf: 38 - 39).

Na wale waliokufuru watasema(katika kutiliana chonza). 'Mola wetu tuoneshe wale waliotupoteza miongoni mwa majini na watu ili tuwaweke chini ya miguu yetu, wapate kuwa miongoni mwa walio chini kabisa (Fusilal/Ha mim Sajdah: 29).

Na (wakumbushe) watakapobishana katika moto huo -wakati madhaifu watakapowaambia wale waliojitukuza, 'Kwa yakini sisi tulikuwa wafuasi wenu, basi Je, mnaweza kutuondolea sehemu kidogo ya moto? Watasema wale waliokuwa wakijitukuza, 'Sisi sote tumo humu; Mwenyezi Mungu amekwisha hukumu baina ya vumbe - (Al-Muumin: 47 - 48).

'Hili ndilo jeshi litakaloingia pamoja nanyi.' Hapakupata mahala pazuri pa kufikia, hakika wao wataingia motoni.' Waseme (hawa wanaosimangwa). 'Lakini ninyi ndio wa kuambiwa namna makaribisho mema! Ninyi ndio mliotusababishia adhabu. Mahala pabaya kabisa hapo.' Waseme (waliokuja nyuma). Mola wetu! Waliotusababishia haya wazidishie adhabu mara mbili huku motoni' Watasema, 'Imekuwaje! Mbona hatuwaoni wale tuliokuwa tukiwahisabu kama waovu? 'Je tuliwafanyia mzaha? Ila macho yetu hawayaoni tu?" Bila shaka haya ya kuhasimiana watu wa motoni ni kweli. (Sad:59 - 64).

KUTAKA KUSAMEHEWA BAADA YA KUKATA TAMAA NA KUKOSA MATUMAINI

Watu wa motoni wamo katika hali ya kukata tamaa kabisa. Adhabu wanazopata ni ngumu mno na hazikatiki. Matumaini yao pekee ni kulia na kuomba waokolewe. Watawaona watu wa peponi na kuwaomba maji na chakula. Watajaribu kutubu na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, juhudi zote hizi zitaambulia patupu.

'Watawaomba walinzi wa motoni: Watataka pia walinzi wa motoni wawe watu wa kati (Mawakala) kati yao na Mwenyezi Mungu na kuwaombea Rehema yake, Mateso humo ni makali, hayavumiliki kiasi kwamba watataka waokolewe japo kwa siku moja tu.

Na wale walio motoni watawaambia walinzi wa Jahannam, 'Muombeni Mola wenu atupunguzie (alau) siku moja ya adhabu.' (Walinzi) wawaambie'Hawakukujieni mitume wenu kwa hoja zilizo wazi? Waseme. 'Kwa nini?" Wawaambie 'Basi ombeni, na madua ya makafiri hayawi ila ni ya kupotea bure'. (Al-Muumin: 49 - 50).

Makafiri watazidi kujaribu kuomba msamaha, lakini bila huruma, hawapatilizwi, wanahangaka:

Watasema, 'Mola wetu! Tulizidiwa na ubaya wetu na tukawa watu wenye kupotea. Mola wetu! Tutoe humu motoni, na kama tutarejea tena katika maovu bila shaka tutakuwa madhalimu. Atasema, 'Hizikeni humo. Wala msiseme nami' Bila shaka kulikuwa na kundi katika waja wangu lilisema: "Mola wetu! Tumeamini, basi tusamehe na uturehemu, nawe ndiwe mbora wawanao rehemu.' Lakini ninyi mliwafanyia stihizai hata wakakusahaulisheni kunikumbuka. Na mlikuwa mkiwacheka. Hakika leo nimewalipa (pepo) kwasababu yakusubiri kwao. Hakika hao ndio waliofuzu. (Al-Muuminuun: 106 - 111).

Kwa hakika haya ndio mawaidha ya mwisho ya Mwenyezi Mungu kwa watu wa motoni. Maneno yake, 'Bakini humu hali ya kuwa ni wenye kupata hiziya na msizungumze nami', ni hitimisho. Kutoka hapo na kuendelea, Mwenyezi Mungu hatawafikiria tena. Watu pia hawapendi kufikiria suala hili.

Wakati waovu wanaungua motoni, wale waliofikia daraja la furaha na Uokovu' wanabakia peponi milele wakifurahia matunda yasiyokwisha waliyopewa na Mola wao. Mateso ya watu wa motoni yatakuwa makali kiasi kikubwa pindi watakapotazama maisha ya watu wa peponi. Kwa hakika, wakati wamo katika adhabu isiyovumilika, wanaweza kutazama furaha ya ya hali ya juu na rehema zilizopo peponi.

Waumini ambao makafiri waliwadharau katika ulimwengu huu, sasa wanaendeleza utimilifu wa furaha, wakiishi sehemu tukufu, nyumba za thamani, wanawake warembo na vyakula na vinywaji vitamu. Hali ya waumini iliyo ya amani na vikorombwezo vyake inazidisha udhalili wa kuwa motoni. Mazingira haya yanaongeza machungu makubwa na majuto kwa adhabu iumizayo.

Majuto huja zaidi na zaidi. Kuacha kufuata maamrishi ya Mwenyezi Mungu hapa duniani huwafanya wajione kuwa wao ni wenye majivuno katika sehemu waishiyo akhera. Watawageukia watu wa peponi na kujaribu kuzungumza nao. Wataomba msaada na huruma toka kwao. Lakini, hizi ni juhudi zisizo na matunda. Watu wa peponi nao watawaona watu wa motoni. Majadiliano baina ya watu wa peponi na wale wa motoni yataendelea kama ifuatavyo:-

'Katika mabusatni watawauliza watu wabaya; 'Ni nini kilichokupelekeni motoni?'
Watajibu: Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakiswali. Wala hatukuwa tukilisha maskini. Na tulikuwa tukizama (katika maasi) pamoja na waliokuwa wakizama. Na tulikuwa tukikadhibisha siku ya hukumu. Mpaka mauti yatatujia. Basi hautafaa uombezi wa waombezi (Al-Mudaththir: 40 - 48).

Katika wakati huu, Waumini na wanafiq watabishana kundi moja dhidi ya jingine. Wanafiq ni wale wanaobaki na waumini kwa kipindi fulani tu. Mbali na kukosa imani katika nyoyo zao, na kwa sababu ya maslahi yao binafsi wanatekeleza baadhi ya shughuli za kidini kama vile ni waumini. Hivyo wanavuna chumo la kuwa kwao 'Wanafiq.' Na katika Jahannam, wanaomba waumini wawasaidie. Majadiliano kati ya makundi haya mawili yameinishwa kama ifuatavyo:

'Siku watakaposema wanafiq wanaume na wanafiq wanawake kuwaambia waumini, 'Tungojeeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.' Waambiwe (kwa shihizai) 'Rudini nyuma mkatafute nuru yenu.' Utiwe ukuta baina yao wenye mlango ndani yake mna rehema na nje kwa upande wake wa mbele kuna adhabu. Watawaita 'Je hatukuwa pamoja nanyi?' Watawajibu, 'Ndio, walakini ninyi mlijitia wenyewe katika ukafiri, mkangojea, mkajitia katika shaka na matamano ya nafsi yakakudanganyeni hata amri ya Mwenyezi Mungu ikaja. Na

mdanganyaji amekudenganyeni kuhusu Mwenyezi Mungu. Basi leo hakitapokelewa kwenu kikomboleo wala kwa wale waliokufuru. Makazi yenu ni motoni; ndio kunako kustahikieni; nayo ni marejeo mabaya kabisa. (Al-Hadid: 13 - 15).

ADHABU ITAKAYOENDELEA BILA YA KUOKOLEWA

Mbali na hali zote hizi za adhabu ya Jahannam iliyokwisha elezwa hadi sasa, kuna namna nyingine ya kuzidisha machungu ya adhabu inayotolewa, nayo ni hii ya 'kudumu.' Hapa ulimwenguni, ukweli ni kwamba, hata machungu au maumivu makali kiasi gani hupungua jinsi muda unavyoendelea, Hutoa faraja kwa mwanadamu. Mwisho wa kila machungu ni faraja na hata kusubiri faraja hiyo hutoa matumaini. Lakini, kwa upande wa Jahannam, matumaini kama hayo hayapo. Na hili ndilo linaloumiza watu wa motoni zaidi. Wakati watakapotupwa motoni, wakafungwa minyororo, wakawekewa makongwa, kupigwa na kukusanywa katika sehemu zilizokuwa nyembamba, mikono yao ikiwa imefungwa shingoni mwao, wanajua kuwa hali hiyo itadumu milele. Jaribio lao la kutaka kujiokoa kamwe halitafanikiwa. Hii inaonesha kuwa adhabu yao itaendelea milele. Hali inayowakabili inaelezwa kama ifuatavyo:-

'Kila mara watakapotaka kutoka humo kwasababu ya uchungu, Watarudishwa mumo humo. 'Onjeni adhabu ya kuungua." (Al-Hajj: 22). Jahannam ni sehemu iliyotengwa kabisa. Makafiri wataingizwa humo na kamwe hawatatolewa. Hakuna njia ya kutokea. Hali ya kuona kuwa wamezingira itawadhihirikia makafiri. Wanazunguukwa na kuta zilizo na milango iliyofungwa kwa makufuli. Hali hii chungu wanaohisi ya kuzingirwa inaelezwa katika Qur'an kama ifuatavyo:-

'Lakini waliokanusha aya zetu, hao ndio watu wa upande wa shari. Moto uliofungiwa utakuwa juu yao. (Balad: 19 - 20).

'Na sema huu ni ukweli uliotoka kwa Mola wenu, basi anayetaka na aamini na anayetaka na akufuru. Hakika tumewaandalia madhalimu moto, ambao kuta zake zitawazunguuka. Na wakiomba msaada, watasaidiwa kwa kupewa maji kama ya shaba iliyoyeyushwa itakayoziunguza nyuso zao. Kinywaji kibaya kilioje hicho. Na mahala pabaya palioje. (Al-Kahf: 29). 'Hao mahali pao ni Jahannam, wala hawatapata makimbilio ya kutoka humo. (An-Nisaa: 121).

Wakati makafiri watakapouona moto, watafahamu dhahiri shahir mahali watakapokuwa. Watatambua wazi kuwa hakuna njia yoyote ya kutokea humo. Katika hatua hii, dhana ya muda itakuwa haina maana, na adhabu ya milele inaanza. Uhalisia wa maumivu na mateso ndio hali halisi huko. Hapo itapita miaka mia, elfu au mamilioni, bado mja hajakaribia ukomo. Miaka milioni moja haina maana

mbele ya milele. Wakazi wa motoni watasubiri mwisho, lakini ni tamaa isiyo na pakushika. Ndio maana umilele wa Jahannam unasisitizwa mno:-

'Mwenyezi Mungu amewaahidi wanafiqi wanaume na wanafiq wanawake na makafiri moto wa Jahannam kukaa humo daima. Huo unawatoshia, na Mwenyezi Mungu amewalaani; nao wana adhabu itakayodumu. (At-Tauba: 68).

Lau kama hawa wangukuwa Mungu wasingeifikia (hiyo Jahannam). Na wote humo watakaa milele - (Al-Aniyaa: 99).

Na wale waliokufuru, watakuwa katika moto wa Jahannam, hawatahukumiwa kufa wala hawatapuguziwa adhabu yake. Hivi ndivyo tunavyomlipa kila asiye na shukurani. (Fatir: 36).

Machungu yote hapa duniani yana tamati. Muda wote kunakuwepo kuokolewa. Yeyote anayeathirika kutokana na machungu ama anakufa, au machungu yake yanapunguzwa. Lakini, Jahannam maumivu yanaendelea bila kupunguzwa, bila kutoa tahafifu japo kwa sekunde chake.

KUMBUSHO MUHIMU ILI KUEPUKA ADHABU

Katika kitabu chote hiki, imesisitizwa kwamba wale wanaozikataa amri za Mwenyezi Mungu, Mola wao, katika ulimwengu huu na wakakanusha juu ya kuwepo kwa Muumba hawatakuwa na ukombozi kesho Akhera. Na kwamba watakabiliana na adhabu yenye kutisha huko Jahannam.

Hivyo basi, bila ya kupoteza muda, kila mmoja anaweza kutambua hali yake mbele ya Mwenyezi Mungu na kujisalimisha kwake. Kinyume chake atajuta na kukutana na mwisho wenye kuogofya.

Mara nyingi wale waliokufuru watatamani lau wangelikuwa Waislamu. Waache wale na wafurahi na liwadanganye tumaini lao la Uongo. Karibuni hivi watajua. (Al-Hijr: 2 - 3).

Njia ya kuepuka adhabu ya milele, njia rehema ya milele na kufikia kukubaliwa na Mwenyezi Mungu kuko wazi.

Kabla hujachelewa, kuwa na imani ya kweli. Tumia muda wako kwa kufanya mema ili upate radhi yake.